# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# CKRC

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

## BURA CONSTITUENCY, HELD AT BURA - TANA SECONDARY SCHOOL

**ON**

**THURSDAY, 6TH JUNE 2002**

.

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARING AT BURA CONSTITUENCY, BURA-TANA SECONDARY SCHOOL ON 6TH JUNE 2002.**

**Present:**

Com. Prof. Idha Salim
Com. Mutakha Kangu

**Secretariat staff in attendance:**

| | |
|---|---|
| Triza Apondi | Programme Officer |
| Metrine Wakhungu | Assistant Programme Officer |
| Lydia Moraa | Verbatim Recorder |
| Omar Dhato | District Coordinator |

**Com. Mutakha Kangu:** Nafikiri tuanze mkutano kwa sababu inaenda na hatutaki kuwaweka watu. Tungeomba kama hatujaanza kama mmoja wenu anaweza kutuongoza kwa maombi, halafu tufungue mkutano.

**Prayer:** Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mungu wa rehema, tunashukurani kwake Allah, Mola wa ulimwengu wote, mwingi wa rehema, mwenye kurehemu. Mfalme wa siku ya mwisho, ni wewe tunakuomba na ni wewe tunakuabudu.
Ewe Mola, utuongoze kwa njia ya haki, sio kwa njia ya waliopotea, au waliokasarika. Amani ya Mwenyezi Mungu iwe juu yenu nyote.

**Com. Mutakha Kangu:** Tukianza mkutano, kwanza ningependa tujijulishe kwenu, ndiyo mjue ni akina nani wako na nyinyi leo na nitampa mwenzangu nafasi ajijulishe kwenu ndiyo tuendelee.

**Com Idha Salim:** Asante sana Commissioner John Mutakha Kangu. Asalaam Aleikum. Mimi jina langu ni Ahmed Idha Salim, ni mwanatume na pia ni Naibu wa Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Katiba. Na nimefurahi sana kuwa tumefika hapa Bura, kwa minajili ya kupokea maoni yenu juu ya kurekebisha Katiba. Asanteni.

**Com. Mutakha Kangu:** Na mimi ninaitwa Mutakha Kangu, mimi ni mmoja wa wanatume na nikiandamana na Professor tutasikiza maoni yenu leo. Nawarudishia shukrani kwa kuchukua jukumu la kuja hapa. Juzi nilikuwa hapa tukichukua maoni huko Hola, Ruenje na huko Garsen na leo tena nimepata nafasi ya kurudi hapa Bura na tusikie watu wa Bura watasema namna gani.

Pamoja na sisi kuna maofisa wa Commission. Huyo ni Moraa, kuna Apondi, Kuna Wakhungu, wanatusaidia.

Siku ya leo tuko mbele yenu tuwasikize nyinyi si sisi tuwazungumzie. Nyinyi ndio mtazungumza, nasi tutasikiza, tuchukue maoni yenu, mnataka katiba ya aina gani.

Na kama hatujaanza, tuna mambo twataka kutaja kwenu ndiyo muelewe ndiyo tujue utaratibu tutakuwa tunafuata.

Kwanza, maoni inaweza kuja kwa njia tatu. Njia ya kwanza ni maandishi; unaweza kuwa umetengeneza maandishi, ile tunaita memorandum na utake kupeana hiyo memorandum ama hayo maandishi bila kuongezea mambo yoyote ya kuzungumza. Na ikiwa ni hivyo ndiyo ungependelea, unapeana hapo pole pole, unaandikisha jina lako, unaweka sahihi na kama uko na shughuli ingine unataka kwenda kufanya, unatoka polepole na unaenda, hatutakuweka ukingojea.

Njia ya pili, unaweza kuwa na maandishi, na pia utake kuongezea hayo maandishi, ama kuelezea hayo maandishi, ukimulika yale maneno makubwa makubwa kwa maandishi yako. Ukiwa unataka kupeana maoni yako kwa njia hiyo, utakuja hapa mbele na uzungumzie, upeane hayo maandishi, umulike yale maneno na ukimaliza unapeana maandishi hapo, unaweka sahihi.

Ikiwa unafuata njia hiyo, tutakupatia dakika tano ya kumulika mambo yenye yako kwa maandishi yako.

Njia ya tatu, unaweza kuwa hauna maandishi yoyote, lakini uko na mambo kwa kichwa yako, kwa roho yako, ungependelea kuzungumza, oral submissions. Utakuja hapa, tutakupatia dakika kumi uelezee maneno yako na ukimaliza jina lako litaingizwa kwa register yetu na uweke sahihi.

Na kwa kufuata hizo njia zote, sana sana zile za mwisho mbili, sisi wanatume tunaweza kuwa na swali la kukuuliza kufafanua mambo yenye umezungumzia. Tunaweza weka hayo maswali na wewe utujibu. Lakini ukipata ni mambo haukuwa umefikiria, hauna majibu, tena unaweza tuambia sikuwa nimefikiria hayo na tutawachia hapo.

Jambo la pili ni kwamba, lugha tunatumia kwa Tume, kwanza kama unataka kuzungumza ukitumia lugha ya Kiingereza, tutakubali, ukitaka kutumia lugha ya Kiswahili, tutakubali, na hata ukitaka kutumia lugha ingine yoyote, ya kinyumbani, ya kimama, tutakubali, lakini utujulishe ndiyo tuweze kujua ni nani anaweza kutusaidia kutafsiri yale utakuwa unazungumza. So uko huru, mtu asiende akisema ningezungumza lakini walikuwa wanatumia lugha siwezi kuelewa. Uko na ruhusa ya kutumia lugha yoyote, na unatuambia tunajua tutafanya namna gani.

Kwa hivyo tutaanza na tunafuata ile list. Watu wakiingia wanaandikisha pale, so tunafuata hiyo list, tuhakikishe watu wanaitwa kulingana na wakati waliingia.
Isipokua tunasema, kwa sababu huu mradi tunataka tuhusishe watu wote; wazee, wamama, vijana, walemavu. Saa zingine tunawezafika kiwango tuone kuna wale watu wanahitaji watumikiwe kwa haraka, tunawezawaita. Kama wazee ama walemavu, saa zingine wamama wanataka kwenda kwa haraka, saa zingine tunaweza ruka list tuite mtu mwingine, lakini kwa sasa mimi ninaona watu hawajaingia wengi, tutaenda na list vile tumepatiwa, ndio tuone itakuwa namna gani.

Tuanze na mwenzetu anaitwa Adan Khalid. Na ukianza kuzungumza, kwa sababu tunanasa maneno unazungumza kwa hii machine, unaanza na kutaja jina lako ndilo nalo linaswe kwa hii machine, wakati tutakuwa tunasikiza tunajua huyu ni fulani. So, unaanza na kutaja jina lako. Asante.

**Adan Khalid:** Mimi kwa jina naitwa Adan Siad lakini kabla sijaanza ningependa kuwauliza swali moja. Kulingana na vile nimeelewa, mlitupatia dakika tano kila mtu kuweza kuongea. Sasa iwapo mtu yuko na maoni chungu nzima na nyinyi mmepeana muda kidogo namna hiyo, itakuwa namna gani sisi kutoa maoni yetu yote?
Kwa hivyo tunataka tuongezewe muda. Mtu atoe maoni mpaka wakati atamaliza maoni yake. Hiyo ndiyo kwanza ninaomba.

**Com. Mutakha Kangu:** Tutaaangalia kulingana na wingi wa watu. Sababu tunasema hivyo ni kwamba kuna sehemu fulani unapata watu wengi na kila mtu lazima anataka azungumze machache. Saa zingine unafika kiwango unapata wengi wanarudia yale wengine wamezungumza.
Kama ile siku nilikuwa Hola, tulianza mkutano saa tatu na tulimaliza saa kumi na mbili jioni bila break yoyote na tulikuwa bado tuna watu saba hatukuwa tumewasikiza. So kwa sababu watu hawajaingia kuwa wengi, tutakuwa tunaangalia. Kama tunaona bado hakuna watu wengi, tunaweza kupatia nafasi uelezee mambo yako sawa sawa. Na ndiyo tulisema ikiwa uko na memorandum, kwa sababu utatupatie utatupatia twende tusome yote, saa zingine inakuwa hakuna haja ya wewe kuisoma yote mbele but kwa sababu watu hawajakuwa wengi, tunaweza kupa wewe muda kidogo uelezee ndiyo uone mambo yako umepeana yote.
So, usiwe na wasiwasi.

**Adan Siad:** Mimi nikianza, muundo wa Katiba tunayoitaka: Kwa maoni yangu ni kuwa tungetaka ya kuwa Katiba yetu hii itangulizwe kwa jina la Mwenyezi Mungu. Katiba yetu isianze kama vile Katiba yetu ya mbeleni ilikuwa inaanza tu na

kuendelea.
Tutangulize jina la Mwenyezi Mungu ndiyo Katiba iwe nyuma.

Halafu Katiba yetu iwe ni Katiba inayowajali au kuwashughulikia wanyonge, watu wasiojiweza kwa sababu Katiba ya awali haikuwa inashughlikia wale ambao hawajiwezi.

La pili: Katiba yetu iwe ni Katiba ambayo inajali makabila madogo madogo. Katiba yetu ya awali ilikuwa haijali ama haishughulikii ama haiwatambui makabila madogo madogo. Hiyo ndiyo muundo wa Katiba tunayoitaka.

Kuhusiana na mambo ya ardhi: Tungependa serikali yetu ya wilaya, tunaomba serikali yetu, inyime haki serikali ya wilaya kutoa ardhi yetu ama sehemu yetu ya ardhi kiholela holela kwa minajili ya kijinufaisha, kwa kuwapa watu, yaani kuchimba mawe ama kukata miti ama kuchoma makaa. Jukumu kama hilo lipewe wananchi wenyewe ili wao wajinufaishe nao.

Tungependa pia serikali iwatolee fidia wakaaji wa manyatta kama vile temporary shelters kama vile inavyotolea fidia wakaaji wengine, iwapo barabara au shughuli nyingine itafanya hiyo manyatta kuhamishwa. Wananchi waregeshewe sehemu yao waliopokonywa.

Tena tunaomba wananchi waregeshewe sehemu yao ya ardhi waliopokonywa na serikali, kama vile Ghalana Game Reserve, Kora Game Reserve, Mchalelo Game Reserve, Bura irrigation scheme and settlement project na Hola irrigation scheme. Haina manufaa yoyote kwa wananchi kwa hivyo warudishiwe sehemu zao za ardhi.

**Com. Kangu:** Yaani the schemes isahauliwe?

**Mr. Siad:** Isahauliwe, irudishiwe wananchi kwa sababu haina manufaa yoyote kwa wananchi.

Serikali itulipe fidia sisi wakaaji wa bure kwa kuleta janga la Mathenge ambalo limeleta maafa mengi sehemu zetu. Zimeua mifugo mengi sehemu zetu, hata mvua ikinyesha namna gani utakuta sehemu yetu haimei nyasi hata kidogo.

**Com. Mutakha Kangu:** Sababu yake ni nini?

**Mr. Siad:** Kwa sababu ya Mathenge, miti ya Mathenge ambayo imeletwa na serikali kwa hivyo serikali yenyewe itulipe fidia na licha ya kutulipa fidia, iwe ni jukumu lao kuondoa Mathenge.

**Com. Idha Salim:** Mathenge iondolewe kabisa?

**Mr. Siad:** Ndiyo, iondolewe kabisa.

**Com. Idha Salim:** Kwa hiyo nyasi itaanza kupata uhai?

**Mr. Siad:** Tunatumai ya kuwa itatutosha.

Tuje kwa elimu sasa: Serikali itulipe fidia sisi kama wafugaji kwa sababu ya kuwacha jamii ya ki-Orma kutosoma ilhali ni jukumu la serikali kuhakikisha imeondoa tatizo la kutojua kusoma na kuandika. Unakuta kwamba sehemu kama hii yetu ya Bura ama sehemu yetu ya Tana River hakuna mahali hata moja ambayo wafugaji wamejengewa shule yao. Hizi shule mnaziona ni shule zimejengwa kuwanufaisha watoto wa wakulima.
Kwa hivyo tunaomba serikali na tunasema serikali itulipe fidia na licha ya kutulipa fidia, litujengee shule. Ni jukumu lao.

Lifanywe kosa sawa na kuuwa iwapo mzazi hatampeleka mtoto wake shuleni. Hii serikali kupitia kwa ma chief na manaibu wao, ifanye hii sheria moja muhimu na ifuatwe kama jambo la kidharura kwani jamii yetu ya ki-Orma hawatasoma iwapo hii sheria italegezwa au haya maoni hayatazingatiwa, hivyo wabaki katika hali ya aibu ya kuhuzunisha.

Kwa hivyo licha ya serikali kutujengea shule, tuwe na sheria ya kuwa iwapo mtu amemuua mtu, hukumu yake itakuwa ni kunyongwa. Jamii yetu ya ki-Orma, ikiwa mtu hatapeleka mtoto wake shule afadhali auawe. Na hii sheria serikali izingatie kabisa. Ikiwa mtu ambaye hakupeleka mtoto wake shule anafungwa miaka kadhaa, basi awe amefungwa miaka hizo kadhaa.

Kama national cake ni mfano wa national schools, basi mtoto wa ki-Orma pia apewe nafasi ya kusoma katika national schools kwani ni vigumu watoto wetu kwenda chuo kikuu kupitia sehemu yetu hii ambayo hatuna mashule na walimu. Hivyo kila kabila wapewe asilimia fulani ya nafasi ya kusoma katika national schools, hivyo mmoja wa watoto wa ki-Orma waweze kuingia chuo kikuu kila mwaka.
Iwapo tumenyimwa hii nafasi basi serikali imetudhulumu.

Tungependa pia serikali ianzishe nomadic boarding schools. Sehemu yetu ya Tana River hakuna nomadic boarding schools hata moja. Ikiwa sehemu zingine wafugaji, sehemu kama North Eastern ama zingine unapata kuna nomadic boarding schools ndiposa unakuta watoto wetu wafugaji hawakusoma kwa hivyo ni serikali wametunyima hiyo. Hata sisi ni watu kama wengine.

Hatua ya serikali ya kuwaajiri waalimu isitumike kwa jamii ya wafugaji kwani bado wako na tatizo la waalimu. Hii ichukuliwe kama hatua muafaka ya kuhakikisha wamesoma. Sisi bado hatuna watu ambao wanaweza kutufanyia kazi ya ualimu. Tuko na tatizo ya ualimu. Hatuna watoto wamesoma.
Kwa sababu hiyo tungependa serikali jambo la kusema hawataajiri waalimu sijui nini, hiyo kwetu isitumike mpaka wakati tutakapopata waalimu sehemu zetu, ambao ni watu wametoka kwetu, watu wetu hasa wafugaji.

Aina ya serikali: Tungetaka serikali ya kirais, itakayo kuwa na Bunge mbili. Nyumba moja ya Bunge ishughulike na wananchi wote wa Kenya, yaani wananchi, wachaguliwe kulingana na uwingi wa watu.
Nyumba ya pili iwe ni ya special interest groups, yaani makabila madogo madogo na watu wasiojiweza. Nyumba ya pili iwe ikishughulikia watu kama hao.

Watu wachaguliwe kulingana na makaazi: Kama kwa mfano wizara hii ya mifugo kuchaguluiwe mtu mfugaji kwa sababu mtu mkulima ambaye anawekwa katika wizara ya mifugo hawezi jua faida ya mifugo ni nini. Ndiposa unakuta wafugaji wanatatizika kwa sababu mtu anawekwa pale, yeye mwenyewe si mfugaji, hajui tatizo la mfugaji nini, hajui mifugo taabu yake ni nini, hataki kujali maslahi ya wafugaji. Kwa hivyo kama ni Ministry ya mifugo, mtu ambaye atakuwa anaisimamia hiyo wizara awe ni mfugaji.

Kuna projects kama drought recovery na arid lands ambayo sehemu yetu ya Tana River iko. Hii project imeletwa ili kuwasaidia wafugaji na jambo la ajabu ni kwamba inasimamiwa na mkulima ambaye hajui tatizo la mfugaji. Ndiposa watu wetu saa hii wakiulizwa kama kuna kuna drought recovery project hapa ama arid land hapa, hata hawajui drought recovery nini na serikali imeleta hii project ili kunufaisha wafugaji. Kwa hivyo tunataka project kama hizi isimamiwe na wafugaji wenyewe.

Ibuniwe ofisi ya Ombudsman: Iwe ni ofisi ambayo itakuwa inashughulikia malalamishi ya watu, wananchi wa Kenya.

Citizen counsel, yaani, mawakili wa kutetea raia: Siku hizi unakuta wale mawakili tuko nao ni mawakili wa serikali. Mwananchi yule mnyonge ambaye hawezi akawa na wakili wake anatatizika hata akiwa na haki gani. Kwa hivyo tuwe na mawakili wa kushughulikia wananchi.

Afya na mambo mengineo: Tunaomba serikali ianzishe dispensaries katika sehemu ya wafugaji. Unakuta sehemu yetu ya Tana River district, hakuna sehemu hata moja iliyo na dispensary ambayo imechengewa wafugaji. Hizi hospitali ambayo tunaona hapa ni hospitali zimejengwa 1980s na zimechengwa ili kuwasaidia wakulima. Kwa hivyo kuna sehemu kama Sabukia, kama Wolesorea, kuna sehemu kama Woldena Titila, ambayo ni sehemu ya wafugaji, hakuna dispensary hata moja. Kwa hivyo ni jukumu la serikali na tunaomba watujengee dispensary.

Tunaomba serikali ipige marufuku madaktari ambao wanafanya kazi ya serikali kuwa na mahospitali zao, clinics zao nyumbani. Unakuta ya kwamba mwananchi wa kawaida akigonjeka, akija hospitali, anaandikiwa dawa, anaambiwa aende kwa hospitali fulani, ya mtu binafsi na kumbe hospitali hiyo ni ya huyo daktari ambaye amekuadikia dawa. Sasa hospitali ya serikali sijui inafaidi nini. Kama mtu anafanya kazi ya serikali, ni daktari, tungependa ipigwe marufuku yeye kufungua hospitali yake.

Tunaomba serikali ya kuwa mkuu wa tarafa, yaani D.O, asihusike katika kamati ambayo inashughulikia kutoa kitambulisho.

Unakuta sehemu hii yetu ya kwamba mtu ametoka Somalia, saa hii utampata aliye na kitambulisho lakini yule mzaliwa wa hapa hana kitambulisho. Kwa sababu gani? Yule mzaliwa hayuko tayari kutoa pesa kununua kitambulisho. Sasa yule DO anakuambia yule mtu wa hapa si wa hapa, yeye ndiye yuko kwa kamati, anakuthibitishia kuwa huyu mtu si wa hapa, na yeye ni mzalendo wa hapa, anataka kitambulisho na mtu wa kutoka mahali pengine, kwa kuwa ako na pesa, amempa huyo DO pesa, anapitishwa kuwa yeye ni mtu wa hapa, anapewa kitambulisho.
Kwa hivyo DO asihusike na ile kamati inashughulikia kutoa kitambulisho. Iwapo ma chief na manaibu wao, headman na wale wazee wameshindwa kuwajua hao, sioni kama DO atadhibitisha kuwa huyo mtu ni mzalendo, mtu wa hapa, au si mtu wa hapa. Kwa hivyo ma chief na manaibu wao, na wale ma headman washughulike na hiyo utoaji wa kitambulisho, wawe wanadhibitisha, lakini DO asihusishwe hata kidogo.

Katika hospitali unakuta ya kwamba mama na mzee wanakuwa room moja wakidungwa masindano ama mwanamke anazalishwa na mwanamme. Hiyo sheria kidini tunaona si sawa. Tunapendekeza kuwa hospitalini, kuwe na room ambayo itakuwa inawahudumia wanawake na ni wanawake wenzao watakuwa wanahudumu, na wanaume wawe wakuhudumiwa na wanaume wenzao. Hakuna haja ya mwanamke kuja kudunga mwanamme sindano na mwanamme kumdunga mwanamke sindano ama mwanamme kuzalisha mwanamke. Hiyo sheria, kidini, tunaona si sawa .

Kuna hii mambo ya watu kupimwa, age assessment fee: Wanalipa pesa kiasi fulani ndio daktari anathibitisha wewe umetosha kupata kitambulisho. Na hii, sehemu yetu, imetumika vibaya kwa kuwa watu wetu wengi ni watu ambao hawajasoma, unakuta ya kwamba mtu mpaka awe na maelfu ya pesa, hawezi pitishwa. Kwa hivyo hii sheria watu wameichukulia vibaya, ndiyo unakuta watu wanachukua advantage ya kuwapora watu wetu wafugaji. Kwa hivyo tunataka hii itolewe kwa kuwa serikali imewanyima ile haki ya kuelimishwa na ndiyo wao wanaporwa kwa sababu watu sehemu zingine wako na ile certificate na ukiwa na certificate, hakuna age assessment unafanyiwa na hakuna pesa unalipa, unachukua kitambulisho.
Hatuoni sababu ya sisi kuwekewa vikwazo kama hivyo, kama ni deal ya kutupora, tuachwe tafadhali.

Tunaomba pia maji masafi: Isambazwe kwa sehemu ya wafugaji. Jambo la ajabu ni kwamba sehemu hii ya wakulima, wakati haya mambo ya kilimo ilianza, kila nyumba ilikuwa na mifereji na jambo la ajabu ni kwamba sehemu ya wafugaji, kutoka hapa mpaka Sabukia ni seventy kilometer, hakuna siku serikali imechimba hata dam iseme mtakuwa mkitumia haya maji. Tunaona ajabu sana ikiwa wakulima wanawekewa mifereji na watu wafugaji, serikali hata haijui wanatumia maji aina gani. Ni kama tumewekwa sawa na wale mifugo yetu yaani. Kwa hivyo serikali itupe maji masafi, kwani ni jukumu lao.

Tungependa barabara isambazwe sehemu ya wafugaji.

Halafu kuna dips, crushes, serikali ichukue jukumu la kujenga dips na crushes, sehemu ya wafugaji, sehemu nyingi ili mifugo zisiadhirike.

Halafu, unakuta ya kwamba sehemu kama Woldena ama Sabukia ambayo ni sehemu mbali sana kutoka division headquar ters, ambako madaktari wanapatikana. Mifugo zetu zinakufa kwa sababu ya ukisefu wa madaktari ama ukosefu wa madawa. Mtu yuko Sabukia, sijui atakuja lini hapa, apige ripoti kuwa mifugo zake ziko na ugonjwa.
Kwa sababu hiyo tungependa kuwe na community health workers ambao serikali imechukua jukumu la kuwa-train, kila location at least, halafu wawe na community pale, wakiwa na hayo madawa, wawe wakitibu hizo mifugo, badala ya mifugo ya mfugaji zikipatikana na ugonjwa, anatoka huko kutafuta daktari na daktari anakuambia yeye gari yake haina mafuta.

**Com. Kangu:** Jaribu basi uharakishe umalize.

**Mr. Siad:** Halafu kuna usafirishaji wa mifugo: Usafirishaji wa mifugo sehemu yetu tunataka ipigwe marufuku ama kama haitawezekana, mifugo iwe inasafirishwa kwa magari. Na kama hilo halitawezekana, tunataka wananchi wenyewe, kwa kuwa wafugaji ni watu wanajua aina yoyote ya ugonjwa, wawe pale ikipimwa, daktari akithibitisha kwamba hii mifugo haina shida. Kwa sababu unakuta saa hii mtu analeta mifugo kutoka Somalia, akifika North Eastern, Garissa, anaenda direct kwa district veterinary officer, anamchotea pesa kiasi fulani, anaandikiwa barua kwamba hizo mifugo hazina neno zipite na yeye hajaona hizo mifugo ziko hali gani.
Kwa sababu hiyo, tunataka ikiwa mifugo kama hizo zitakuwa zinaenda, wananchi wawe pale wakithibitishiwa ya kuwa zimepimwa na ziko na afya.

Ninafikiri nimemaliza lakini kuna kitu kidogo ningeongezea, hiyo sijaandika.

Kuna district tender committee: Hii district tender committee iko na tatizo kubwa sehemu yetu, ni sehemu zote ninafikiri, lakini sehemu yetu imezidi. Unakuta ya kwamba district tender committee Chairman wao ni DC, nafikiri, halafu wale kamati zake ni heads of the departments na hawa heads of the departments, ni wale kila baada ya miezi kadhaaa wametoka sehemu zingine, hawajui hali ya wilaya hiyo au sehemu hiyo. Sasa, wanatoa yaani tender yao kwa mtu tu ambaye hawamjui, ambaye ile kazi inatakikana afanye, hatafanya inavyotakikana. Sasa tunataka committee hawa wawe ni community, wawe ni wananchi wenyewe. Wahusishwe, wawe among the tender committee.

Halafu, Chairman wa County Council: Tunataka achaguliwe na wananchi, isiwe ni ma councillors wanakaa huko kuchaguana wao kwa wao.

Halafu kuna hivi vyama vya kisiasa: Mimi ningependekeza kuwe na vyama viwili pekee yake ya kisiasa. Kusiwe na vyama vingi.

Halafu, kuna jina tumebandikwa ya wafugaji wa kuhamahama: Hii kuhama hama ndiyo unakuta serikali imetukatiza huduma. Sisi wafugaji hatukatai, hii kuhama hama ikatwe kwa sababu ndiyo unakuta mfanyikazi wa serikali akiambiwa aende afanye

huduma fulani sehemu fulani, anaenda anasema wamehama. Hii kuhama hama ndiyo inafanya huduma mingi ikatike kwetu. Kwa hivyo tunataka hii kuhama hama itoshe, isitumike kwetu.
Ninafikiri nimemaliza.

**Com. Salim:** Unasema kwamba mmekatiwa huduma kwa sababu ya kuhama hama saa zote. Sasa suluhisho ni kitu gani?

**Mr. Siad:** Yaani wafugaji wa kuhama hama. Hilo neno tu kuhama hama litolewe, tubaki wafugaji, tosha.

**Com. Kangu:** Asante basi, andikisha pale kijana, pale iko register na upeane copy ya hiyo hapo na kama hatuja muita mtu wa pili, ninataka kwanza nimwite District Co-ordinator, pengine ana jambo au mbili anataka kusema kwa sababu tulianza kama ameenda nje kidogo, halafu ndiyo tuendelee. Na ikiwa kuna members of the committee, may be he can introduce them before we continue.

**Omar Thato:** Asante sana Commissioner Prof. Idha Salim, Commissioner Mutakha Kangu, Programme Officer Atieno, viongozi wa tabaka mbali mbali na wananchi kwa jumla hamjambo? Mimi jina langu naitwa Omar Dhatho na ndiye district co-odinator wa mambo ya Katiba katika wilaya ya Tana River.
Ningependa kuwakaribisha rasmi kwa kikao hiki, kutoka Commissioners na wananchi ambao wamehudhuria na pia nitachukua fursa hii kuwapongeza kwa kujitokeza mapema ili tuanze kazi ya kuchukua maoni ya watu wa Bura. Niko na kamati katika sehemu ya uwakilishi bungeni ya Bura ambayo ingawa ilikuwa na matatizo mengi mwanzoni, lakini bado tuko na kamati na wale wanakamati ambao mko hapa ningependa mje mbele ili wananchi, wale ambao pengine hawajawahi kuwajua, mupate fursa pia ya kuonekana na commissioners.
Nafikiri tuko watatu hapa. Katika kamati yetu ya uwakilishi bungeni ya Bura, tuko na Mheshimiwa Mohammed Galgalo, ambaye ni mbunge wa sehemu hii, tuko na chairman wa Tana River county council ambaye anaitwa Salat Gharacha, ni member wa kamati, mimi pia ni member of the committee, tuko na mwanachama ambaye anawakilisha vijana ambaye anaitwa Ibrahim Wario, sijui kama yuko ama ametoka kwa shughuli mbali mbali, yeye ndiye team leader wa kamati hii ya sehemu ya Bura. Tuko na Elizabeth Wanjiku, simama watu wakuone, alikuwa anafanya usajili pale mlangoni. Tuko pia na Aden Luli ambaye pia anafanya usajili.

Wale ambao wamesajiliwa katika sehemu ya uwakilishi bungeni, mwingine alikuwa ni Maramba Abdalla Hussein, naye alikuwa na matatizo ya kiafya na alituacha kama miezi miwili hivi iliyopita. Tuko na Jamila Salat Wato, ambaye amejiondoa kwenye kamati kwa matatizo ya kinyumbani, tuko na Johora Omar, naye pia amejiondoa kwa sababu ambazo hazingeweza kuepukika. Hao ndio wana kamati wa sehemu yetu uwakilishi bungeni ya Bura.

Kwa hivyo baada ya hapa, tutakuwa na mkutano wa kuchukua maoni upande wa Madogo siku ya jumamosi, tarehe nane. Kwa hivyo tukitoka hapa tutaenda Madogo na huo ndiyo utakuwa mkutano wetu wa mwisho katika wilaya nzima wa Tana

River kwa sababu tayari tumechukua maoni upande wa Galole na Pia upande ya Garsen. Kwa hivyo wale hawatapata nafasi kutoa maoni siku ya leo, wanaweza kufanya hivyo tukiwa Madogo siku ya Jumamosi. Na ningependa pia kumwalika Bwana DO lakini amesema ako na shughuli mbali mbali, hajafika. Kwa hivyo ninasema karibuni na mjaribu kutoa maoni kwa haraka haraka ili tupate watu wengi iwesekanavyo watoe maoni yao na tutakuwa na nyinyi mpaka jioni.
Tumejaribu kuangalia kama baada ya mkutano, wananchi ambao wanatoka sehemu za mbali wanaweza kupata kitu kidogo wakaweka kwa tumbo ndio waweze kurudi. Kwa hivyo msiwe na wasiwasi wale ambao watakaa, ili ukiitwa jina uwe umetoka kwenda nje. Tukae kwa makini, ukitoa maoni, pia usikize ya wenzako mpaka tumalize mkutano kwa njia mzuri. Kwa hivyo ninasema karibuni na tutakuwa na mkutano mzuri. Karibuni na asante sana.

**Com. Muthaka Kangu:** Asante basi Bwana Dhatho na tuendelee na wale wanatoa maoni, Mohammed Ali wario ingawaje aliandikisha kama observer. Ali Wario?

**Ali Wario:** Kwa jina la Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema mwenye kurehemu. Kwa jina ninaitwa Ali Wario, mimi ni mwenyekiti wa taifa wa wafanyi biashara wa mifugo nchini.

Nikianza Bwana Mwenyekiti, bara letu la Afrika, au sisi jamii ya ki-Afrika, kabla ya uhuru inayodaiwa leo, tulikuwa watu, tulikuwa mataifa yenye uhuru, utawala, hadhi na kila kitu ambayo leo wanadai wale walokuja kutudhulumu kwamba sisi tu watu wadhaifu, sisi tu watu wasiokuwa na mbele. Waafrika ni watu walikuwa na hadhi yao, watu walikuwa na utawala wao, na mtindo wao wa maisha.
Ninasikitika ukoloni ulipokuja, umevunja utawala wetu, ukavunja mataifa yetu, yakakusanya vikundi vya kikabila ili wahalalishe dhuluma ya kutunyanganya ardhi yetu, raslimali zetu na utu wetu pia.
Kwa hivyo mimi ninaamini uhuru ulikuwepo kabla ya Kenya kupata uhuru. Uhuru huu wa sasa ni uhuru tuna shaka nalo, limekuwa tatizo kwetu sisi, lakini Mwafrika alikuwa na uhuru wake, Mwafrika alikuwa na haki yake, Mwafrika alikuwa akifanya biashara, wakishirikiana watu wa sehemu mbali mbali.
Kwa hivyo sisi tutakalo ni uhuru wa mwafrika.

Mtaniwia radhi, paper yangu haiko kamili, nafunga safari kwenda Hola kwetu, kwanza mjue hali yetu ya Tana River. Hili jina mnalisikia Tana River ni kwa sababu ya mto inayopatia Wakenya power. Majuzi ma-commissioner mlipopimiwa kidogo, mkapunguziwa matumizi ya taa, nasikia kelele imetufikia mpaka hapa Bura. Miaka arobaini leo, hata generator hatuna huko na tunategemea Tana River. Kwa hivyo jana I had to travel to Hola kutafuta mahali ya kupiga chapa, sikupata, I had to go back to Garissa, as I am sitting here, ninazungumza nikitoka Garissa na baadhi ya makaratasi yangu haiko kamili hivi. Kwa hivyo ni baadhi ya dhuluma mnastahili kushuhudia. Resources si ndiyo hii hii inapatia Kenya taa na sisi wenye hiyo resource tunadhulumiwa.

Nikianza na karatasi yangu Bwana Mwenyekiti.

A new constitution should expose, articulate and rest upon clear national values and aspirations, among these should be the following:

Justice for all,

Equity for all Kenyans

Human development and unity for prosperity

Free compulsory universal education; hii ni sheria na ninaomba hii na ninatia sishindo zote hapa; iwe free universal education mpaka darasa la nane, bure, bure, tusishurutishwe. Sheria ni hii, hatukutoa nauli mara hii kwenda Lancaster kuiandika, leo mimi ninataka hii iwe sheria, Bwana Mwenyekiti, na ninatia umuhimu wote hapa.

Dhuluma yote inayofanyika hapa ni kwa sababu ya watu kukosa masomo. Na masomo ikiwa mimi nimedhulumiwa kiasi ya kuwa siwezi nikapata mkopo wa chai, nitapata masomo wapi? Na wale wanachukua tax kwangu. Kila nikinunua sigara, nikinunua kiberiti, peremende, mimi ninatoa tax kwa hii serikali. Serikali inaokota pesa, wajibu wao hawatekelezi. Mimi nitakalo ni elimu ya bure kwa watoto wetu mpaka darasa la nane.

Welfare for the less advantaged and the marginalized Kenyans such as the people of Tana River district: Tumekaliwa kichwani miaka yote hiyo. Angalia ile mifugo tuko nayo hapa, angalia ile miendo tuko nayo hapa, angalia Bura settlement project ilipokuwa hapa, nani leo awe maskini katika sehemu hii? Lakini kwa vile tumedhulumiwa, leo asili mia themanini na nne ya watu wa wilaya hii ni maskini.

The Muslim community should not leave by any other law exept that prescribed by Islamic Sharia. Hii inaenda kwa jamii ya Kislamu. Sheria ya Kenya iwepo, lakini sheria ya Uislamu itekelezwe kwa Waislamu. In regard to the above, Bwana Mwenyekiti, this Commission should not pass a law, that Parliament should not pass a law, either now or in future which should supersede the ruling or the Quran. Tuna tatizo kubwa sisi hapa, sisi tu Waislamu, sisi tukiwa jamii ya Kislamu, Quran imetutosha, imetoa haki ya yule mtu aliyekufa, yule ambaye yuko hai na yule ambaye atakayezaliwa.

Leo tumeletewa sheria za kuchanga, na sisi kuna mahali ambayo kuwa inafikia, wewe ni muislamu na matendo yako hayaridhishi Mwenyezi Mungu, kwa nini? Kwa sababu sheria ya serikali inakutaka wewe umuasi Mwenyezi Mungu. Sisi tutakalo, sheria yoyote isipitishwe ambayo ita-overule, ita-supersede Quran. Iwapo sheria itatolewa, sababu ukileta sheria leo ambayo ita-supercede Quran, you are creating a lasting dispute, a dispute ambayo haiwezi kuwa solved as long as I am a Muslim by faith na ninajua nifanyalo mimi inanitoa katika sera ya uislamu, basi mimi, sina haki ya kuifanya kile, afadhali mniue na nisipofanya mimi basi nitahukumiwa. Kwa hivyo sheria hapa, isi-overule Quran.

Kadhi’s court should be given full responsibility of manning all Islamic affairs and should operate independently from the current law courts. Kadhi hata kazi yake ni kufunga mwanamke ndoa au kumfungua, hana kazi ingine katika nchi ya Kenya.

Why is he there? Sisi tunataka Kadhi apewe responsibility ya kuhukumu mambo yote ya Kiislamu, sio tu kumfunga mwanamke ndoa na kuifungua hiyo ndoa, siyo hiyo. Tutakalo apewe wadhifa wote wa kutekeleza inayostahili kutekelezwa na courts.

Police custody and prisons, which will abide by Islamic sharia to be establilshed for Muslim inmates. These clauses can also use the other side. Bwana Mwenyekiti, maudhui ya jela ni kuboresha maisha ya yule mtu aliyefungwa. Lakini jela zetu inadhoofisha maisha, inaharibu zaidi hadhi ya wale wafungwa, kwa nini? Kwa sababu wanaume mia moja wanalala nyumba moja, hapa chini, wote wametandika pamoja hapa. Wale wanaume miaka saba miaka tano hawakukutana na wake wao; utawazuia wao kutofanya uchafu namna gani? Kwa hivyo jela yetu inaharibu kabisa, inaharibu hadhi. Hii mambo ya ushoga na kila kitu unayosikia, chanzo chake ni kule jela.

Bwana mwenyekiti, the word "Lord": The word "Lord" should not have any equivalent except Lord, God, the Almighty. Kuna jambo inatokea ambayo some of the offenses we are doing inasikitisha sana. Wewe unaingia kwa court ya Kenya, unainamia judge, kisha unamwita Lord; ushatoka katika Uislamu, wewe si Mwislamu tena. So the word "Lord" isiwe na maana ingine juu yake ila Mwenyezi Mungu aliyeumba ardhi na mbingu. Judge jana alisoma, leo anaitwa Lord, haya ni heshima gani? Aitwe Sir, aitwe Honourable, any other title but not "Lord".

Bowing and prostration: Both in Parliament and in our courts, iodolewe, ni kinyume na Uislamu. Anayesujudiwa ni Mwenyezi Mungu muumba, si binadamu, si Speaker wala si Judge. Kwa hivyo kitendo hii tumeletewa na Wazungu na sisi bila kuangalia imani yetu, tukajaa ndani. Mimi ninaomba hii mambo ya prostration, kwenda kumsujudia judge, kwenda kumsujudia speaker, iondolewe katika sheria yetu.

An urgent poverty alleviation programme be formulated and implemented as follows. Iwe sheria, isiwe ni fedha ya kwenda kuomba kwa Wazungu msaada. We have the tendency of begging donors, we write very good papers which cannot help Kenyans.

Leo tunataka sheria iweko ambapo poverty alleviation itakuwa sheria na kifungu cha kwanza, revival of Bura settlement project. Hii project imebeba Wakenya muda mrefu Bwana Mwenyekiti. This project needs less than three hundred million to revive it but the president of this Country used 2.7 billion Shillings kwa ndege isiyokuwa na repair, 2.3 billion shillings, Eldoret airport inayopokea ndege mbili kwa mchana. Unajenga 2.7 something kwenda kuweka kuweka industry ya risasi, tunapigana na nani? Lakini look at the Bura settlement project, Wakenya wangapi wangenufaika iwapo huu mradi ingekuwa inawapatia nafasi za kazi, chakula na kila kitu. Leo this one is not viable. We are lacking priority, we have to go for aeroplanes, risasi na kadhalika na unawacah miradi kama hii inakufa na Wakenya wanakufa na njaa.

Tunataka revival of Bura settlement project iwe ni sheria, isiwe ni tafadhali kwa serikali.

Famine Relief Programme be replaced with a sustainable productive scheme that guarantees food security. Gunia moja kutoka

America, what is the cost of transporting that to Kenya? Leave alone the food nutrients in it. Imeletwa hapa kama ina vidudu, hatuna la kufanya sisi tu waombaji, Wamarekani wanataka sisi tule vidudu, serikali yetu has no policy in place to address this. Tunataka schemes, tuko na mto hapa. Ikiwekwa, hizi schemes zifufuliwe, Wakenya watanufaika.

Micro-credit schemes and entrepreneurship educatoin be advanced through government to help establish and promote trade and savings.

A government policy which encourages a shift from nomadic activity to intensive ranching be encouraged to avail engagement and investment opportunity.

That we are created human beings with the same fundamental rights among which are the right to live, the right to own property, prosper and the right to free movement and settlement in any part of the republic of Kenya and demanding no more rights than other Kenyans but prepared not to concede to not any lesser rights than entitled to fellow Kenyans. Sisi hapa tu wananchi, kuna wenye nchi, sisi hapa tu wananchi sisi. Haki yetu ni akipenda kina Moi na wenzake kule. Wakipenda tuna haki sisi, wasipopenda, hatuna tunacho sisi, kwisha.
Kwa hivyo, sisi hatutaki haki kuwashinda wengine na tusipewe haki chini ya wengine, hatutakubaliana.

The new democratic constitution to be established in Kenya must correct and remove the injustices perpetrated against the people of Tana River district buy both the Kenyatta and the Moi governments: Wameuawa watu hapa pasipo na sababu yoyote; Haji Musa aliuawa hapa na kuna sub-chief mmoja alitolewa kwa nyumba akauawa. Hakuna mahali utawapeleka, wao wameamua kuua na wao wako juu ya sheria, hakuna tufanyalo sisi. Kwa hivyo Katiba itakayokuja iwe Katiba ya kutulinda sisi, iwe katiba ya kutuepusha na maudhi kama hayo. Tusiwe tunauawa at will by the sitting government.
The Constitution must repeal all oppressive laws and practices that contribute to humiliate the people of Tana River district, principle among these are the outlying district act and the requirement for extra identification paper for the Tana River residents i.e through the certificate of verification.
Mambo mawili hapa: Sheria ya outlying district; Lamu, Garissa, Tana River, wakiamua serikali kesho asubuhi watu wauwawe, watauawa because of that clause. This outlying district iwe repealed.

Halafu hapa kwetu unatafuta kitambulisho, haya iko kwa jamii ya Kisomali, yeyote aliye na origin ya Kisomali, hata jamii ya Wordei, wanalazimishwa waje na kadi nyekundu, hii kadi nyekundu ni ya nini Professor?

**Com.:** (inaudible)

**Mr. Wario:** Lamu, Tana River and North Eastern Province, ndizo outlying districts. Wakiamua serikali kesho kuleta

wanajeshiwa elfu kumi kuhangaisha sisi manyumbani mwetu, hatuna amani tena sisi.

Hii mambo ya identification: Kitambulisho ni cheti kinachostahili kumilikiwa na kila Mkenya atakapofikisha miaka kumi na nane. Leo ni kinyume. Ukifikisha miaka kumi na nane, mpaka utafute pesa ya kwenda kuhongana. Kisha sisi tu wadhaifu zaidi kwa sababu red card, red card mpaka uende uweke mezani, ikiwa wewe Mwordei, hautapata, wewe Msomali aina yoyote, hautapata. Hii red card iondolewe, wapewe wao walioleta red card.

The pastoral communities in Kenya are the biggest victims of historical, political and ecomomic marginalization and their pastoral economy has not been fully mainstreamed into the national economy despite its great potential and therefore we recommend:
Need for special legislation and national policy to address and deal with pastoral issues including management, use and shairing of pastoral resources based on their unique ecological, social, cultural, economic and political context as well as customary, normative systems.

Ndugu yangu, sisi wafugaji, dhuluma tuliofanyiwa ni kubwa kushinda jamii ingine yoyote ya nchi ya Kenya. I have all the evidence to prove this, tulifanyiwa dhuluma kubwa.
Hapa ng’ombe ngozi yake, kila mtu kujua ng’ombe umuhimu yake, ataangalia nyayo yake kwanza, amevaa ngozi aina gani. Is it a leather shoe? What is it costing? Sometimes the shoe you are putting on and the price we are paid for our cattle are the same. Nyama, usiangalie mfupa, maziwa, hizo vitu ingine yote usiangalie. Kwa nini? Kwa sababu we are lacking a policy to address this issue.

We again recommend that the new constitution should compel the government to put in place a ministry of pastoral development. Isiwe tafadhali kwa serikali itakayokuja, iwe ni lazima tuwe na wizara ya kuangalia haki ya wafugaji. Tuwa na wizara itakayoangalia mambo ya uzalishaji ya mifugo, soko ya mifugo, matibabu ya mifugo na mali ya asili inayopatikana katika sehemu ya wafugaji.
We want a ministry of pastoral development.

Special consideration for the people of this area such as entry point to universities, to special education and literacy development programmes. Leo hii tunaabiwa bwana Commissioner, kwamba mtoto kwenda kwa teacher training colleges ni lazima awe na “C” with clusters in it. Look at one thing. Hii wilaya yetu ya Tana River tulikuwa na El-nino ambayo effect yake ilikuwa mbaya kushinda wilaya ingine yoyote. Baada ya El-nino, kukaja drought, baada ya drought kukaja clashes, baada ya clashes tuko kwa floods sasa. Ours has been interchanging calamity, one to another.
You cannot let these children ambao wanakaa hapa to compete freely na wale watoto wako Nairobi. Facilities inayopatikana Nairobi haipatikani hapa kwetu kwa hivyo watoto wetu kabla hawajaandika neno “A” washadhulumiwa. Then you are expecting the same children to go and compete na wale watu wako na laboratory kubwa kubwa na hivo vitu. So, we want special consideration wapewe watoto wetu ili wapate fursa na wao kwenda kukaa universities. Sio kwamba hatuna watoto but

facilities. Ile facilities tunayo hapa ndiyo inalazimu watoto wetu kukaa nyuma kila mwaka.

**Com.:** (inaudible)

**Mr. Wario:** Ni sawa Bwana Mwenyekiti.

Compulsory free universal education; I am adding that one again. Pastoral education system should be introduced and implemented within the pastoral areas. The current education system is meant for people with permanent settlement. Ikiwa mfugaji ----? Huna bahati tena wewe, mtoto wako leo atakuwapo shuleni, kesho atahama na wewe, akirudi hapa ana uhakika ataanguka mtihani. We want pastoral schools.

Traditional, religious, judiciary mechanism be introduced and respected. Nikikupa mfano moja Bwana Mwenyekiti; wamepigana watu wawili mmoja akauawa, aliyekufa amewacha kwake mjane na mayatima. Aliye hai, anawekwa jela, anawacha kwake mjane na mayatima. Our Constitution is not giving us something here. In Islam for instance, wamepigana wawili wakauwana, aliyekufa analipwa fidia, ya ngamia mia moja au ng'ombe mia mbili. Sasa wale mayatima wake, wale wajane wake wana kitui ya kutegemea katika maisha lakini kwa Katiba yetu, yule mwingine anafungwa, kufungwa si suluhisho, ni tatizo. Kwa hivyo tunataka kama kuna judiciary mechanism ya kimila, kama jamii ya hapo wanasema hii kesi sisi tunaweza kuihukumu, basi wapewe. Ikiwa dini wanaweza hukumu conflict ya jamii, wapewe. Si lazima kwenda kwa prosecutor na judge kutuhangaisha kule.

An identity card should be use instead of cash bails and bonds: Bwana Mwenyekiti, wewe kuwa Mkenya ni kitu kubwa, the nationality. Ikiwa you are a poor man, ukifanya makosa uende cell ya Kenya, hutatoka hapo mpaka siku ya hukumu. Badala ya cash bail, watu wapewe identity cards i-stand as surerity. I mean, akikataa kuja, basi nationality yake iwe withdrawn. Huwezi withdraw pesa kwa bank, huwezi fanya anything in this country without an identity card. So an ID card is enough to be anything, inaweza kuwa inakusimamia kwa kila kitu. Isiwe mambo ya cash bail, ikiwa wewe ni maskini, cash bail utatoa wapi? Kwa hivyo sheria hii ina dhuluma dhidi ya wanyonge, kwa hivyo ibadilishwe.

All land known as trust land, which is still unadjudicated and unregistered, is to be refered as land under customary tenure.

All such land which is used or occupied by the local indigenous and from which they derive their daily livelihood shall be vested in them on the basis of either private or customary tenure, depending on the prevailing circumstances.

Such land that is not occupied and is not in the immediate use of the local residents of an area shall be set apart for and vested in the indigenous communities in the areas of ---?

Land use rights of pastoralists be recognized and respected to avoid conflict between them and the farming communities, competing for the same land under natural resources.

Bwana Mwenyekiti ukinipa fursa hapa, angalia vita tuliopigana Tana River, Mhorma na Mpokomo kuuana miaka yote hiyo, kwa nini hatukupigana miaka yote hiyo? Ni kwa sababu Tana River had been declared an adjudication area. Walipo-declare, they did not look at the lifestyle of the people of Tana River district, waliangalia tu sheria tuliyonayo leo inazungumza kuhusu mkulima na hiyo ndiyo mwisho wa sheria, mfugaji has no role here. Now I have livestock and I have to alternate between existing ecological zones for me to survive. Look at the carrying capacity of our land, usione haya mathenge ukafikiri uko highland, hii ni jangwa.

Land use rights of pastoralists be recognized and respected to avoid conflict.

The fundamental and transforming reforms be undertaken to the local government authorities as follows: Serikali za wilaya; hii ndiyo mfano mzuri wa utawala leo, lakini kuna matatizo makubwa. Kwa nini? The local government Act Cap 265 be reviewed to empower the councils in managing their affairs and those of the municipalities.

Mayors, town chairmen and chief officers of the councils and the municipalities should be elected directly by the people. Tupewe fursa sisi tuchague Chairman, Mayor, Clerk na Treasurer. Wanakuja watu kutoka Nairobi kuja kukalia hapa, ndiyo Chairman wetu, ndiyo Clerk wetu, ndio Treasurer Wetu. Kazi yake kubwa ni kuziokota na kwenda tu, lakini iwapo tutapewa fursa ya kuchagua mmoja wetu aende akalie councils zetu kama clerk, kama treasurer, basi taabu ambayo tunayo leo isingetokea.

The councillors should be paid from the consolidated fund a flat rate and the council should by law train the Councillors in courses of government and management. Ukienda Nairobi City Council, Councillors wanalipwa elfu hamsini kuenda mbele, kuja Tana River, wanalipwa elfu saba na kadhalika, hawa Councillors, wao ni kama wabunge, wamechaguliwa na watu, walipwe kutoka consolidated account a flat rate. Ukilipa wa Nairobi fifty thousand, hata wa Tana River umlipe fifty thousand. Hapa unampa seven thousand, Nairobi unampa fifty, the responsibilities are just the same, kura iliyomchagua councillor ndiyo iliyomchagua mbunge, ndiyo ilimmchagua Moi, kwa nini na hao wasilipwe kutoka Consolidated Account?

Sixty per cent of the wealth and the taxes in the district should be controlled by the councils unlike now where the ministry of local government controls our authorities. Asili mia sitini ya rasilmali zetu iwe ni Council itaiendesha kinyume na sasa wizara kuishikilia kutoka huko. Kwa hivyo unaona Bwana Mwenyekiti, unasema nifunge virago, nitafunga, tarehe nane niko na wewe tena.

**Com. Mtakha Kangu:** Asante. Niko na swali moja ndugu. Mwanzo umesema serikali i-intensify ranching badala ya kuendelea na nomadic life, tuwe na intensified ranching, which is assumed now that people will settle in one place watapatiwa facilities ya kulisha mifugo yao and so on. And then ukisonga mbele you continued to say the government should put up schools for pastoralists, tuwe na ministry ya pastoral development, mbona tusiseme sasa tuwe na

ministry ya livestock development ama hiyo business ya ranching because ukisema ministry of pastoral development, you assume we are continuing with the nomadic..?

**Mr. Wario:** Thank you very much for that concern. One, since the creation of mankind on this earth, Yesu ni mfugaji, Yesu, amechunga, kisha leo mimi ni mfugaji, mimi, look at the time between me and Yesu. Now, any policy planner of this he sits, the only thing he can advice you ni kwamba, wacha pastoralism and start an new life, how? How do I do this?

**Com. Kangu:** It has to be gradual.

**Mr. Wario:** It has to be gradual, so when I am saying tunataka serikali ianze mambo ya ranching, nilizungumzia chini kwamba ilete investment. Sisi tunachunga sasa, hatuna tunacho, lakini tukiwa na ranches, tukiwa na hizo vitu, maybe watu watakuja ku-invest in our ranches na tutanufaika zaidi. But for this area, the most viable way of life, for Tana River district, 38,964 square kilometers, less than 10% is arable land. So patoralism, hakuna namna itaweza toka kwa mikono yetu hapa kwa hivyo, neno moja ya mwisho tafadhali.

Nimeweka map ya Kenya hapa, I am doing on something, nimekwambia tuna tatizo ya taa, sijamaliza hizi vitu, nimeleta map ya Tana Rriver hapa. Tuna tatizo, sisi hapa tulipo tunapakana na wenzetu. Upande hii kuna Wasomali, upande hii kuna Wakamba, huku kuna Wameru, huku kuna Waborana, huku, tuko pwani, lakini hivyo hivyo tunapakana na Wagiriama. Mpaka huko imesukumwa imefika mahali inaitwa Kurau, ishasukumwa mpaka Tana River, mahali inaitwa Kurau. Upande hii ya Eastern imesukumwa imeletwa hapa karibu, North Eastern wamesonga ndani, na kuna sublocation mzima which is going now, imeenda, sub-location wananchi wako, wenyewe wana title deed as we are speaking today, it’s a whole Sub-location, the owners have their title deeds. So, my last point is, administrative boundaries should be respected, iwachwe vile ilivyo.

Kama mtu amesoma ana ma degree zake, awe nayo, lakini kwetu atuachie.
Wewe ni mtu wa serikali unajulikana, ndiyo lakini kwetu utuachie, usituletee zishindo. Asante.

**Com. Idha Salim:** Umesema kwamba ungependelea mtu badala ya kuambiwa alipe bond, achukuliwe ID yake. Hakuna athari kwamba ukilichukua ID yake, kesho atakwenda kuchukua nyingine? Kwa urahisi sana?

**Mr. Wario:** Hapa, iwapo itafanyika hivyo, then inathibitisha kuwa wale wanaotoa ID cards are not sure of what they are doing. But if we would have one centralised system, hii dunia ya macomputer, isipokuwa Tana River hatuna, utapiga ujue fulani kapata kitambulisho. It is simple.

**Com.Mutakha Kangu:** Asante sana, weka sahihi na upeane.

**Mr. Wario:** "***Uhuru sijauona na tunda silibaini, iwapo tumepigana tukaongoa mkoloni. Limebaki kubezana na uto kutodhamini. Tunda la uhuru ni ipi na Mkenya shamba huna?"***

**Com. Mutakha Kangu:** Asante basi. Jibril Omar na nikumbushe wale wameingia nyuma, hawa nimewapatia muda kwa sababu walikuwa na maandishi na mambo inaonekana ya muhimu kwa nyinyi nyote. Lakini tulisema sana sana tunapatia mtu dakika tano kama ako na maandishi na kama hana maandishi na kama hana maandishi, dakika kumi. So, mjaribu kulinda masaa. Mzee, unaanza na kutaja jina.

**Jibril Osman:** Mimi ndiyo ninaitwa Jibril Osman.

**Com. Mutakha Kangu:** Na wale wako nyuma, please msipige kelele.

**Mr. Osman:** Mimi niko na maoni ya kusema. Kwa hivyo kama ni mambo ya kubadilisha Katiba, mimi naona mtu kama ameandikwa Sub-chief ama Chief, wanaandika mtu, kijana wa miaka ishirini apate sub-chief, halafu ile sehemu analetwa ama yeye amepata, anaelewana na watu wengine, haelewani na wengine. Wale haelewani nao wako kwa shida mpaka huyu mtu amalize miaka hamsini na mitano ndiyo atoke kwa kazi ya serikali, shida ile itakuwa bado.
Kwa hivyo mimi nimeona labda ibadilishwe iende chini hii miaka hamsi ama kazi ya chiefs ipewe muda kama miaka kumi hivi mtu akifanya kazi ya chief, awache hiyo kazi kwa sababu wale wananchi wanaumia. Moja hiyo.

Ya pili: Kulingana na hii Katiba yetu ya sasa, tunaweza kuchagua mbunge hapa, constituency yetu hii, miaka tano. Mtu akichaguliwa akae miaka tano, sasa ile miaka tano inakwisha bila sisi kuona yule mbunge kwa sababu kwa vile yeye amechaguliwa miaka tano, hakuna kitu ya kufanya.
Kwa maoni yangu, iwekwe hapa kizuizi, baada ya miezi tatu, mtu akikosa kuja ile constituency yake, iweke sheria awanyiwe kitendo fulani, halafu aogope sheria.
Kama hawafanyi hivyo, mtu anangoja miaka yake ikiisha ndiyo tunamuona yuko kwa Mathenge. Miaka tano ile ingine yeye hajali sasa kwa sababu hakuna kitu yeye anaogopa, unajua binadamu lazima aogope sheria. Hiyo ni ya pili.

Maoni ya tatu: Local governments, hii watu wa county councils. Ile sehemu ambayo anapata faida nyingi, hawafaidiki na ile faida ambayo wametoa.
Kwa mfano hapa Bura county council wanatoa pesa nyingi zaidi. Sasa ile pesa inasemekana ipelekwe huko Hola, Nairobi, ndiyo baadaye tutapata faida, hata hatuoni. Kwa nini wakati ile faida inachukuliwa ile faida, ifaidishe ile sehemu ile? Ndiyo wapate faida yao. Kwa mfano kama Bankel, wanapata kwa wiki moja, zaidi ya elfu mia mbili hivi na hawapati hata ndururu. Ile pesa inachukuliwa inaletwa hapa Hola, ati wanapeleka Nairobi, sasa wale hawafaidiki. Si afadhali ikawanywe pale kuliko unangoja itoke Nairobi.
Ninataka maoni yangu irekebishe ile sheria, ile mahali ambayo inapatika, mapato, ibadilishwe.

Lingine: Kulingana na maoni, unajua saa ingine niko na maoni, halafu yule wa mbele yangu anasema hiyo maoni, si hakuna maana mimi niongee, si afadhali niongee ile yangu ile fupi?

**(Audience):** Ni kweli.

**Mr. Osman:** Kwa hivyo kulingana na wale waliosema mbele yangu, upande ya kitambulisho, hiyo haina maana kwa sehemu yetu hii kwa sababu aliye na pesa ndiye anapata. Mzaliwa wa pale hapati. Kwa hivyo waodolewe wale wa serikali wanaohusika na mabo hayo kwa sababu mkubwa anahongwa pesa, mtu anatoka jana Mogadishu anapata, yule amezaliwa hapa hawapati ile ID. Kwa hivyo nawauga wale wa mbele yangu.

Shida ingine ni kusema mtu kama anakosa makosa, ashtakiwe, apelekwe kotini kuliko mtu akishikwa, wakae naye waongoje mpaka alipe kitu fulani. Kwa hivyo mtu akishikwa, apelekwe kotini ama aachiliwe.

Kwa leo maoni yangu ni hayo, nangoja tarehe nane.

**Com. Mutakha Kangu:** Asante. Weka sahihi pale. Tupate Juma Wario.

**Juma Wario:** Commissioner Mwenyekiti, na Commissioner uliokuja naye, wageni mlioandamana nao, kwanza ninawaambia mkaribie hapa Bura na la pili ni kuwajulisha kuwa ninajulikana kwa jina Juma Wario. Ningependa kutoa maoni yangu na memorandum yangu nataka muniwie radhi iko kwa machine, haijatoka na nitawasilisha kwenu siku ya jumamosi lakini kwa siku ya leo ningependa kuyapitia yale yaliyo kwenye memo hiyo.

Kwanza: Ningependa haki za wafungwa iangaliwe sana, kwani wafungwa hawa huwa wanafungwa katika jela na wakati unapomfunga huyo mfungwa, unawadhulumu watu wengi ambao wanamtegemea huyo mfungwa, kama watoto wa shule na mama. Na hao watu ambao ni very innocent wako nyumbani ni watu ambao katika hiyo kosa mtu mmoja alifanya hawakufanya, lakini wanapata shida kwa sababu yake.
Kwa hivyo mimi ningelipenda mfungwa afungwe wakati mwingi katika kifungo cha nje au anaweza kutumikia serikali katika kifungo cha nje na awe anaweza kufika nyumbani na kutekeleza mambo madogo ambayo watu ambao wamemtegemea angeweza kuwasaidia nayo.

Pili: Ningependa kuwaambia ya kuwa kuna hawa wakimbizi wanaotoka sehemu mbali mbali kuja kuingia Kenya na kutambaa mpaka sehemu za wilaya. Hao watu ingewezekana, wapewe kadi ambayo ziko computerised, kama atakuja kutafuta kitambulisho ya taifa, aweze kujulikana kuwa yeye ni mkimbizi, asiwe anaweza kututatiza katika sehemu hizi.

Lingine: Masomo ya watoto katika sehemu ya watu wa kuhama hama, haitiliwi maanani. Kwa hivyo ningependa maneno ya masomo ya watoto, hasa wasichana, ikae katika vitabu vya sheria lau mtu kama hataweza kupelaka mtoto wake shule, iwe sheria hiyo inaweza kuwaadhibu kwa njia moja au nyingine iliu kuwahamasisha watu hao kuwapeleka watoto wao shuleni.

Serikali itoe mashule ya kuhama hama ambayo ingeweza walimu wawe wanaweza kuhama na hawa watu ambao wanahamahama, watoto wao pia wapate elimu. Na katika hizo shule za kuhamahama, tungependa waalimu waajiriwe kutoka jamii hiyo ya kuhamahama. Kama hiyo jamii hawatakuwa na waalimu wa kutosha, waalimu wengine watafutwe kutoka jamii ambayo iko na desturi sawa na hiyo jamii, wasitolewe sehemu zingine, wawe wanaweza kuhamahama na hao watu.
Kwani kama utachukua jamii wasiohamahama na uwapeleke sehemu hiyo, itakuwa hizo shule zitakosa masomo kwa sababu hawataweza kuhamahama na hao watu wa kuhamahama.

Sheria hii ya kurithi wanawake itolewe katika sheria kwa sababu ya magonjwa ya hapa na pale. Mtu asije akasema hii iko katika sheria ni lazima nimuoe mwanamke huyu na hali kumbe yeye mwenyewe yuko katika magonjwa, awe ataambukiza hiyo jamii ingine.

Mambo mengine ni mali ya asili: Mali ya asili, kama Tana River, tuko na mali mingi ya asili lakini kwa vile haimilikiwi na watu wenyewe, haya mali ya asili hayatusaidii. Kama Tana River iko na mawe ya Gypsum ambayo inachimbwa katika locations ambazo ziko katika Bura na Bura ukiangalia, kutoka irrigation ife ni kati ya zile locations maskini zaidi katika nchi hii. Kama hiyo Gypsum ambayo inachimbwa sehemu ya Tarubende. Ingekuwa tunamiliki sisi wenyewe, wale watu wa kusaga simiti wangelikuwa wanatupitia sisi na tungekuwa tunapata hizo pesa. Lakini wanakuja kuchimba katika sehemu yetu na wanajitajirisha na kupeana hizo ushuru kwa watu wa county council na sisi tukiwa tuko katika umaskini, na utajiri unapitia kwa watu wengine.
Kwa hivyo tungelipenda mali ya asili tumiliki sisi wenyewe, tuwe tunaweza kulinda na mwenye anataka kuchimba vitu kama hivyo awe anatupotia ili tupate hizo pesa na hizo mali.

Chairman wa county council achaguliwe na watu, asiwe anachaguliwe na hao hao watu wa council.

Mobile dispensaries pia ziwekwe kwa sababu watu hata hawapati first aid katika sehemu za wafugaji kwa sababu district hospital iko mbali, kilomita kama mia tatu, mbali zaidi na mahali watu wenyewe wanaishi.
Kwa hivyo serikali ituwekee mobile dispensaries ili tuweze kunufaika na vitu kama hivyo.

Kuna mito ambayo, ni seasonal, ambayo zinapita kutoka sehemu ya juu na kutiririka katika mto Tana. Ningelipenda serikali ichimbe dams katika hizo mito ambayo ni seasonal. Ikae katika vitabu vya sheria na iingie katika budget ya serikali ili dams zichimbwe katika hizo seasonal rivers kama vile river Ermani, Galole na sehemu za Lakabana huko, yote hizo ni sehemu ambazo zinatiririsha maji mengi. Kama tungelikuwa tumechimbiwa dams, hakungekuwa na mkusanyiko ya watu katika River

Tana ambayo ingeweza kupuguza clashes. Watu wangeweza kutumia hiyo maji ya seasonal rivers. Hata tungeweza kufanya irrigation na watu hawangeweza kukusanyika sehemu ya mto Tana.
Na hiyo tafadhali ningelipenda ikae katika kitabu cha sheria.

Ofisi ifunguliwe ya mtu wa kutetea haki za wananchi: Sisi wakati mwingi haki zetu zinadhulumiwa na tunashangaa ni wapi tutaenda kushtaki. Unaambiwa ukishtaki kitu fulani, wewe umevunja sheria ya serikali, unaogopa, lakini kama kungekuwa na ofisi kama hii, tungelikuwa tunapeleka mashtaka yetu na mambo yetu pengine yangeangaliwa.

Attorney General achaguliwe na vyama vyote ambavyo vimesajiliwa Kenya. Asiwe anachaguliwa na mtu mmoja mmoja peke yake ili kupunguza mambo ambayo sisi wenyewe hatungeweza kuyajua.

Bura settlement scheme: Wakati mwingi ikiwa inazungumza, ifunganishwe pamoja na Hola settlement scheme kwa sababu Hola ni scheme ambayo ilikuwa hapo awali kabla ya hata Bura kuwa hapa. Kwa hivyo Bura na Hola settlement schemes ziingie katika vitabu vya sheria. Isiwe ni kitu ya kuzungumzia watu tu hapa na pale kwa sababu kama itaingia kwa sheria, tutakuwa na uhakika ya kuwa hizi vitu zitakuja kufufuka ili umaskini mkubwa mkubwa ambao unakumba sehemu hii inaweza kukabiliwa.

Kitu ingine mimi ningeweza kuzungumzia, kusiwe na mtu ambaye atakuwa juu ya sheria katika Kenya hii yetu, isipokuwa Allah subhaanahu wataala. Kwani kama kutakuwa na mtu ambaye atakuwa juu ya sheria, mambo mengine mengi yataharibika na sisi hatutaweza kukabiliana nayo kwa sababu tunamwogopa, yuko juu ya sheria, tukizungumza hivi tutashikwa.
Kwa hivyo ningelipenda kila mtu katika Kenya yetu awe chini ya sheria, sheria iwe juu yetu.

**Com. Mutakha Kangu:** You have one more minute.

**Mr. Wario:** Asante. Mtu yeyote asiwe juu ya sheria.

Ministry of pastoral development vile mwenzangu alivyotangulia kusema, tafadhali ikae katika vitabu vya sheria.

Ardhi ya wafugaji kama vile Tana River na sehemu hizi zingine, kusiwe itagawanywa kwa mtu binafsi kwa sababu hiyo haitalingana na vile sisi tungeliweza kukaa kwa sababu tuko na mifugo wengi ambao wanalisha, tunataka hiyo iwe communal land, iwe tunaweza kutembea free na kulisha mifugo yetu.

Boundaries ikae kama zamani. Kusiwe na kusongesha boundaries hapa na pale kwa sababu italeta clashes bure.

Kwa hivyo memorandum yangu itakuja siku ya jumamosi, huko ambako mtakapoenda, Madogo, ningeliwaambia karibuni Bura. Asanteni.

**Com. Mutakha Kangu:** Na tupate Mariam Mohammed although alisemekana ni observer. Biramu Khalija, still an observer, Mohammed Mustafa?

**Mohammed Mustafa:** Tume ya Urekebishaji wa Katiba ya Kenya, viongozi na watu wa tabaka mbali mbali, Asalaam Aleikum?

**Audience:** Aleikum Salaam.

**Mohammed Mustafa:** Mimi jina langu Mohammed Mustafa, ni kijana nimekuja kutoa maoni kama kijana.
Mimi ningependa serikali iweke sheria sehemu ya wafugaji kama location ya juu.

Dispensary: Hospitali ni muhimu sana. Kuna locations nyingi ambazo hazina hospitali, dispensaries. Wananchi wamepata shida ya kutosha kwa sababu mtu ukigonjeka, kuja kutafuta gari i kuletwa hapa hospitali ni kazi ingine kubwa sana na watu wengi hawawezi kwa sababu ya pesa. Hata malaria inawamaliza watu huko kwa sababu ya kukosa matibabu.
Ninataka iwekwe sheria, location ya juu iwe ni lazima iwe na hospitali na malipo iwe ni juu ya serikali.

Ya pili, sisi wafugaji, sehemu yetu ya juu, wananchi wako na shida kubwa ya maji. Kuweko na dam kila sehemu ambako watu wanakaa. Serikali ichimbe dam, iwekwe sheria, iwe juu ya serikali, wananchi wapate maji safi ili ipunguze shida ya maji.

Ya tatu, daktari wa wanyama wakae kila location ili wapate shida ya wanyama haraka kuliko wewe unatoka huko sehemu ya huko juu, unakuja hapa kupiga ripoti ya ugonjwa wa ng'ombe na wao tena wanasema gari yao hakuna mafuta.

Wanyama wanaendelea kupata shida, wanaendelea kumalizika. Iwekwe sheria daktari wa wanyama akae kila location.

Barabara ya sehemu ya juu: Serikali isambaze barabara. Location ya juu hakuna barabara, mawasiliano ni mabaya na sehemu nyingine hata serikali ikipanga saa hii mobile clinic, hata kazi haiwezi enda. Ni shida kubwa sana, barabara iwekwe.

Kitambulisho: Kuweko na muda wa kutembelea kila location kwa sababu kuja kutafuta kitambulisho hapa district ama division, wananchi hawawezi kwa sababu ya gharama.
Ukija kutafuta kitambulisho sehemu ambayo siyo yako, lazima utumie mfuko wako.
Tafadhali iwekwe kwa sheria, watu wa kupeana kitambulisho wapewe muda ya kutembelea kila location.

Ingine ni juu ya Chief ama Sub-chief: Mimi nimeona wachaguliwe na wananchi wenyewe, ama councilor, kwa sababu serikali wanaangalia certificate lakini wazazi wanajua kila kijana tabia yake. Nani anawasikiliza watu na ukipata hiyo cheo nani

anaelewana na watu na nani haelewani na watu, na wazazi wanajua. Kila kijana kabla hajapata kazi anajua, lakini serikali inaangalia certificate pekee yake.

Wale wengine, ukipata chief ama sub-chief, kuzungumza hawajui, na wako na hasira ya haraka na serikali haijui huyo mtu ako namna gani lakini wazazi wanajua na kwa sababu hiyo mimi nimeona chief na sub-chief wachaguliwe na wananchi.
Mimi nimetoa maoni hayo mafupi, asanteni sana.

**Com. Mutakha Kangu:** Na Abdulla Yusufu? Imesemekana ni observer, Balesa B. Mathew?

**Balesa Mathew:** Bwana Mwenyekiti, ma Commissioner, viongozi na wazee pamoja na wageni, hamjambo?

**Response:** Hatujambo.

**Mr. Balesa:** Ninachukua fursa hii kupeana mapendekezo yangu na kabla sijapeana, mimi ni Mwalimu wa hapa shule ya Kirimani, majina mmeshasikia.

Kwanza nitaanzia na pendekezo langu la majimbo: Kulingana na mimi, ninaonelea Kenya iwe na mfumo wa majimbo kwa sababu ukiangalia kutoka wakati tulipopata uhuru, tunaona ya kwamba sehemu zingine za Kenya zimebaguliwa. Kwa mfano, ukiangalia kama mkoa wa Pwani, kama mkoa wa Kaskazini Mashariki, na Turkana na kadhalika, unakuta ya kwamba tumebaguliwa jinsi ya kwamba we are not enjoying the Kenya national cake. Hatuja-enjoy kabisa. Sehemu kama Nairobi zina-enjoy, mambo yao yanafanywa haraka haraka, maendeleo yanafanywa haraka haraka, lakini ukiangalia sehemu kama hizi za mkoa wa Pwani, North Eastern province, Turkana and what have you, unakuta ya kwamba hakuna kitu.

Kwa hivyo kuondoa tatizo hilo, ninonelea tuwe na mfumo wa majimbo, ya kwamba viongozi watoke area hizo ambazo watasimamia miradi yao wenyewe kuliko mtu wa nje kuja kutusimamia kwa sababu mtu wa nje hawezi kukuongoza vile ambavyo unataka miradi yako ifanyike, kama ni resources and what have you.

Kitu kingine ambacho ningetaka kupeana mapendekezo ni kuhusu wilaya yetu ya Tana River: Wilaya yetu ya Tana River, kutoka tupate uhuru, tumeachwa nyuma kimaendeleo. Na ningependelea kutoa maoni ya kwamba serikali inapopitisha haya mapendekezo, ituangalie, pia ituorodheshe katika hayo mapendekezo, kwa mfano, kutoka tupate uhuru, hatujakuwa na lami, lami imeanza hivi majuzi, mpaka ikasimama sehemu ya hapa Mnasiri Mnasiri huko, three years ago na mpaka saa hii nothing has happened. Haijulikani kwamba what had happened, lami imesimama, hakuna viongozi ambao wanaweza kutetea hali hiyo ya lami, lami iweze kuendelea,
Transport: Kuna kuwa na communication barrier na kadhalika. Kwa hivyo tatizo hilo ninaomba serikali kwamba wakati inapopitisha hizo pendekezo, waweze kuliangalia.

Tatizo lingine ni habari ya electricity. Tana River pia hakujakuwa na electricity kutoka tupate uhuru. I think so far Tana River is one of the neglected areas in terms of electricity. Ukiangalia Lamu, wanayo, uliangalia hata Garissa, wanayo, Tana River alone, I think it is only Tana River hatujapata

Hapa Tana River we have got a lot or resources ambao tunaweza kufanyia kazi hiyo electricity but we have been neglected in that area.

Ukiangalia habari ya TV, watu saa hii wako dot com, sisi we are still in the uncivilised era in Tana River. Watu wako dot com, mambo ni ma-Computer, ma TV na what have you lakini in Tana River, hata hizi booster za kwamba inashika waves za TV, hatuja wekewa and yet we are saying that we have uhuru. What sort of uhuru do we have in Tana River? We have not enjoyed the uhuru.

Tumebaki nyuma kimaendeleo kabisa. Ukiangalia sehemu mpaka Malindi hapo, hapo Gongoni Gongoni hapo, wanaangalia latest news za TV, Tana River hakuna. Ukiangalia Lamu, majirani wetu tu hapo, wanaagalia news kutokana na TV, Tana River hakuna. Ukiangalia Garissa, wanaangalia news kutoka TV, Tana River hatuna. Why are we neglected like that? We are unfortunate. The government has to do something on that area.
Kwa hivyo Bwana Mwenyekiti, uangalie hiyo maneno.

Jambo lingine ni kwamba Tana River yetu it has got a lot of potential in terms of land resources and also animal resources but currently ukiangalia, there is sabotage. Let me term it as sabotage because all the irrigation schemes, plus village irrigation schemes have been paralysed or rather have been killed and as a result of that, there is great poverty that has affected the people in the District. For example ukiangalia shule yetu ya Hirimani hapa, it is composed of students from the settlement schemes, they cannot pay fees because the Bura irrigation scheme has failed and the government had been so reluctant, it was not serious to improve on that or to rectify that problem. Therefore poverty has stricken the settlers around Bura and they cannot even pay fees to our school.

Sasa ninatoa hayo maoni ya kwamba serikali iangalie kufufua hizi irrigation schemes zote za Tana River ili iondoe poverty kwa wananchi wa Tana River kwa sababu tukikuza mimea, tutaweza kupata pesa za kuwatoshelezea watoto wetu mahitaji ya shule; kuwalipia fees, kuwapatia chakula na kadhalika maana tunategemea mimea na mifugo. Kwa hiyo area hii serikali imemaliza kilimo. Ukiangalia Bura Irrigation Scheme used to be the best cotton producing area in Africa but there was a lot of sabotage and it has failed completely. I don't know why, so the government has got to interverne on that one.

Let me continue. Ukiangalia kuna haya mambo ya loans, bursary, bursary fees in the universities: Hizi universities za Kenya, watoto wanapewa loans na kusoma lakini ukiangalia, serikali haijafikiria ama iweke sheria ya kwamba hizi mid-level colleges

plus secondary schools waweze kutengewa pesa ili waweze kusomea. Pesa yote inapewa universities za ma loan na kadhalika, while they had forgotten that there are also some middle level colleges plus secondary schools which will require those loans so that they can continue with their education. There are so many poor people, there are so many poor students who cannot raise fees to join those middle level colleges and what have you, so the government has to do something on that area.

The other issue ni hizi power za President: The powers of the president, kwa maoni yangu, ninaonelea ya kwamba zipunguzwe kwa sababu some of the presidents are misusing that clause that they are above the power, that they can do anything na utakuta ya kwamba wana mpaka powers za ku-appoint and fire senior people. Kwa mfano, they have got powers to appoint these managing trustees, ambassadors, senior civil servants and what have you. If that is the case, it means that those appointed people will be puppets of the president. The moment they mess up or the moment they don't do as per the president, they are fired so they cannot work effectively, they cannot work without being swindled here and there. The president can swindle them. Kwa hivyo kwa maoni yangu ninaona ya kwamba hii maneno ya the president appointing senior people, hii maneno iwachiwe Bunge manake kama President atamu- appoint may be managing trustee wa mahali fulani, halafu huyo managing trustee hakukubaliana na president, the next day ataambiwa wewe hauko kazini. Anatolewa na hali hata hakufanya makosa, ni kwa sababu hakukubaliana na president kwa ile mpango yake.
Ningependelea hizo powers zipunguzwe.

The other issue is about the election of councillor and MPs: Some of the coucillors and MPs in Kenya have got low academic backgrounds. Some of them have not even reached form four level and that one has brought low quality decision making in terms of development, in terms of contributing to the government and what a view.

**Com. Mutakha Kangu:** What do you propose? What level do you propose?

**Mr. Baleza:** Okay. With the councilors, I propose that the minimum academic qualifications or background should be at least form four level so that they can make rational decisions and contribute effectively when they go to Parliament.

**Com. Kangu:** I think you have made your point. And the MPs?

**Mr. Baleza:** The MPs should have a certificate of form four level. At least they should have division three and above, division three in those days, most of them had learnt those days, the former days. Division three and above or rather D+ and above. They can make rational decisions when they go there and even contribute effectively during the Parliament sessions.

We have the issue of title deed in the district. Since uhuru, Tana River was neglected in terms of issuing of title deeds until recently when that programme started, but unfortunately I heard that that programme had stopped because of the clashes and what have you. It is my suggestion that the government should strengthen that programme to continue so that land can be issued

with title deed to minimize controversies and problems, because the moment you have the title deed, that land belongs to you and you can be able to invest on long term projects because it is yours but if there is no title deed, then you cannot develop that land. So we need title deeds, especially in the arable areas.

**Com. Mutakha Kangu:** Time is over.

**Mr. Baleza:** Give me just one minute.
Finally but not least, on the issue of increase of salaries to civil servants and other workers, I can say that the government is actually overlooking in some of the areas. If you move around and do a survey in most of the areas in the country, you will find that the middle level cadres are the ones who do the donkeywork. They normally do the donkeywork while those senior people, the most senior people, do the work of signing and what have you but when it comes to increment of salaries, the middle level cadres who normally do the donkey work are left, they are not awarded effectively, the ones who are awarded are the senior people. Why that discrepancy?

**Com. Muthaka Kangu:** That should be all with you Mwalimu. I think we have given you enough time.

**Mr. Balesa:** With those few remarks, thank you very much. Can we have Noor Aabarufa Shemo.

**Noor Shemo:** Commissioners, wananchi, Asalaam Aleikum?

**Audience:** Aleikum Salaam.

Noor Shemo: Mimi ninaitwa Noor Abarufa Shemo, nitatoa maoni yangu binafsi.
Nitaanza na umilikaji wa ardhi: Ardhi isiwe chini ya serikali kuu ama serikali za mitaa ama watu binafsi. Iwe chini ya wazalendo halisi wa hapo. Hapo nina maanisha ya kwamba kama sisi watu wa Tana River, huwa tunapata matatizo mengi kutokana na hii mambo ya umilikaji wa ardhi. Pengine mtu kutoka juu aende akarudi mpaka mtoni imekuwa ni shida. Kwa hivyo tungependa kuwe free kwa wazalendo halisi, wakaaji tangu zamani.

**Com.?** Kitu gani hiyo?

**Mr. Shemo:** Umilikaji wa ardhi.

**Com.?** Na ukisema wazalendo, ni watu gani?

**Mr. Shemo:** Wazalendo wa halisi ni kama sisi wakaaji wa Tana River, vile sisi tuko hapa Tana River, tuko Pokomo, Orma na

yule ambaye pengine wametoka nje. Unajua kama sisi hapa tunapakana na watu wa North Eastern na unajua watu wa North Eastern pia wanapakana na Somalia na Somalia hawana serikali. Kwa hivyo lazima iwe chini ya wazalendo halisi wa Tana River.

Elimu ya watoto wa shule: Elimu iwe bure kwa watoto wote wa nchi hii na mzazi atakaye kataa kupeleka mtoto wake shuleni ashtakiwe na kufikishwa mahakamani.

Serikali za mitaa: Mayor, mwenyekiti wa baraza za wilaya, wachaguliwe na wananchi wenyewe na vipindi way kuhudumu iwe miaka nne.

Elimu kwa madiwani: Madiwani wawe na elimu ya shule ya msingi, yaani primary school; hapo nikimaanisha ya kwamba kuna wengine wanapendekeza ya kwamba form four au nini, sisi hatuna hiyo, tunaangalia mtu ambaye anafaa kwa sababu hauwezi chukua fisi, aende akuchungie mbuzi, si atakula amalize? Huyu mtu, hata kama yeye ni form four, kama yeye si mtu mzuri, utakubaliana naye?

Bora mtu ajue kusoma na kuandika.

Wabunge maalum ama madiwani maalum: Uteuzi kama huo uondolewe na badala yake, mishahara wanayolipwa, marupurupu, zitengwe kwa miradi muhimu ya maendeleo kwa sababu hakuna kitu wanafanya na umaskini ndiyo hii inatukabili hapa.

Utendaji kazi kwa wabunge: Wabunge wafanye kazi masaa ishirini na nne kama sivyo, wapunguzwe mshahara yao na hiyo pesa itengwe kwa miradi muhimu ya maendeleo.

President awe ni mtu ambaye amefika chuo kikuu na umri uwe ni miaka arobaini na tano.

Bunge lidumu miaka minne.

Stima: Kama vile sisi watu wa Tana River, tulipopata uhuru, hatujaona kitu inaitwa stima. Stima sisi tukitoka hapa tukifika Malindi tunaona stima hata watoto wetu hawajui stima nini. Sisi wale tumetembea ndio tunajua, wanaiita mayai ya kuku.

Kwa hivyo katiba ishughulikie hiyo kitu, hata sisi tufurahie kitu kama hiyo.

Kwa hayo machache, sina mengi, asanteni.

**Com. Mutakha Kangu:** Hakuna swali, tumpate Isaac Karhayu.

**Issac Karhayu:** Chairman na Commissioner, na wageni ambao mmekuja nao, na viongozi wenzangu ambao wamekuja kuchangia mjadala huu wa Katiba. Yangu tu ni mapendekezo ya kwamba kuwe na shule bure kutoka standard one mpaka standard eight.

Ikiwezekana President awe amefika kiwango cha university kwa sababu tukichagua President ambaye hajasoma, kuna udhaifu mkubwa sana, kama vile tunavyoona sasa.

Na mfumo wa utawala: Mimi naweza kuchangia upande wa majimbo lakini sisemi ya kwamba ati watu wa sehemu zingine wapate kuondolewa katika hilo jimbo, lakini iwe ni majimbo on revenue, yaani asilimia sabini na tano ibaki katika lile jimbo na asilimia ishirini na tano iwe katika serikali kuu. Wanaweza kutengeneza budget zao na sabini na tano inaweza kuangalia miradi ya jimbo lao kwa sababu sasa inaonekana kama itaendelea mfumo kama ule ule, basi ni wazi ya kwamba majimbo mengine yatakuwa mkia mpaka Yesu atakapokuja.

Changio lingine ni juu ya wafugaji: Ikiwezekana, kwa sababu za shida zinazotupata, wafugaji waweze kutengewa sehemu zinaitwa ranch na waweze kupatiwa title deeds katika hizo ranch na waweze kulisha pale ndani ili kuzuia msongamano ama makosano kama vile hali inavyojitokeza wakati huu.

Nitachangia tena lingine la uchaguzi: Sehemu zingine unakuta ya kwamba watu wanataka mtu fulani lakini unakuta askari wanakwenda pale, wanakuwa wakali mpaka wanaingisha masanduku ya kimagendo na wanasaidia yule mtu kupata kura na kuwa mshindi. Kwa hivyo askari wasiwe na shughuli zozote wakati wa uchaguzi.

Nitachangia kwamba Tana River tumeachwa nyuma katika hali za redio. Saa hii hapa Tana River ni KBC pekee yake ndiyo tunasikiza ambapo ukienda sehemu zingine unakuta kuna channel nyingi ambazo wanazisikiza na wanapata kupevuka mawazo yao. Hapa ni KBC pekee yake, kwa hivyo frequencies ambazo zinakuja hapa, ziruhusiwe hata zile za channels zingine ziingie Tana River ili nasi tukapate ku-enjoy the national cake kwa upande wa mawasiliano.

Ninachangia pension: Pension unaweza kwenda retire na cha ajabu ni kwamba unaona mtu ameenda retire, ameishiwa na kila kitu na anaweza kukaa miaka kumi, hata zaidi ya miaka kumi bila ya kupata pension. Hali hii imeleta matatizo mengi kwa pensioners na kwa hivyo mnapoandika hiyo Katiba, ikiwezekana mtu anaporetire tu, the next month, awe anapata pension yake kabisa.

Nikichangia pia hapo, iwapo pensioner amepata matatizo pengine ya kufungwa jela, huyo mtu, matatizo ni kawaida kumpata mwanadamu, awe anapatiwa, bali asiwe anapatiwa vikwazo ya kuwa kwa sababu umefanya makosa umeingia jela, kwa hivyo hautapata pension yako.
Je kama hatapata pension, hataweza kujisaidia na nini katika maisha yake? Kwa hivyo mapendekezo yangu ni kwamba apatiwe bila masharti yoyote.

Ninafikiri nitakoma hapo, ili wengine nao wapate kuchangia. Asante.

**Com. Muthaka Kangu:** Na Yusuf Ware? Huyo ni observer, Shukri D. Kolio? Pia yeye observer, Osman Bonaya? Hayuko. Na Ahmed S Mohammed? Na ukianza Bwana Ahmed na wengine wenye hawajakuja, ujue unaanza na kutaja jina lako, kwa sababu tunanasa mambo yote katika hii machine kwa hivyo lazima tupate hata jina lako na ukimaliza unaandikisha pale na uweke sahihi kwa register yetu. Basi tukusikize Bwana Ahmed.

**Ahmed Mohammed:** Asante Mabwana Commissioners na wananchi. Ningependa kuchukua fursa hii kwanza kidogo nichambue kidogo mambo ya historia. Singependa kuchukua nafasi kwa sababu zile presentations zangu zote zitakuwa very brief. Jina langu ni Ahmed Sheikh Mohammed and I am the project coordinator, Tana River Peace, Reconciliation and Developent, so ninawakilisha civil society.

It is known through history that self-identity and ethnicity is a very essential factor in Kenya. It has provided a basis of self-definition and appropriation of socio- cultural identities. However, it has engendered negative perceptions in relation to our national cohesion.

Ethnicity has more intensely founded a sub-national identity and in effect, more Kenyans will view themselves as belonging to the sub- national and then secondly to the national. In this dual citizenship, the sub-nationality, will become very important, basis on which materials and other priviledges of the government are shared.

Ethnic priviledges redefine political power, leadership and governance in general.

The government was therefore seen as an avenue for material gain and endless favours to ethnic groups from which the leaders came. This is the root cause of retrogressive culture of ethnicity, of eating syndrome hence the talk about time for this or that tribe to eat.

As a political goodwill, the constitutional arrangements would be an ideal basis for a government of national unity. That is my proposition, because of the nature of ethnicity we have.

To avoid all these proplems, we need a government of national unity because it will address immediate national reconciliation and national ethnicity devoid of suspicion and mistrust.

To come back to my proper presentation now, is that, at the national level, the President, I advocate for a very strong President but with checks and balances.

The issue of a Prime Minister is a creation of those people who want to stay in power or who want to position themselves, otherwise it is not of much interest to us.

The President be elected together with his Vice President. The Vice President should be elected directly by the people on any political party ticket.

Both of them should gunner fifty per cent of the total popular vote, at least.

The President should be the head of state and Commander in chief of the armed forces while the Vice President should be the head of government.

The President should not be above the law as is the case now. He should serve two five-year terms and the Vice Ppresident three five-year terms.

The MPs should serve three five-year terms only.

Education: It is a problem in the pastoral and in all hardship areas that the attitude towards education has been very negative and for that matter I propose that:
One: Education in the first place at primary level should be free but compulsory.
Secondary level should be free to marginal and hardship areas of Turkana, Samburu, Isiolo, Marsabit, Moyale, Garissa, Mandera, Wajir, Tana River and Lamu.

Citizenship: A Kenyan should be identified by a passport, not an identity card because at the moment we have a lot of identification papers; we have birth certificate as an identification paper, we have the ID card, we have the passport, we have the screening cards, we have employment cards, they are just too many papers in our pockets. So to avoid all these lapse, we have to have only one which is very important, you can use it within and outside, the passport.

Honestly speaking, the current Constitution has been so biased when it comes to citizenship because Section 87 of the Constitution is very clear about where we belong, the people of all this region, and even Coast province, North Eastern including Tana River and whatever because you cannot get a passport without going through a very rigourous and very embarrassing situation. If you are to get a passport today, you are told to fill a hundred and one papers from the Sub-chief, Chief, DO, DC and then the moment you reach the immigration office in Nairobi, the PP7 clearly identifies who we are because it says persons claiming to be Kenyan, by the way I don’t know, because how…

**Com.?** It is all right, may be you could propose the solution.

**Mr. Sheikh**: The solution is that we should be registered. If a Kikuyu is given one paper for filling the Kenyan passport, then

anybody from any of the marginalized areas; from coast, from North Eastern from any other part should fill the same, we should not be loaded with a hundred and one papers.

About economic empowerment: I propose for this area to be given investment promotion incentives with specific special support to the livestock sub-sector because honestly, when it comes to livestock, this is our life. Pastoralism is a way of life like anything else, like coffee, like sugar, like tea but in the current constitution, there is nothing much for the pastoralist.

We have a lot of animals with us. The drought comes, wipes them out, we have no market for them, the government says we should discard normadism. If were to discard, where do you go, where do you take these animals because we have no market for it, we have nothing, the government has not put in place any mechanisms for the patoralist on dispose of the animals or to improve on the livestock.
There is no market, there is no factory, so I propose that factories should be placed in all livestock areas, pastoral areas and the government should look for outside export market like the way they are doing for coffee and other sectors.

I also propose the establishment of a ministry of pastoral affairs. I believe there is a minisry of livestock, yes, but it has nothing in place for the pastoralist.

The other thing is about the provision of basic infrastructure: It is a nightmare in all this marginalized areas; this is because of marginalization. This marginalization has to go, so that the basic infrastructure and whatever people have been talking about, communication and all those things be put in place.

The other thing is about positive discrimination in senior public service appointments: In these marginal areas, we have been kept too far away from the rest of Kenyans and from the rest of our brothers and for that matter, for us to catch up with them, for us to be at the same level with them, there should be some element of positive discrimination in appointment to senior position of the government, for us to feel that at least now we are in the government. This one should be quaranteed by this new Constitution.

The Judiciary: Establishment of an enlarged and improved Kadhi's court. A Kadhi should be qualified in both law and Islamic Sharia. Any Kadhi to be appointed to this positon must have the two qualifications concurrent. At the same time, we should also have Islamic jails.
A Kadhi should be given full power like any other judge or any other margistrate.

About the land tenure: All the government land should be reverted to the community under the custodyof traditionally established council of elders because we have no faith in the current local government authorities. They are supposed to be holding in trust the land for the community.

The other issue is about water: River Tana is the life of the district of Tana River. It should be protected and the people of Tana River should be given the right over the use of Tana River like Egypt is given the right over use of River Nile when we know that 80%, almost a hundred per cent, of the Nile water comes from the East African region but Egypt, right at the corner, at the delta, is given the right over the use of the Nile, so Kenyans, Ugandans, Tanzanians are not allowed to use lake Victoria for any major irrigational purposes because that one is enshrined in the Nile agreement of 1929. Why don't we do the same for Tana River because putting up a lot of dams on the upper stream denies the people down stream a lot of rights over the use.
That is why most of these schemes actually collapsed. The Hola scheme actually collapsed because the river moved away from its site almost two or three kilometers, from the site where the water used to be got.

**Com.?** What is the solution?

**Mr. Sheikh:** The solution is that people downstream should be given absolute right over the use of the river.

The last one is about the Electoral Commission: We know the Electoral Commission at the moment cannot do anything much. I propose that the Electoral Commission should be empowered by giving them a court that deals with election offences, that is directly under Electoral Commission and a police unit, police electoral crime which is responsible to the Electoral Commission of Kenya. Those are the few presentations I had. Thank you.
**Com. Mutakha Kangu**: Thank you very much Mohammed. You can sign there. Mohammed Idle Omar, an observer, Bashira Henry? Bashira Henry is an observer. Issa Shambu? Zacharia Owino? An observer, Khalija Ali, an observer, Mohammed Galole?

**Mohammed Galole:** Asante. Bwana Chairman, na Commissioners ambao waliandamana na yeye, viongozi wetu wa Bura, watoto, Salaam Aleikum. Kwa jina naitwa Mohammed Galole, Councillor wa Irmani.
Nikitoa maoni yangu nitaanza na elimu Bwana Chairman: Kenya wakati ilipata uhuru tuliambiwa walichukua ahadi kwa watu wake kuwa vitu tatu itakuwa inapotezwa; moja ikiwa ni ujinga,
Bwana Chairman, sehemu yetu hii, hata wakati huu sisi tuko na ujinga na ikawa Katiba imerudishwa tupange ingine. Tuna shida ya elimu, na ningependekeza kama tutapanga ingine, sehemu hii yetu, kwanza Kenya ama viongozi wale walichukua hiyo ahadi, tupewe fidia kwa sababu ya sisi, wananchi wa sehemu hii kutumiwa vibaya.

Bwana Chairman, shule ningeomba isiwe hiari ya mtu, iwe ni lazima. Mtu apelike mtoto yake shule. Asipopeleka iwe ni hatia.

Bwana Chairman, watu tunaambiwa nafasi ya waalimu kuandikwa hakuna na sisi wakati huu ndio tunapata vijana watatu katika district hii. Vikwazo kama hiyo iondolewe kwa sehemu ambayo viongozi wetu wa nchi hii walitulalia kwa sababu hiyo wakati wowote ambao tutapata vijana waandikwe.

Bwana Chairman, vikwazo vingine, shule mpya haiko kwa programme ya serikali. Ningesema vikwazo kama hiyo iondolewe. Kama mwananchi anataka kujenga shule mahali, isiwe inawekwa hizo vikwazo. Shule ipewe namba, mwananchi ajaribu.

Bwana Chairman, vile viongozi wengine walisema, ningeomba shule iwe ni lazima na bure tena.

Bwana Chairman, nitarudi kwa ma chief: Ningesema vile mmoja alitangulia, wachaguliwe na wananchi. Sababu ni kuwa mtu akichagua chief kwa watu, awe amepata kirauni aje akae hapa karibu miaka ishirini na tano, kama atakuwa hatekelezi kazi yake, maendeleo haitakuwa hapo, na labda kifo imchukue, hatatoka huko, haendi transfer, itakuwa shida kwa hiyo sehemu, ndio sababu tunasema achaguliwe.

**Com. Mutakha Kangu:** Kwa muda gani?

**Mr. Galole:** Muda wa miaka mitano.
Naomba ma chief pia wakienda leave, wapewe allowance ya leave kama civil servants wengine wanavyopewa, na wao pia wapewe. Ijapokuwa hawaendi nyumbani mbali, lakini ile kazi wakonayo ni nyingi sana. Kwa hivyo ninaonelea hata kama haihesabiki kilomita pale, ataenda sehemu yake atembelee watu, kwa hivyo apewe hiyo allowance ya leave kama wengine.

Kitambulisho: Kiongozo ambaye ni mzaliwa na hatoki pale, sisi tunajua ni chief, haendi transfer. Ningependa ma chief wapewe nafasi, wasiwe wanaongozwa na ma DO ambao wamekuja transfer, chief awe na power zaidi ya DO mahali pa registration.

President: Ningelipendekeza wakati mwingine tuliambiwa muda President atakaa na iwe sheria haimruhusu ni kama miaka kumi. Kwa maoni yangu mimi nimeona miaka mitano baadaye asimame kwa kiwanja achaguliwe, miaka tano mingine asimame achaguliwe, huo mwingine unayokuja hana ruhusa ya kusimama.

Mimi ningelipendekeza kama huyu mtu pengine anapendwa na wananchi, kwa nini sheria imkataze? Kwa hivyo kwa maoni yangu ningesema sheria isimzuie watu wakataze yeye kura. Asikose kwa upande ya sheria , asikoze kusimama kutafuta kura.

**Com Salim:** Hata baada ya kupata miaka mitano ingine,ikiwa watu wanamtaka aendelee?

**Mr. Galole:** Aendelee. Sheria isimzuie.

**Com. Salim:** Aendelee mpaka lini?

**Mr. Galole:** Aendelee mpaka kufa kwake kama watu wanampenda.

**Com. Mutakha Kangu:** You have one minute.

**Mr. Galole:** Nimesema kama Electoral Commission ya nchi, isichaguliwe na mtu mmoja kama President, ichaguliwe kutoka sehemu zingine ama achaguliwe na viongozi wale wako pamoja na president.

Bwana Chairman, watu wa kuhamahama, wakati huu kama Tana River tumelaliwa sana. Watu wa sehemu ingine ndiyo wanatuingilia sana, kutoka nchi ingine hata wakimbizi wako hapa. Ningesema kila mmoja, wananchi wetu, kila mmoja arudi katika district yake. Nikisema hivi, katika recruitment ya serikali yote, ndiyo tuna shida. Nafasi ambayo tunapata inaenda kwa district ingine. Kwa hivyo ningelisema nafasi kama hiyo ya recruitment pia ikitokea iende kwa district na iwe wananchi wa pale, vijana wa pale ndio wapate.

Yangu ni hayo, nasema asante sana.

**Com. Kangu:** Tupate Peter ole Kabusya, hayuko, Fredrick Otieno, hayuko, Mwana Hamisi Homa?

**Mwana Hamisi Homa:** Maafisa wote wa Katiba pamoja na wananchi tuliokuja pamoja. Nashukuru sana kwa kualikwa hapa. Hamjambo?

**Audience:** Hatujambo.

**Mwana Hamisi:** Yangu ni maoni kuhusu…..
**Com.?** Tuambie jina tafadhali.

**Mwana Hamisi:** Jina ni Mwana Hamisi Homa. Ni Chairlady wa Maendeleo ya Wanawake, Bura Location.
Ninaongea kuhusu hapa kwetu kwa niaba ya tuliokutana tukaandika memorandum.

Tumeonelea kwanza, ile kawaida yetu ya zamani ya watoto kutahiriswa inaumiza sana. Mimi ni mmoja wa kusaidia na sisemi, ninasaidia tu wale tunatahirisha pekee yake, wote tunasaidia na hakuna mzazi ambaye ako na raha lakini hasa kwa sehemu hiyo ni dhiki sana.
Tumeamua tuwache hiyo desturi, wengi wetu wameitikia na kuna wale ambao hawataki.
Kwa vile hawataki, nimeomba serikali watufanyie mkazo, watupatie nguvu ya kutembelea wale wenzetu na kuwaelezea ili wapate kufahamu ile shida watoto wetu wanapata.

Kingine: Sisi wanawake tuko na shida sana na mimi ni mmoja ingawaje hiyo sehemu mimi nimetoka lakini watoto wetu bado

wanatembea kwenye hiyo sehemu. Wanaume wanatuonea. Ukikosea, hatakujibu na mdomo, jibu ni mkono. Hata tumechoka hapa tulipo wanawake jamani.
Serikali mtuangalilie haya mambo. Muwaambie wanaume kwamba hata sisi ni binadamu kama wao tu. Tukikosea, wawe wanatueleza tukaweza kusikia.

Hayo ni maoni nimetoa kutoka kwa wanawake wa hapa Bura.

Na tena, nafasi za kazi: Nafasi za kazi kwa vijana na wasichana; wote ni wetu lakini katika wasichana huwa ni chache sana. Kwa hivyo wasichana, ingawaje kuna wengi wanalia kwamba hawasomi, lakini sisi wa Tana River, wanachelewa mmoja ama wawili, lakini wengi wao wanasoma lakini wasichana wananyimwa sana sehemu ya kupata nafasi.
Tunaomba serikali iangalie sana haya mambo maanake kila mtu akipata, amejipatia, hakuna yule anapata anampatia mwenzake. Kijana akipata, akiwa kijana anajijenga, akioa, anajisikia yeye ako kwake. Na msichana pia akipata atajijenga, akiolewa ajisikie kweli mimi nimeondoka na ninaenda mahali na akienda anaonekana kama yeye ni mtu. Hiyo ndiyo vile tunataka kama ingewezekana.

**Urithi:** Urithi kwa upande wa wanawake, sisi tunafinywa sana. Kuna wengine wanaolewa na waume na pahati mbaya asizae, anakaa na huyo mume, wanalima, wanalima, akifa, pengine wale mashemeji wanaona vile wakikuwa wanaendelea, hiyo sehemu yao wamefanya vizuri sana. Sasa mume akifa, akibaki mke kwa vile hana mtoto na hakuna vile atajitetea. Mwafrika hasa kikubwa ni mtoto, ndiyo utajitetea useme "ninakaa hapa kwa ajili ya huyu mtoto wangu. Mkinifukuza kwa shamb na huyu mtoto ataenda wapi."
Kama sasa Mungu amekunyima kuzaa, unafukuzwa tu kama mbwa. Serikali iangalie hiyo mambo. Hiyo ndiyo maoni yangu.

Ya pili, pengine tena ya mwisho, sisi tunazaliwa wasichana na wavulana. Babako yuko na mashamba makubwa makubwa lakini leo akifa, unaona wavulana wanapata sehemu, sehemu, sehemu, lakini wewe unaambiwa ni mwanamke, hutapata sehemu. Si afadhali hata huyu mume kama atapata maguu hamsini, angaa hata wewe upate maguu ishirini, ya kupangusia machozi ya mzee wako. Hii ni kazi yake aliyofanya na ni mahali amekulelea, kijana akipata maguu hamsini upana, wewe ukipata maguu ishirini upana, angaa utafutia machozi. Lakini hapo sisi hatuna, tunalia, hapa Tana River hakuna hiyo desturi, mwanamke hana share kabisa kwa babake, babake akifa, amekufa basi.

Hiyo ndiyo tunalia. Ninashukuru sana, asanteni, na pale kwenye kuandika nikuambie wazi, mimi nimenyimwa elimu na wazee wangu. Nilipoolewa ikaja ngumbaro, nikapambana na ulezi mgumu, sikwenda ngumbaro chochote. Nikaamua ngumbaro na mtoto wangu akiwa chokoraa, ni kitu gani mzuri? Nikasema hapana, mtoto akisoma, ni afadhali kuliko niende ngumbaro.
Kwa hivyo mimi ni Mwana Hamisi Homa lakini sijui kuandika.

**Com. Idha Salim:** Ngojea swali moja mama. Asante sana kwa maoni yako. Ningependa kuluuliza jambo moja. Umesema

ukija wakati wa kurithi, wanawake hapati ardhi, hawana chochote kabisa, kabisa. Tuseme hao, kwa majina yako naona kama ni Mwislamu na hao wanawake ambao, tuseme, pia ni Waislamu, je hao ambao wanakataa kuwapa wanawake haki zao chini ya sheria, pia ni ya Waislamu.

**Mwana Hamisi:** Wote ni Waislamu.

**Com. Idha Salim:** Kwa hivyo sheria inasahaulika hapa. Kama tujuavyo, msichana hupewa nusu ya sehemu ya mvulana.

**Mwana Hamisi:** Hapewi chochote si kwetu hapa, kwetu Tana River. Ukianzia kidini, mpaka mahari, twajua sisi tuko -----------. Ikiwa baba yenu amekufa, hapa nyumbani mko wavulana na wasichana. Pengine vijana wameoa na wasichana wameolewa. Mtakuja hapa mlie, ile kahawa inapikwa hapo, pamoja na ile chakula unakula, basi umesharithi.

**Com. Idha Saliim:** Sijui yuko Kadhi ama koti ya Kadhi hapa Tana River.

**Mwana Hamisi:** Kadhi wa koti yuko.

**Com. Idha Salim:** Na mkamwendea?

**Mwana Hamisi:** Hatujaenda, sisi hatujawasilisha kitu hasa mwaka huu ilipoletwa hii Katiba tumeshukuru.

**Com. Idha Salim:** Kuna haja hapa ya kumwendea Kadhi. Yeyote ambaye amedhulumiwa na mzazi wake, akasahauliwa kwa kuwa ni msichana tu, aweza kumwendea Kadhi, akahakikisha kwamba sheria ikafuatwa. Hilo ni kama kuwapa ishara tu kwamba yawezekana, maana ikiwa baba ni Muislamu na watoto ni Waislamu, msichana anayo haki zake na kwa hivyo maendeleo ya wanawake na wewe ukiwa ni kiongozi, inataka uwaelimishe haki zao na wapatiwe haki zao.

**Mwana Hamisi:** Sawa.

**Com. Mutakha Kangu:** Asante basi. Na tupate Yakub Komora.

**Yakub Komora:** Asante sana ma Commissioner na wananchi. Salaam Aleikum. Mimi ninaitwa Yakub Komora, ni chairman ya Supkem hapa Bura Division na nitatoa maoni yangu.
Kwanza nitaanza na upande ya masomo: Sisi katika hii wilaya yetu ya Tana River masomo yetu ni duni, hatuna masomo, katika hii wilaya yetu ya Tana River, hasa sehemu za juu huko, kama ijeremani, location nzima ambaye ziko kilomita nyingi inakaa kuwa shule moja na hiyo shule huenda ikawa imeanza juzi juzi.

Kwa hivyo iwe katika Katiba, katika hii district yetu, isemekane masomo ni lazima na watoto wasomeshwe bila malipo. Serikali iwasimamie iwasomeshe kutoka darasa la kwanza hadi form four.

La pili: Katika sehemu hizi za wafugaji tuwe na soko huru kwa sababu sisi ni wafugaji, hatuna soko muhimu katika hii wilaya yetu, ambayo inajulikana siku fulani ni soko ya mifugo, watu wakutane, wananchi wapate mapato. Kwa hivyo tuwe na soko huru katika hii wilaya yetu, kama sehemu tatu hivi, ijulikane kote nchini ili siku hiyo tupate watu kutoka sehemu mbali mbali wakija kununua mifugo yetu.

Tatu: Katika hii wilaya yetu, masomo yetu iko chini. Kwa hivyo wale ambao wanasimamia kama sehemu za location, ma Councillors, wasiwe na lazima kuwa wamesoma kwa kuwa sisi hatuna masomo.

Katika hii wilaya yetu ya wafugaji, waalimu katika wilaya nzima wako thelathini pekee yake. Kwa hivyo kama tungelikuwa na masomo, hatungetatizika. Hatuna masomo kwa hivyo haiwezekani mtu kutoka nje aletewe sisi tumchague.
Kwa hivyo yule mtu wetu ambaye yuko pale, hata kama hana masomo, tutamchagua na iwe katika sheria.

**Com. Mutakha Kangu:** Katika cheo gani?

**Mr. Komora:** Katika cheo cha Councillor kwa hivyo isiwe lazima awe na masomo.

Na pia chief; kama sehemu hii yetu ambayo watu wanakaa kabila mbili, iwe ni lazima, kama chief ni kabila moja, assistant wake awe kabila ingine kwa sababu hiyo imeleta shida kubwa katika hii wilaya yetu.
Na pia hawa ma chief wachaguliwe na wananchi na isiwe ni lazima, kwa vile sisi wakazi wa area hii hatuna masomo, awe na masomo. Mfano au sababu, kuna area yetu ambayo walikuwa wamekaa ma chief ambao hawajasoma na assistant chief wake wamepata ma seniors, kila mmoja ametoka akiwa senior na katika hiyo location, hawajapata matatizo hata kwa siku moja, lakini baadaye imesemekana ya kwanza ni jua kali, wawe watoto ambao wamesoma ndio wanachaguliwa.
Wamechaguliwa, serikali wamechagua, shida wakati walipata hiyo crown mpaka leo mzozano, clashes iko mingi. Kwa hivyo kusiwe na lazima ya masomo.

Upande ya Waislamu: Sheria yoyote ya Wakristo isiweko kusimamia Waislamu. Waislamu wawe free. Sheria ya Waislamu imeshaandikwa kwenye kitabu, hakuna wakati hiyo Katiba itabadilishwa mpaka dunia imalizike ndiyo hiyo Katiba ya Waislamu ibadilishwe.

Urithi wa wanawake iko katika dini ya Kiislamu na kwa hivyo mtu yeyote ambaye amenyimwa haki yake ya urithi anaweza kwenda kwa sheikh yeyote kwa sababu urithi ni haki yake, kila mmoja awe na haki ya kurithi baba yake. Hiyo iko katika sheria ya dini ya Kiislamu. Kama hiyo sheria haijatekelizwa kwa hivyo wako ma Kadhi katika district hii ama katika wilaya ingine.

Kama ikiwa huyu mtu hajakufanya mzuri, kwa hivyo unaweza kwenda kwa ma Sheikh ili uelekezwe itakuwa namna gani.
Yangu ni hayo, asanteni.

**Com. Muthaka Kangu:** One question ndugu ngoja kidogo.

**Com. Idha Salim:** Samahani Sheikh, Bwana Yakub, umesema kwamba ikiwa chief ametoka kabila moja, assistant chief atoke kabila nyingine. Kuna makabila mangapi hapa?

**Mr.Komora:** Hapa area yetu kuna kabila mbili, sehemu mbili ya kila division iko kabila mbili.

**Com. Idha Salim:** Asante. Niliona kwamba kama kuna zaidi ya mbili, italeta matatizo kidogo.

**Com. Mutakha Kangu:** Tupate Noor Mahmood.

**Noor Mahmood:** Tume ya Kurekebisha Katiba Wageni mashuhuri, wazee, vijana wenzangu, hamjambo?
Majina naitwa Noor Mahmood Samwel.
Ningependa kutoa maoni kidogo kwa upande wa haki ya wanadamu: Hasa Kenya, watu wa Tana River, tunatumiwa sana kama chombo kisichofaa. Kwa mfano mke wangu akishikwa, sina haki ya kumwona, ni mpaka niende police station, nitoe pesa ndio nimwone.

Cha pili, watu wetu hawajui haki yao na wanateswa sana. Huenda ikawa itokee vita baina ya kabila mbili, baada ya vita kuisha, badala ya aliye fanya makosa ashikwe, inakuwa ni GSU wanatumwa kupiga watu kama punda kwa sababu hawajui haki yao. Watu wetu wanaambiwa GSU hawawezi kushikwa na sheria, hawawezi kushtakiwa. Mimi ninashangaa sana kwani kabila zingine wanapigana Kenya na hakuna GSU wanapelekwa, hakuna watu wanapigwa kama punda, watu wa Tana River wanafanyiwa hivyo kwa sababu ya kutosoma.

Kingine nimeshindwa kujua, huenda ikawa kutokee kuna shifta wanatokea barabarani, kuna wizi unatokea, inakuwa vita sana, yaani wizi wa Tana River au Shifta wa Tana River alifanya kitu kisicho julikana dunia hii.

**Com. Salim:** Ungetupa mapendekezo yako tujue jinsi ya kurekebisha mambo ambayo yote ni manufaa. Cha muhimu ni mapendekezo yako ya kurekebisha.

**Mr. Noor:** Nashukuru sana. Kwa upande wa kuleta GSU na kupiga watu, ningependa waliofanya makosa washtakiwe, washikwe na pelekwe sheria na kama walifanya makosa wafungwe kama hawana hatia waachiliwe.

Ingine ningependa kuongezea ni uchaguzi wa Chief: Ningependa chief achaguluiwe kwa sababu mimi niko Bura na mtu anaenda kutoka mahali ingine anaenda kwa DC anahongana pesa, anaambiwa wewe utakuwa chief wa Bura na mimi simjui. Huenda ikawa kabila hiyo hatuelewani.
Kwa sababu hiyo ningetaka chief naye achaguliwe.

Kingine ni masomo ya Mbunge na Councillor: Sisi watu wa Tana River hatuna elimu. Ningetoa pendekezo au maoni kwamba tufanyiwe afadhali anayejua kusoma na anayejua kuandika upande ya Councillor na Mbunge, awe amemaliza form four na yuko na certificate.

Ingine, kuna viongozi wa serikali wanakuja mahali au wanaletwa mahali fulani, wanakaa kwa muda, baada ya kukaa kwa muda huo, wanapelekwa transfer. Bura irrigation scheme, kuna maneja moja aliletwa, mimi kufungua macho kwangu nilimwona pale hadi wa leo yuko hapo. Ningependa wafanyikazi wa serikali wafanye rotation na wapewe ma transfer, na wengine waje, huenda ikawa wataleta mabadiliko.

Ingine ni kitambulisho: Haswa watu wa Bura au watu wa Tana River au wafugaji, tuko na taabu sana ya kitambulisho. Kwa mfano, mimi ni Morma nakuta nimechukua kitambulisho. Ndugu yangu naye ameandikisha apewe kitambulisho, anaambiwa alete screening card naye si Msomali wala hakujua babake kitu hiyo, na anaambiwa alete. Taabu hiyo tuko nayo sana na hata hatujui, au wengi wetu hatujui mahali shida imetokea. Tunakuta watu wanateseka sana; unakuta msichana ameshaolewa akazaa watoto wawili, watatu, hana kitambulisho, anaambiwa enda rudi. Kila siku form yake iko pale, mara imevunjika hivi, wengine ni kihongo. Kimetusumbua sana huku Tana River.
Officer mmoja ukienda kwake, kama ni kitambulisho, anakuambia lete kitu kidogo. Sasa mtu wa kwetu naye anafikiri hiyo kitu ndiyo sheria iliyoko, yeye hajui kuna nini sasa inabidi atoe. Je, mimi nimetoa niko nayo, kuna ndugu yangu naye hana pesa na hajui hali ya kwenda, sasa inakuwa halali kabisa.
Maoni yangu ni hayo, ninashukuru sana kwa kuja kwenu, karibuni hapa kwetu. Asanteni.

**Com. Mutakha Kangu:** Tumpate Halima Gure.

**Halima Gure:** Asante sana Commissioners, kwa jina mimi ninaitwa Halima Gure, mimi ni Chairlady katika Bura division na nina maoni yangu hapa kidogo.

**Com.?:** Umesema wewe ni chairlady wa nini?

**Halima Gure:** Maendeleo ya Wanawake, Bura Division.
Kile kwanza ningesema ni upande ya elimu: Kwa maoni yangu naomba iwe bure.

**Com. Mutakha Kangu:** Wale wanaopiga kelele, tunawaomba mumpatie nafasi yule anazungumza, wale wanaandikisha pale mlangoni, jaribu kuzungumza kwa sauti ya chini, msimsumbue anayezungumza. Endelea.

**Halima Gure:** Upande wa elimu iwe bure.

Upande mwingine, wanawake hatupewi haki yetu kama ipasavyo. Tunanyimwa elimu, wanawake ndio wanafanya kazi ya nyumbani, na wengine hata nyumba kujenga, ni kina mama wanajenga, na hiyo ni kunyimwa haki. Tunataka kina mama tupewe haki zetu.

Na upande mwingine ni kusema, na mwingine mbele yangu ameongea, baba akiaga dunia, mtoto wa kike hana haki ya kurithi mali ya baba yake. Kama ni mashamba, ng'ombe, ama biashara yoyote. Huyu msichana hana haki. Baba akifa ni wavulana wanachukua hiyo mali, msichana sasa ni kurudi mkono mtupu, anakaa.

Upande wa kitambulisho imetutatiza. Headman akikuja anakupitisha, wazee wanakupitisha, assistant chief anakupitisha, chief anakupitisha, hapo, DO ambaye ametoka mahali ingine, hata hakujui ama hajui mahali unaishi, anakurudisha siku ya vetting. Sasa tungeomba Tume ya Katiba, hii mambo ya kitambulisho irudi mikononi mwa chief pale location.
Yangu ni hayo tu, asanteni.

**Com. Mutakha Kangu:** Doreen Adundo, observer, Harriet Kerubo, hata yeye amesema ni observer, Peter Kimathi?

**Peter Kimathi:** Commissioners wa Katiba, wananchi, hamjambo?

**Audience:** Hatujambo.

**Mr. Kimathi:** Mimi ninaitwa Peter Kimathi, Chairperson wa Makini Primary School.
Maoni yangu ni kusema, ningeomba serikali katika wilaya zote za Kenya zilizo nyuma, zipewe elimu ya bure, kama Tana River yetu, kutoka standard one mpaka standard eight.

Ningeomba serikali iweke sheria ya kwamba ma chief waingilie mambo ya elimu, wasimamie elimu yenyewe.

**Com. Salim:** Watafaidi kwa njia gani?

**Mr. Kimathi:** Watafaidi kuwa baada ya miaka ingine kumi, tutakuwa na viongozi wa kutuongoza.

**Com. Mutakha Kangu:** Lakini watatusaidia vipi?

**Mr. Kimathi:** Watatusaidia kulazimisha yule mzazi aliye na mtoto na hataki kumpeleka shuke, apelekwe shuleni kwa haraka.

Maoni yangu ingine: Katika Kenya kuna Schemes, zile area za scheme ambazo zimetengwa na serikali kwamba ni scheme isiwe ni ya watu binafsi. Watu wanasema hapa ni ketu huko ni kwetu, katika Kenya nzima, scheme zote zimeteuliwa na serikali. Mfano ni kama hii scheme yetu ya Bura. Hapa ni karibu kabila kumi na kitu ama karibu ishirini na kitu katika Bura. Umeweza kusikia vile wanasima kuwa tuko na kabila mbili au tatu. Scheme iko ma-kabila zote za Kenya .

Mali ya scheme, kuna haki ya mtu yeyote kuandikwa chief. Chief yeyote anafaa kuandikwa ni chief ambaye amesoma, afanyiwe interview. Mtu ame soma kwa sababu ataongonoza nchi vizuri.

Yale mengine, kwa sababu ya wale wilaya ziko nyuma, ningeomba serikali iwe na boarding katika kila division kwa sababu watu wako nyuma sana. Hasa hapa kwetu Tana River, sisi ni watu wa kuhama hama, wakati tunahama, watoto wanaenda. Shule zinabaki bila watoto, watu tumejenga shule na watoto na wazazi wamehama na wameenda.
Kwa hivyo tungeomba kila division iwe na boarding, tukihama tunawacha watoto pale shule, tuenda kwa malisho yetu.

Ingine: Mimi ninashangaa kusikia tenant katika Kenya. Ardhi ni ya watu Wakenya wote. Ningeomba serikali iondoe hilo jina kwa sababu yule mtu yuko mahali popote Kenya ni Mwanakenya na ardhi ni ya Kenya. Apewe title deed kumiliki hayo mashamba. Mambo ya kuitwa tenant iondolewe katika Kenya mzima.
Kwa hayo machache, ninasema asante.

**Com.Mutakha Kangu:** Abdi Ariche?

**Abdi Ariche:** Bwana Chairman, wananchi, hamjambo?

**Response:** Hatujambo.

**Abdi Ariche:** Jina langu ni Abdi Ariche, ninatoka Bura-Tana. Mimi ninatoa maoni kuhusu mambo ya utawala katika Kenya. Kutoka Kenya ilipopata uhuru, tunaweza kusema Kenya imepata uhuru lakini sisi hatujaona uhuru mpaka wa leo na kwa sababu yake, ukiwauliza wananchi wa Tana River serikali ni nani leo, hawatakueleza serikali ni nani.
Wanajua serikali ni polisi, DC na watu wengine, lakini hawa wananchi wenyewe hawajui haki yao na hawakuekewa, hawawezi wakakuambia serikali ni nani. Kwa upande hiyo tulipata dhuluma nyingi sana katika district ama katika utawala wa Kenya kwa vile sisi hatujasoma na hatuelewi kitu gani kinaendelea. Mpaka saa hii, sisi hapa tunaitwa kwa mambo ya kurekebisha Katiba lakini hiyo Katiba tunaona tukiandika na badala ya kuendesha mbele mwandiko hiyo, itaelekeshwa itasomwa upande wa nyuma kwa vile thuluma ilikuwako wakati wa kimbele.

Ninaomba Tume ya Kurekebisha Katiba, hii Katiba ikiandikwa, ihusishe kila mtu na waelewe ya kuwa hiyo kitu kimewekwa maanane na umuhimu ya hiyo kitu ifikie wananchi wa Kenya.

Nikirudi nyuma kidogo, utakuta mtu anakamatwa na polisi anapelekwa pale ndani, yeye hana makosa, anawekwa siku tano, siku sita, siku saba na baada ya kuwekwa, anawachiliwa. Dhuluma bali si polisi pekee yake, hata utakuta chief anachukua utawala wake, kwa vile kulikuwa na Chief's Act, lakini siku hizi ilitupwa, lakini bado inaendelea katika Tana River bado iko. Unaweza kukuta chief anachukua ----- bila kujua watu ama wazee ama yoyote, anaweza chukua mtu na kumweka ndani ama kutesa watu ama aende district ingine anachukua askari bila DC ama DO ama mtu yeyote kuhusika ananyanyasa wananchi na kuwatawala na kuwaweka ndani na kuwekelea vile anataka maneno. Kitu kama hiyo kimetendeka katika Tana River na iko hata sasa.

**Com. Salim:** Sasa Bwana Abdi, ungependelea nini ifanywe?

**Mr. Ariche:** Ningependelea ma chief, sio masomo, kama vile watu walikuwa wanasema. Zamani kutoka wakati wa wazee wetu, ama mbeleni tulikuwa na ma chief ambao hawa chiefs walikuwa wanarithiana kutoka ujadi, kama wafalme. Wazee hawa ndio nataka iongozwe kwao, chief achaguliwe na wananchi.

Kama inatakikana masomo, assistant chief yake awe amesoma.

**Com. Salim:** Unaonaje habari ya polisi ya kuweka watu jela kwa muda? Hapo una pendekezo gani?

**Mr. Ariche:** Hapo ninapendekeza ya kwamba polisi wasiweke mtu ndani bila sababu. Kwa sababu mtu kama anajua haki yake, angeshtaki serikali, lakini sasa sisi hatuna, hatuwezi tukaishtaki serikali kwa sababu hatujui rights yetu.

**Com. Muthaka Kangu:** Endelea Mzee.

**Mr. Ariche:** Bado ninaendelea na upande wa administration. Utakuta, hii Tana River, tuko handicapped kabisa, hakuna kitu sisi tunaweza kufanya kwa sababu upande wa DCs office, kuna vitu nyingi zinatokea kama ma NGOs wanaleta msaada, kuna pesa ya maendeleo inatengewa katika district ambayo inatakikana wahusishe ma-chief, ma chief wataka kuanzia sub-chief, inatakikana awe na sub-DDC halafu location mpaka kwa division, iende kwa district. Kitu kama hiyo Tana River hakuna kwa sababu chief anachukua amri kutoka kwa DC, DO wa division wakati anaitisha hiyo kitu, yeye anaitisha wale watu anapenda na wanapitisha kitu isiyo na msingi, wanafanya kivyao.

DDC, hata ma area councillor hawaingii. Ni wale wakuu wa serikali na DC na ma DO, wanafanya kivyao. Hata hakuna mzee

mmoja wa area hiyo anaweza kuhusika. Ma councilor hawahusiki, wanaita chairman pekee yake. Kitu kama hiyo ninataka ipotee, hii kitu iwe katika wananchi, pamoja na ma councilor wawe katika DDC. Wazee wa area waitwe, kila area mtu mmoja, na councilor wote wa sehemu hiyo waitwe na wahusishwe katika DDC, ile neno inapitishwa lazima wajue.

**Com. Mutakha Kangu:** Uko na dakika moja, jaribu umalize. Umebakia na dakika moja, endeklea umalize.

**Mr. Ariche:** Okay. Nikiendelea tena, hii sehemu kuna contract nyingi inatoka ya serikali ambayo watu wa area hii wangesaidika, wakipata contract na kuna watu walio na uwezo ya kufanya hiyo contract

**Com. Salim:** Ungetupatia mifano ya contracts ambayo wananchi wangefaidika nayo.

**Mr. Ariche:** Contract zingine ni za kutoka NGOs kama kuchimba ma-dams, kupeana chakula katika national youth service na vitu ingine kama kujenga manyumba ya serikali. Hii kitu kama wangepewa wananchi wa sehemu hiyo, wangefaidika, lakini utakuta kuna mtu mmoja katika ofisi ya DC anaitwa supply officer, mamlaka yote yeye ndiye yuko nayo. Hata kama wewe umetimisha chochote, yeye anaweza kutoa mtu kutoka sehemu ingine mbali sana na ampatie, na wewe hata ukifanya nini uwezi kupata. Utakuta ile utajiri ya nchi hii inaenda sehemu zingine. Hiyo inataka ikatwe, contracts zilitokea,, wapewe wale watu wa sehemu hiyo ili wapate kufaidika.

(Applause)

Cha sita, katika nchi hii yetu, utakuta kuhusiana na hii serikali yetu, kila mpango nasikia inatokana na Executive. Hii Executive, wakati zinapangwa ni ma-minister.

**Com. Salim:** Ungependelea nini?

**Mr. Ariche:** Ningependelea hii kitu, kama kuna mpango ya Kenya nzima, ni lazima itoke kwa grass root, sub-location, hawa watu waondolewe hiyo mamlaka ya kufanya vile wanavyotaka.

**Com. Mutakha Kangu:** Mzee sasa sema la mwisho, masaa yako yamekwisha.
**Mr. Ariche:** La mwisho, sisi Tana River, hapa tuko na area na mlisikia kulikuwa na clashes ambaye zilitoka kati ya Orma na wa Pokomo. Hii clashes, kitu kinasababisha si sisi wenyewe tuluikosana. Hii area tuko nayo ni area moja ambayo iko na rutuba kabisa ambayo kwa wakulima na kwa wafugaji ndiyo nzuri sana lakini sisi kwa vile hatuna elimu, hatuna njia. Utakuta hii area, ziligawanywa sehemu mbili zilipeanwa kwa watu. Wale watu waligawanyiwa, wananchi walikuwa ni wachache sana.

Hizo sehemu zilichukuliwa na watu ambao ni wenye pesa na wanakaa Nairobi, hiyo ardhi yote wamepora. Baadaye wakitaka

kupora ardhi ingine,wakaanza kusema wa Pokomo mchukue panga, mtakatiwa title deed na hao wa Pokomo, tulikuwa tunakubaliana na hao, hakuna mpokomo mmoja atapata zaidi ya ile shamba yake ile alikuwa nayo. Ile ardhi ingeporwa na ingeuzwa kwa watu wengine. Kwa hivyo hiyo kitu inatakikana irudi kwa wananchi, kwa mkono wa wananchi wakae chini, kama ardhi imetolewa, lazima wananchi wahusishwe, wakae chini na waelewe ni kitu gani watafanyia hiyo ardhi yao.

**Com. Mutakha Kangu**: Asante basi.

**Mr. Ariche:** Asante.

**Com. Mutakha Kangu:** Andikisha pale Mzee, andikisha na uweke sahihi. Abdi Soman, observer, Hassan Adomo? Andrew Owino, observer, Barnabas Monari? Basi kuja Mzee.

**Barnabas Monari:** Commissioners wa Katiba na wananchi, hamjambo? Jina langu ni Barnabas Monari. Mimi ni mkulima hapa Bura. Nimekuja hapa mwaka wa eighty two na nikalima miaka sita, kilimo ikaanguka. Sasa hii ndiyo taabu. Ninataka kusema hata tukisema maneno mengi, hayatatufaa kitu kama sisi tutakuwa na wizi, tutakuwa na ufisadi katika maofisi kubwa kubwa, hakuna chochote tunaweza kufanya.

Wakati ule tulikuja hapa kama watu elfu nne, na mabibi na watoto, na sasa tumefikia watu elfu hamsini, karibu sitini, na hakuna kitu yoyote tunafanya, na ile ilisababisha haya mambo yote ni ile ufisadi.
Mimi ninaambia hii kamati ya Katiba, bila ufisadi kwisha katika nchi hii, hakuna chochote kitaweza kwenda mbele.

**Com. Mutakha Kangu:** Na wewe unasema ufisadi, ufisadi umalizwe kwa njia gani, ni yapi maoni yako kuhusu ufisadi?.

**Mr. Monari:** Kumaliza ufisadi? Kama mimi nitapatikana nimefanya hiyo makosa ya ufisadi, nisiachwe, nikamatwe, mali yangu ichukuliwe, na nishtakiwe kotini, nifungwe. Hiyo ndiyo itakuwa njia moja ya kumaliza ufisadi.

Kuendelea na hiyo, ninafikiri miradi mingi katika Kenya, imeangushwa na njia hiyo hiyo ya ufisadi. Je, sasa hata kama mimi nitakuona wewe ukifanya hiyo ufisadi, nitaenda kwa nani? Nikienda kwa serikali, watu wa serikali ndio wenyewe, sasa nitaenda kwa nani? wataniambia hayo tutaangalia, hakuna mambo ile inaweza songa mbele.

**Com. Mutakha Kangu**: Asante. Umemaliza ama bado kuna ingine?

**Mr. Monari:** Nimemaliza, yangu ilikuwa ni hayo.

**Com. Mutakha Kangu:** Asante basi, andikisha pale. Ramadhan Yefe ni observer. Nenda uandikishe pale, Dende Moti,

observer, Ali Watijo Shire, observer, Hussein Jara? Also observer.  Mohammed Aloo?

**Com. Idha Salim:** Tafadhali sema naam au ndiyo.

**Com. Mutakha Kangu:** Ni wewe? Haya! kuja basi.

**Mohammed Aloo:** Mimi ninaitwa Mohammed Aloo.  Kwanza nimeshukuru kwa vile leo tumekutana na members wanaohusika na mambo ya Katiba.  Kwa hii jambo ilikuwa sisi watu wa Tana River, kama mlikuwa huko bara, hatujasikia, ni kuona mwanz0 ndiyo leo.  Nimerudisha shukrani kubwa sana.
Jambo la kwanza ninataka kusema ni mambo ya elimu.  Sisi wakaaji wa Tana River, mbeleni hatujasoma, lakini sasa tumejaribu kidogo kidogo, tunaendelea, lakini tunataka mkazo kwa upande wa serikali kuanzia sub-location mpaka location, chief aweke mkazo kuhusu upande wa elimu. Mtu yeyote ambaye hataki kupeleka mtoto wake shule, apelekwe kotini ashtakiwe.

Jambo la pili ambayo ni muhimu sana katika wilaya ya Tana River, mtu anaitwa DO, ambaye ni civil servant ya serikali, anakuja kukaa division.  Huyu ndiyo atakuwa Chairman kuhusu vitambulisho ambayo hawezi kujua, mtoto yangu wala yako ndiyo wanakuja kusimamia mambo ya kitambulisho.

**Com.?** Unatakaje Mzee?

**Mr. Monari:** Ninataka wenyeji, mzee ama chief, si DO anakuambia mtoto yangu hapana jua, toka kwa ofisi yangu.
Hiyo ndio muhimu, ninataka hiyo sheria iondolewe.

Jambo lingine ya nne, hii mambo ya rent ya kumiliki ardhi.  Huu mto wa Tana River si ya Pokomo pekee yake; wa Orma wako ndani, Malakote wako ndani, Pokomo wako ndani, Korkoro wako ndani, wa Sanya wako ndani.  Wakisema wamiliki  hiyo shamba, muanze kutoka chini ya mto, hizo kabila tano zote, wapate haki zao kutoka mto kwenda mpaka juu.

Jambo la tano, ni vile mwenzangu hapa amesema, kame Abdi Arte aliongea, ni mambo ya sehemu ambayo inatokea tender, kufanya msaada, yaani kwenda kuchimba dam, ama transport ya kubeba mahindi ya World Food Programme.
Tunataka tender kama hiyo ikitoka, isiwe DC wala DO anakaa ofisini anapanga, kuwe na kamati ya wenyeji, wajue hiyo tender nani anapewa.

Jambo la sita: Sisi hapa Tana River, tunasikia kama serikali wanatoa mkopo.  Serikali ikitoa mkopo, hatujui huo mkopo unatioewa na nani.  Kama ni mkopo, kamati ni DC na watu wake, wale watu wa nje kama wakulima na wafugaji, wanasikia wilaya ya Tana River inaingia pesa ya mkopo kiasi fulani, lakini sisi wenyeji hatujui hiyo pesa nani anapewa.  Tunataka hiyo pesa kama hii, serikali ikitenga kutoka Parliament, ipitie wenyeji, wawe kamati, wenyewe, kutoka location mpaka sub-location.

Ile ingine nilikuwa nikitaka kusema imesemwa na watu wengi sana. Tunaomba kitu kimoja, ambayo zaidi ya miaka ishirini tumekuwa hapa Bura, tunasikia hii scheme yetu ya Bura itafufuka itafufuka, hatujui kama itafufuka. Tunataka serikali akishindwa, wapatie wafadhili, si lazima mpaka iwe mkono wa serikali.
Yangu ni hayo machache, asanteni sana kwa kutufundisha mambo ya Katiba, na mkiandika Katiba, muandike maoni ya wananchi vizuri, siyo muende mubadilishe tena baadaye. Asante.

**Com. Mutakha Kangu:** Na Julius Emana? Observer, Isaac Wario, observer, Ismael Kofa, observer, Mohamood Doshua, observer, Mohammed Masedane? Hutaki kuzungumza?

**Mohammed Masedane:** Waheshimiwa, na wakubwa na watoto, hamjambo?

**Audience:** Hatujambo.

**Mr. Masedane:** Mimi nina homa zaidi, koo yangu imekuwa kidogo.

**Com.?:** Pole.

**Mr. Masedane:** Naomba kwa serikali ya Kenya yetu, ikubaliwe majimbo.

Ya pili ninaomba serikali yetu ya Kenya, ikikubaliwa, tunataka president wa Kiislamu

**Com. Idha Salim:** Sijui ni kwa nini jambo kama hili, maoni kama haya inawachekesha wengine? Kila mtu ana haki ya kutoa maoni yake bila ya kuingiliwa. Tafadhalini, kimya tusikize. Endelea Mzee.
**Mr. Masedane:** Ya tatu, naomba kwa serikali, itufanyie msaada kama -----?

**Com. Idha Salim:** Iwafanyie nini?

**Mr. Masedane:** Hayo mambo mawili.

**Com. Idha Salim:** Asante basi.

**Com. Mutakha Kangu:** Weka sahihi pale Mzee. Tupate Gogu Galano. Hayuko? Yuko wapi? Basi kama hayuko, tumsikie Simba Arde. Simba Arde.Wewe ndiwe nani? Gogu Galanu, haya chukua kiti basi.

**Gogu Ghalanu:** Commissioners na wale wamefuatana nanyi na wanyonge wenzangu,
Salaam Aleikum.

**Response:** Aleikum Salaam

**Gogu Ghalanu:** Mimi ninaitwa Gogu Ghalanu Banta, chairman Tana Repo – Tana Natural Resource Management Organization ambayo inaelimisha wananchi jinsi ya kuhifadhi sehemu ya nchi.
Mimi maoni yangu, hii sehemu yetu inaitwa operation area. Sehemu ya operation area hii, maana ya operation area tuliona ni sehemu ambayo wenyewe hawana haki, sababu tuliona jeshi wakija operation, mtu anashikwa, anauawa, anawachwa. Tukiuliza tunaambiwa ni operation area.
Tungependa haya maneno yanayoitwa operation area, serikali iondowe maanake hicho kitu kinatuumiza.

Upande wa askari: Hauwezi kujua huyu ni AP, ama ni polisi ama ni KPR, wote wanavaa jungle, kofia kepi. Hata mtu akikushika akikupiga, akikuwacha, huwezi kujua ni nani kwa sababu ile uzi ambayo inaonyesha huyu ni AP au ni Polisi, wanavalia jungle juu, wakificha ule uzi usionekane ni gani. Tuliona kweli operation area ambao hawana haki. Serikali iondoe hiyo, kila askari awe na namba yake kwa bega ionyeshe ndiyo wale wanajua kusoma hata wakipigwa wajue ni askari fulani ama ni namba fulani.

Ya pili, kitu tungependa, serikali tunaona kama inatuonea sisi wakaaji wa Tana River. Iko hii Bura irrigation, iko Hola irrigation, iko TARDA, wale wanapanda mchele. Hizi schemes tatu zote zimekufa na serikali kwanza ilitumia pesa nyingi sana kujenga hizo scheme na baada ya miaka mitano, hizo scheme zimekufa na tuliona hiyo kwanza ni njia moja ya kuangamizwa, kuitwa operation area.

**Com.?:** Tafadhali toa pendekezo.

**Mr. Ghalamu:** Kitu ningependekeza ni kwamba serikali irudishe hizo schemes maanake hii chakula mnatuombea, kama hii chakula ya msaada, relief. Hicho chakula kina gharama kuliko hizo schemes. Hiyo scheme ifufuliwe ndio wananchi wasiwe wanaombewa chakula, wajisaidie na hiyo rasilmali yao.

Tena, hakuna district mbali kuliko Mandera saa hii. Iko na stima, iko na barabara, wanasikizwa na serikali. District ya kwanza Tana River ni Hola, ni ya kitambo sana, kwa nini hii district haina stima, haina barabara? Tunaona serikali inatuonea, kutuita operation area. Kwa hivyo, tafadhali, serikali ituondolee hiyo, itufanyie sisi kama Wakenya wengine.

**Com. Mutakha Kangu:** Jaribu umalizie.

**Mr. Ghalamu:** Jeshi la Kenya tunaomba, kuliko wapatiwe mshahara na ushuru ya kutoka kwa wananchi, hizi contracts za barabara, wapatiwe. Hizi barabara wajenge hao wenyewe, madaraja na hali kadhalika ndiyo hiyo contract mshahara itakuwa hapo hapo ndani, watakuwa wamefaidi wananchi na serikali pia.

NGOs hawaji hapa Tana River na hawaitambui kwa sababu serikali inawaambia kuwa huko Tana River, kuna Shiftas, mkienda huko mtauwawa na hii, inaweza kuwa makosa ya serikali ya kuumiza nayo wananchi. Kwa hivyo, tungeomba, sisi ni kama wananchi wengine.

North Eastern NGOs wanaenda, wanafanya kazi, na hakuna sehemu mbaya kama North Eastern. Bunduki ikitoka Somalia, yote inapitia North Eastern, hali wenyewe wanahudumiwa, kwa nini sisi wakaaji wa Tana River, NGOs wasituhudumie?

Kwa maoni yangu, NGOs pia wajue upande hii Shiftas hawako, ni serikali inatulalie, itusaidie kama wengine. Aleikum Salaam, Alhamdhulilahi wabarakatuhu.

**Com. Mutakha Kangu:** Simba Arthe? Kuja hapa hivi na tuanze mara moja kwa sababu masaa inaenda.

**Simba Arthe Dhilo:** Kwa jina ni Simba Arthe Dhilow, councillor wa area, Bura location.

Nikianza, langu la kwanza ni kuhusu scheme yetu ya Bura: Ninafikiri hii scheme yetu ya Bura, kuna watu wa Kenya wote hapa, kwa hii scheme ya Bura. Ni scheme ambayo ikipatikana kufufuliwa, inaweza kuwa ya manufaa kwa Wakenya wote, ile chakula inatoka hapa.

**Com. Mitakha Kangu:** Endelea tu. Na tuseme kama ni kurudia yenye wengine wamesema, unaweza sema tu unaunga mwenzako mkono kuhusu mambo ya kurevive scheme.

**Mr. Arthe:** Ndiyo. Ndiyo mimi ninakuja.

**Com. Mutakha Kangu:** Asante.

**Mr. Arthe:** Hii division…

**Com. Idha Salim:** Samahani Bwana Simba, Bwana Mwenyekiti wa kikao anasema, ikiwa unataja jambo ambalo limekwisha tajwa na wenzako mbeleni, jakuna haja ya kuchukua wakati kueleza, tumefahamu. Endelea na kitu kipya. Sema tu irrigation scheme, kama wenzangu walivyoeleza, tungependa i ----

**Com.Mutakha kangu:** Ama ukitaka rekebisha kidogo, unajua ukitaka kurekebisha mahali mwenzako alizungumza, mimi ninakuja kurekebisha mahali mwenzangu alizungumza.

**Com. Idha Salim:** Hiyo ni tofauti…..

**Mr. Arthe:** Sawa. Wale Wakenya wanaishi hapa ni wengi sana na hapa division hii ya Bura, tushapewa na sub-district wakati ingine. Na subdistict tulipewa, hatukuwahi kuona hiyo sub-district. Hakuna DO1 alikuja, bado tuko division tu mpaka sasa. Tunaomba vile ilipitishwa na Mzee, hiyo sub- district yetu tunataka kuiona.

Ya pili ni upande ya elimu, mambo ya KNUT, hii ya kusimamia waalimu. Hichi chama cha KNUT inaangalia haki ya waalimu pekee yake, haiangalii haki ya watoto kuendelea kusoma shuleni. Serikali inatambua haki ya waalimu pekee yake, hawatambui haki ya watoto wale wanasoma, tunaomba serikali, hii chama cha KNUT kama haitambui haki ya wanafunzi, iondolewe pia.

Jambo langu la tatu: Mambo ya NGOs. Mambo ya NGOs inaanzia district huko. Sisi tunaomba wakija kwa msaada hapa, waanze katika sub-location, ile mahali wanataka kuja kufanyia maendeleo, waanze huko chini.

Langu la mwisho ni juu ya ile kitambulisho nyekundu watu wanafungwa nayo kutoka Nairobi. Hii kitambulisho kuna mwenye alitoa, na yeye mwenyewe sasa hayuko kwa hiyo shida, shida imerudi kwetu. Tunataka kama Wanakenya, hii kitambulisho nyekundu ipotee kabisa. Tusiwekewe masharti ya vijana.
Asanteni sana.

**Com. Mutakha Kangu:** Na tupate Abdi Wario? Huyo ni observer, Muso Koto, hayuko, Moses Mugo, observer, Dickson Mwangi? Songa hapa.

**Dickson Mungai :** Hamjambo Bwana Commissioner na wahudumu wako, raia watukufu wa Bura. Kwa majina ninaitwa Dickson Kiragu Mungai..
Sasa kidogo ningependa kugusia Parliament au Bunge, hasa utengenezaji wao wa sheria, na kujipendelea wao pekee.
Mwanzo kwa mishahara yao, wamedunisha mishahara ya hao wengine kama waalimu na madaktari. Unakuta daktari yule aliye na mshahara ya juu sana ni upto sixty thousand, na mwenzake anakanyaga kuanzia eight hundred thousand.
Unakuta shule kama nursery schools, hata mwalimu yule wa kufundisha, senti zake mpaka zikusanywe na wananchi ikiwa kibunda kama kile ni treasury ya raia na kinaondoka hivi hivi. Kwa hivyo pia hiyo ninaonelea afadhali bunge wakae chini wajadiliane, wapunguze hiyo mishahara yao ipate kusaidia miradi mingine kama hiyo nimetaja.

Ya pili ni kwa ofisi wa mkuu wa sheria, Attorney General: Kwa maoni yangu ningeonelea, kuweko na ofisi au koti fulani special imetengewa hasa wale wenye makosa ya kuua kwani wanakaa rumande zaidi ya miezi sita, hawajafunguliwa mashtaka na hawajafikishwa kotini. Wao huwa hawajulikani ni wa nani, ni kufia kule ndani na ugonjwa, pengine ni ya kuhara, kuumwa na kichwa and such, na unakuta mtu sometimes, ni innocent.
Ningependelea, kwa vile pengine ofisi ya Attoney General huwa iko occupied, wafungue ofisi zingine au koti zingine, aidha kwa

district and so on.

Nikiongoka hapo kidogo, ninagusia habari ya chief. Kweli tukifuatilia kusema chief awe akichaguliwa na raia, kwingi tutakuwa tumeingiza ukabila.
Pili, tukisema huyu chifu asiwe na masomo, tumepuuza ile morale ya elimu hasa kwa watoto. Atakuwa akisema babangu ni chief na hakusoma, babangu ni DO na hakusoma, kwa hivyo hata mimi nisiposoma, bado nitapata ile nafasi ya kuchaguliwa kama chief.

**Com. Salim:** Toa pendekezo.

**Mr. Mungai:** Kwa hivyo pendekezo langu ni huyu chief achaguliwe kimasomo. Aende awe ni wa standard eight, ni mtu anajua kusoma na kuandika, hata sub-chief wake awe ni hivyo hivyo.
**Com. Salim:** Kiwango gani cha elimu?

**Mr. Mungai:** Ile ya zamani ni standard seven, kuna wengine wao wako na hizi cheti ya standard seven na kuna wale wa standard eight, kuna wale form four.

**Com. Idha Salim:** Sasa leo, wacha ya zamani.

**Mr. Mungai:** Hata ya zamani, sijakuelewa.

**Com. Idha Salim:** Anasema unataka chiefs wawe wamesoma kiwango gani cha elimu?

**Mr. Mungai:** Kuanzia standard seven mpaka form four.

**Com. Mutakha Kangu:** Haya! Endelea.

**Mr.Mungai:** Nikimalizia, naguzia kidogo kuhusiana na hizi schemes. Hapo awali kuna msemaji alisema serikali inajua kila sehemu, lakini ninasikitika kwa sababu Bura ni kama ilitoka kwa map ya Kenya.
Hasa ukiangalia hospitali, afya ya binadamu hapa ni kama imesahaulika. Unakuta hospitali kama hii yetu hapa hakuna kitanda, hakuna madawa ya kutosha, hakuna gari, kwa hivyo unakuta watu wengi wale wanaishi hapa, kukipatikana outbreak kidogo ya ugonjwa, wanafia hapa hapa dispensary hii.

**Com. Salim:** Pendekezo?
**Mr. Mungai:** Hapo ningependekeza serikali itukumbuke, iturudishie vitanda vyetu vya hospitali, kutuongezea madawa na hasa

ambulance.

Yangu ni hayo tu.

**Com. Mutakha Kangu:** Na Christine Numba, observer, Virginia Wayua, observer, Hassan Godole Oloo? Na wengine waache kelele tumsikise Bwana Oloo.

**Hussein Aloo:** Maofisa wa Katiba, wananchi, Salaam Aleikum?

**Audience:** Aleikum Salaam

**Hussein Aloo:** Mimi nitaongea Kiorma, warudishe kwa Kiswahili.

**Com. Idha Salim:** Unataka kuzungumza Kiorma?

**Hussein Aloo:** Ndiyo. (Orma)

**Translator:** Anasema maneno yake ni machache na saa imesonga.

**Hussein Aloo:** (Orma)

**Translator:** Mbele yake kuna watu wameongea mengi, ataongea mambo mawili.

**Hussein Aloo:** (Orma)

**Translator:** Kuhusu kitambulisho na usalama. Hayo tu.

**Hussein Aloo:** (Orma)

**Translator:** Anasema yeye ni headman. Kijiji chake, wale watoto ambao wamezaliwa hapo wote yeye anawajua, na wazee anawajua, lakini DO na Chief hawana habari na hao watoto, lakini assistant chief anawajua.

**Hussein Aloo:** (Orma)

**Translator:** Kamati wa kitambulisho, wawe ni wazee wa hapo hapo, wakiongozwa na headman ndiyo wawe wanaongoza hiyo kamati.

**Hussein Aloo:** (Orma)

**Translator:** Tunataka watoto wetu wapewe vitambulisho na isiwe vikwazo lazima wapitie DO. Moja ni hiyo**.**

**Hussein Aloo:** (Orma)

***Translator:*** Yale mengine wenzangu wameongea.

***Hussein Aloo:*** (Orma)

***Translator:*** Kuhusu usalama, Tana River kumeingia wageni wengi sana, kutoka district tatu, na vitu vikiharibika, inasemakana ni watu wa Tana River, kila kitu ni watu wa Tana River.

**Hussein Aloo:** (Orma)

***Translator:*** Wanajeshi wanakuja hapa, wanafanya operation, sisi wazee tulishikwa tunaambiwa toeni bunduki, wengine wako hapa.

***Hussein Aloo:*** *(Orma)*

**Translator:** Kwa hivyo sisi tunataka namna hii, kama sisi ni wazee, viongozo wa Tana River, hawa wageni ambao wameingia kwa wilaya hii warudishwe kwao, kila mtu akae mahali ambako wametoka.

**Hussein Aloo:** (Orma)

***Translator:*** Wao ni Wakenya lakini wako na mahali ambapo wamezaliwa, warudi mahali wametoka ili chochote kibaya kikipatikana, tuulizwe saa hiyo kwa sababu tuko pekee yetu.

***Hussein Aloo:*** (Orma)

***Translator:*** Lakini kama tumechanganywa na wengine ambao hatujui wametoka wapi, kukitokea chochote, sisi tusiulizwe.

***Hussein Aloo***: (Orma)

***Translator:*** Amesema yake ni hayo tu.

**Com. Mutakha Khangu:** Asante Mzee. Kithane Godana? Haya! Endelea Mzee.

**Kithane Godana:** Mimi ninaitwa Kothane Godana, mimi nafikiri miaka yangu ni mingi sana, nimeshaona mambo mengi sana lakini naona mimi ninajua, sisi kama watu wa Tana River hatuko ndani ya Kenya.
Mimi ninasema hivi kwa sababu Kenya, kila pahali pake, unaweza kujua maendeleo na mambo yake yote. Hapa Tana River, hakuna mtu anajua maana yake na maneno yake yote.
Hata kama serikali inatoa pesa ya kufanya kazi, inakaa ndani ya benki, mpaka irudishwe bila ya kutumiwa kufanya kazi.

Mwaka wa themanini na moja, Mzungu mmoja alikuja akasema dams kumi mtatengenezewa, mpaka sasa hakuna dam hata moja ilitengenezwa, ninasikia pesa ilirudi.

Nyuma yake tena wakasema kuna dams nne inachimbwa, mpaka saa hii hawajachimba na ninafikiri miezi hii sita ikiisha,

inaweza kurudi tu.

Kwa ajili inakuwa namna hii ni kwa sababu hakuna watu wetu ndani ya kamati ya kujua pesa inatoka wapi na inaingia wapi maana serikali inatuma serikali inakaa hapa, wao wenyewe kitu ingine wanakula na kitu ingine wanarudisha wao wenyewe.

**Com. Mutakha Kangu:** Sasa unataka namna gani?

**Mzee Godana:** Ninataka kamati yetu, kama pesa ya kufanya kazi, sisi wazee tujue na watu wetu wajue namna gani pesa inatumika.

Tena Tana River hii, sisi tunalala midomo mtupu tu, hapana raia kukaa maanake wakati wa vita ya Somali na sisi, ndugu yangu aliuawa, serikali walinipatia bunduki ya kuhonga. Wakati walinipatia mimi------, Wanasema wewe uko na bunduki ingine, hata sasa wanafanya operation hapa.
Walinipiga, wakachimba kaburi, wakasema ingia na sikuwa na hatia. Sasa sisi tunataka kama Kenya namna inavyokaa maanake Kenya mchana na usiku watu wanauana na bado sijasikia mtu anachimbiwa karibu na anawekwa.

Kenya wanauana usiku na mchana, na sisi hapa wanaweza kamata manyatta mzima na kuweka ndani ya cell. Sasa sisi, hapa Tana River, sababu mimi ninasema hatuko ndani ya Kenya, sisi leo, vile mmekuja, sheria mpya, sisi hatakuwa ndani ya sheria ya mbele.

Sheria mpya hii tunataka iingie ndani ya Tana River. Hayo ni maneno yangu.

Ya pili: Sisi hatuna masomo na masomo yetu, yaani unajua, kama wewe ni kiongozi wa kunionyesha pahali mzuri, lazima wewe pia utakuwa mjinga kwa sababu maongozi mazuri hakuna.

Sisi tunataka watoto wale wadogo, wa nursery, mwalimu wao aandikwe na serikali halafu watoto wakianza nursery, mwalimu wao alipwe na serikali.

**Com. Idha Salim:** Na ile school ingine Mzee?

**Mzee Godana:** Ile skuli ingine pia ninataka namna hiyo mpaka darasa la nane.

Watoto wetu tukiwasomesha hapa Tana River, hakuna kazi wanaandikwa. Ndege inakuja hapa, inakaa inarudi tu halafu watu watu wengine wanaandikwa pahali wao wanataka. Hata kama wewe una ujuzi gani, hakuna mtu anawaandika watu wa Tana River.

Ninataka mtu akisoma mpaka form four, serikali impatie kazi maanake hata mimi niligharamika. Kwa ajili hata kama anaanguka kidogo, lazima kuna kitu anajua. Hata mwaka huu sisi tunaona mwalimu mwingine anasoma college na watoto wa form four, -----? Wanashinda wale watu bado kwenda college, sisi tumeshaona.

Maneno yangu, sisi tunataka tuwe kama watu wa Kenya na Kenya mpya kwa sababu sisi hatakuwa kwa Kenya ya mbele.

**Com. Mutakha Kangu:** Asante. Tumesikia. Haya! Idris Ali?

**Idris Ali:** Mimi ninaitwa Idris Ali. Ningependa kusema kuhusu mambo ya elimu, kama Mzee mwenzangu alivyosema, kuanzia nursery hadi standard eight ifanywe bure.

Ya pili ni kuhusu wafanyikazi katika Tana River. Ikiwa kazi yoyote imetokea, iwe mtu wa Tana River ameandikwa.

Ya tatu ni kuhusu mto Tana: Sisi hapa ninafikiri tuko makabila matano, kwa hivyo hayo makabila matano yote wapate title deeds.

Ya nne ni kuhusu kitambulisho: Kitambulisho iwekwe chini ya wazazi, siyo DO au DC, iwe chini ya kamati ya wazee.

Kuhusu upande wa hospitali, ningependa serikali ituhudumie. Hakuna dawa, watu wanagonjeka nyumbani, wanakufa. Tungeomba serikali, upande wa serikali wahudumie wananchi kama ilivyo kuwa zamani.

Kuhusu upande wa irrigation scheme, kukitokea contract yoyote, watu wa Tana river waajiriwe.

Yangu ni hayo tu, asanteni.

**Com. Mutakha Kangu:** Na Moti Kuno, ni observer, Makari Mohammed, pia yeye ni observer, Ali Zangus, ni observer, Halima Kunai?

**Halima Kunai:** Maofisa wa serikali kutoka mbali, mabibi na mabwana, salaam aleikum?

**Audience:** Aleikum Salaam.

**Halima Kunai:** Mimi ninaitwa Halima A. Kunai. Yale ningesema, wenzangu wameongea.

Nitaongea mambo ya kina mama: Sisi wakina mama, Tana River, hatuna haki yoyote. Tukiolewa, mabwana zetu wanatupiga, tukienda haja kubwa ama ndogo, mpaka tuombe ruhusa. Hapo sisi hatuna haki, upande wa kina mama.

Upande wa masomo: Ikiwa mimi na kijana mmoja tumelelewa pamoja, wanasomesha kijana, mimi wananiambia fagia nyumba,

kwa hivyo sina haki.

Jambo lolote likitokea, hatuna shauri, mabwana zetu wakifa, ama mababa zetu, hatuna haki, tuna ----?

Sisi kina mama tunataka haki yetu, Serikali itambue, itupatie haki yetu.

Siku hizi Kenya ni ya kila mtu, mwanamke na mwanamume ni sawa, kwa hivyo tunataka upande wetu wa Tana River District, tuwe sawa na wanaume.

Mambo ya kutahiri: Inasemekana wasichana wetu wasitahiriwe, lakini sisi wakina mama tumesema tutahiri, tunatahiri, lazima tutahiri, hiyo ndiyo mila yetu. Hata kama ni kidogo tutahiri tu kwa maana ni aibu sana kwetu msichana asipotahiri, ni aibu sana.

Hawezi kutembea na marafiki zake, hata wanaume wanatutusi, kwa hivyo tunataka haki yetu.

La tatu: Wengine wakina mama hawana bwana, bwana zao wamekufa, wengine wamekufa na ukimwi, watoto wengi wako nyumbani.

Hatuna mtu wa kutusaidia, kilimo kimekufa. Wakati Wwazungu walikuwa, tulikuwa tukisaidika na kulima lakini wale wamesoma walisema Wazungu waondoke, wakati Wazungu waliondoka, shamba ilikufa.

Kwa hivyo sisi hatuna maendeleo yoyote, hata kama tukijikokota, tunaambiwa hatuna mahali pa kwenda. Tukienda district, mambo yote inatupita kwa maana sisi wakina mama wa Bura division hatuna masomo.

**Com. Idha Salim:** Mama unataka jambo gani kwa wajane na watoto wao ifanywe?

**Halima Kunai:** Tunataka serikali itusaidie kwa upande wa kusoma na ulezi. Serikali itusaidie kwa maana sisi tulikuwa tukitegemea kilimo, sasa hatuna kilimo tena. Serikali itusaidie kwa chochote kile.

Upande wa kusoma, wasitulazimishe kuvaa uniform maana hatuna chochote cha kuwapatia. Watoto wetu wetu wasome bila uniform, hata wakifunga kitambaa ya kienyeji, serikali itukubalie tafadhali. Asante sana.

**Com. Mutakha Kangu:** Asante. Hassan Wario ni observer, B. Murira, observer, Awee H. Shambalo, observer, Mama Harietho, pia yeye ni observer, Khadija Haji Elima, observer, Halako Noor? Hayuko. Rehema Hassan? Haya endelea.

**Rehema Hassan:** Commissioners, nyote mliofika hapa, habari zenu?

Maoni ya kwanza ambao ningelipenda nitoe kwa serikali, ningeliomba serikali kama ingeliweza, ipunguze nguvu za MPs. MPs wamekuwa na nguvu kiasi cha kuwa wao ndio wana-control nchi yote mpaka mwananchi chini shinani.

Kwa sababu sisi tunavyoelewa huku chini, MP tunamchagua kule aende watutee sisi wanyonge ambao hatuna nguvu ya kuingia

katika Parliament lakini tukiwachagua, wakienda kwa Bunge, siku hizi imekuwa wamepata nguvu ya kwenda kujitetea wao na familia zao.

Tunawatuma kule kwa sababu si kila mtu ateenda aende aingie kwa Bunge ajitetee. Unaona wao wanaenda, wanaweka mijadala yao, wacha tuongezwe mishahara kiasi fulani. Kwani kuna mtu fulani huku nyuma analalamika kuwa ananyanyaswa kwa mishahara. Kuliko waulize serikali waone kuwa wale watu wanafanya kazi ngumu, waone hiyo mishahara yao wataitatua namna gani, wanawacha kuzungumzia mishahara ya wale wanyonge, wanatetea mishahara yao, wanaongeza mishahara yao hata mara mia moja zaidi ya wale wengine.

Unapata mtu anapata mshahara sijui laki tatu, wewe subordinate staff pale kwa ofisi ya civil servant, unapata shilingi elfu mbili, na huyu MP na familia yake mtaingia kwa the same supermarket, mnaenda kwa duka sawa, mnaenda kwa soko sawa, ukinunua mfuko wa unga shilingi thelathini, yeye pia atanunua kwa hiyo bei thelathini, hatununui bei tofauti na MPs, tunanunua bei sawa.

**Com. Mutakha Kangu:** Ni kitu gani unataka ifanywe?

**Rehema Hassan:** Ningeliomba namna hii, ikiwa wako na maoni yoyote pengine wanajisikia kujitetea kwa upande wao, warudi nyumbani, shinani, tuje tujadiliane na wao, ndiyo waende wapendekeze maoni yao.
Vile wametuma saa hii Katiba tunajadiliana, hata mambo yao maanake sisi ndio tumewatuma, warudi huku tujadiliane ndio iende tena Bunge ipite.

Usawa katika Bunge kwa upande wa kina mama: Tungeliomba serikali namna hii, unajua wakina mama tuko wanyonge, hatuwezi kupingana na mwanamume hata hivyo, hata kama tunasema tukuwe nguvu sawa, hata tufanye namna gani, hiyo iliumbwa na Mungu, hatuwezi kuwa sawa.
Kwa hivyo tunaomba serikali iwe na ile roho ya huruma pia.
Upande wa usawa bungeni ni namna hii; mwanamke ninaweza kusimama nipingane na huyu mbunge mwanamume, na wako na njia nyingi sana za kutunyanyaza. Ungelipata hata wakati ule kulikuwa na rallies za siasa, unapata wewe umeenda kusimama kuongea kwa rally, wanaume wakianza kukubeba, wengine wanaanza kukuchuna kwa mapaja, wengine wangine wanakutekerenya, mwishowe unaona hata wewe mwenyewe unakuwa discouraged unawacha na huwezi kushindana na yeye.

Kwa hivyo ni obvious anapita yeye, wewe unaanguka. Kwa hivyo tungeliomba namna hii; ikiwa yule mbunge atakaye chaguliwa ni mwanamume, akipita, yule nominated awe mwanamke. Na kukuwe na nominated MP katika kila constituency ndio tukuwe sawa, ili yule akipita mume, mwanamke awe nominated.
Mwanamke akiwa elected, mwanamume akuwe nominated, tuwe sawa Bungeni.

Tatu ni upande wa mishahara ya wafanyikazi: Ningelipenda vile serikali imesema inataka kuangalia mishahara yote iwe sawa, wafanye hivyo na wafanye kwa ukweli. Kwa sababu unapata watchman ameandikwa na hajawahi enda shuleni hata siku moja, ameandikwa tu aende akachunge pahali na kwa vile yeye ni wa parastatal, anapata mshahara mara thelathini ya kwangu na mimi pengine nimesoma nimefika pengine form six, ni graduate na yule ambaye hajasoma anakula mshahara zaidi yangu.
Kwa hivyo mishahara yote ifanywe sawa, kusikuwe na mshahara wa parastatal, kukuwe mshahara wa askari, wa nini, wa nini, yote iangaliwe sawa.

Upande mwingine ni vijana: Vijana wanapenda sana kuchezea wasichana wa watu; unapata kijana anaweza kupatia msichana wa mwingine mimba, na asimuoe, yeye anaendelea na elimu, mimi wangu nimeletewa nyumbani, namlea na mjukuu pamoja.
Ningependa serikali iweke sheria na sheria yenye nguvu zaidi kuhusu vijana watakao weka msichana yoyote mimba. Laiti atakubali amuoe na akae naye miezi kadhaa na amuache, maanake wako na hiyo tabia, anakubali siku ile, for the sake ya siku hiyo. Anakubali anaoa msichana, anaenda anakaa na yeye, baada ya miezi sita anamrudisha kwa mamake ati ako na tabia mbaya. Msichana hakuwa na tabia mbaya siku ile wakitongozana lakini atakapozaa, akimchukua, huwa ana tabia mbaya, anaturudishia. Kwa hivyo atakaporudisha msichana, iwe ni sheria kuwa ataangalia huyo msichana na mtoto mpaka mtoto afike umri wa miaka kumi na nane, ule umri wa kuolewa.
Amsomeshe, amvishe.

Nyengine ni kuongezea tu kwa upande wa urithi wa wakina mama: Unajua wakina mama pia tumeonewa sana. Mimi ninaweza kuwa nimeolewa, nikaishi na bwana kwenye nyumba, tumenunua na bwanangu kijiko, nimenunua gari, nimenunua TV nimeweka, tumetafuta na yule bwana; siku ile bwana anapokufa, una pata watu wa bwana wanakuja, kila kitu wanabeba, inakuwa sasa ni cha kijana wao ndiye ametafuta, wanasahau tulitafuta na kijana wao.
Kwa hivyo ningelipenda au ningeliomba kuwekwe sheria ya kuwa ikiwa bwana amekufa, yale mali ambayo tumetafuta na bwana wangu, yawe ni yangu na watoto wangu kwa sababu tumetafuta na bwana na tumewatafutia hao watoto, juu mashemeji wakichukua ujue inaenda kufaidi watoto wao, vile anaangalia watoto wake, hataangalia watoto wangu.

Na serikali pia ningelipenda kitu kimoja, kwa upande wa Tana River: Unajua hatujaona uhuru sisi, bado, sisi hatuna uhuru kabisa. Sisi ndio ni wananchi, lakini uhuru, vile mwenzetu alizungumza mwanzo hatujauona kwa sababu serikali inapokaa kwa Bunge, huwa inapanga budget ya serikali nchi nzima na naami kuwa wanapanga kila district ina pesa kiasi fulani wanatakikana wahitaji, kila province, kitu kama namna hiyo. Na sisi tunashangaa, wanapopangia upande wa transport, pengine mabarabara, kurekebisha lami kule sijui Nyarchonyo, sijui wapi huko Kisumu, ehe, wanasahau kuwa Tana River bado lami tangu uhuru upatikane, hatuna lami, hata watoto wetu wana-fail mashuleni kwa sababu ya barabara mbaya. Unapata hata wengine wanataka kukosa mtihani; mtu ame-book mtihani Garsen lakini hawezi akafika kwa mtihani kwa sababu kwao ni Bura, na barabara ni mbaya.
Kwa hivyo serikali ipange uhaki sawa nchini kwa kila mtu ili kila district inje matunda ya uhuru. Kwa hivyo iangalie, ikiwa Tana River haijahudumiwa kwa upande wa barabara, iweke. Ni kitu gani Tana River inakosa? Haina lami? Ndiyo waweke lami, vile

wanapanga mambo ya kuweka lami kule Nyalgunga, wapangie pia Tana River, zile sehemu kwa hivyo zipangiwe sawa sawa.

Tunashangaa tumeonewa sana sana. Unapata hata district mpya imeanza juzi, iko na miezi chache, haijafika hata miaka, siwezi sema ni mwaka, tayari wameletewa watu wa KenGen, wamewekewa stima, sisi mpaka saa hii Tana River tunawakisha koroboi, ehe, na mnatarajia watoto wetu wasome. Watoto wakianguka mitihani, wanasema wale watu wako nyuma, watoto wao hawasomi. But hatuna uhaki sawa, hatujaonja matunda ya uhuru nchini.

Kwa hivyo tunaomba serikali tafadhali, ikiweka sheria Bungeni, ipitishe ya kuwa ikiwa wanapanga mipango ya mwaka ya nchini, wapangie kila district sawa sawa.

**Com. Mutakha Kangu:** Haya! Jaribu kumaliza.

**Rehema Hussein:** Pia ninaomba serikali ipange siku maalum ya Bunge. Kwa sababu tunachagua wabunge na wanapotelea Nairobi, wakisema ati wako Bunge kwa sababu inaanza Monday to Friday. Kwa hivyo wanakaa tu Nairobi, kwa hivyo kuanzia ile siku tumemchagua akasema ametangaza kwa hall pale ameenda Nairobi, anakuwa yeye ana-attend tu Bunge. Kwa hivyo hapati kurudi huku nyumbani, ajue matatizo yetu ndiyo ayapeleke Bunge. Anakaa tu Nairobi, so long as yeye anakunywa soda baridi na ma ice cream, anatusahau sisi huku.
Kwa hivyo wapangiwe siku maalum, hata kama ingeliwezekana iwekwe kuwa pengine wanaweza kuwa hata mara moja kwa wiki ili ule muda mwingi wawe nyumbani, wapate kuchukua shida zetu wakipeleka Bunge.

Mambo ya contract imeshazungumziwa. Kwa hivyo ninaunga mkono ya kuwa tender ikitokezea, ipatiwe mwenyeji na tenders maofisini ninaomba itolewe. Katika sheria ya Kenya, hizi ma tender za maofisi ati huyu ndiye atanunua ruler, huyu ndiye atanunua nini, hiyo ndiyo imeleta ufisadi maofisini na hiyo ndiyo imeangusha projects nyingi sana hata ukisema pengine hii scheme ya Bura inaweza kuwa imeangushwa na hiyo mambo ya tenders hizo, maanake huwa hawafanyi haki.
Kwa hivyo hii mambo ya tender board, hii tender board tunaomba itolewe kwa maofisi, watafute njia ingine ile ambayo ni ya kusaidia, ambayo itasaidia maofisi.

Land demarcation, hii mambo ya ugawaji wa ardhi: Ninaomba srikali ikiwa inataka kugawanya ardhi, isiingilie watu ghafla. Unajua kama hii issue ya clashes ya Tana River, zimeletwa kwa sababu serikali imeleta hilo jambo ghafla kwetu; wamekuja kusema tunakuja kugawanya ardhi lakini bado hawajaelimisha huyu mwenyeji kuwa ugawaji wa ardhi ni nini na nini madhara yake na nini faida yake.
Kwa hivyo ikiwa ugawaji wa ardhi wowote utafanyika, kuwe na elimu, yaani watu wawe educated, waje wasomeshe mwenyeji kuwa ardhi itagawanywa namna hii, haya ndiyo madhara yake, hii ndiyo faida yake, kwa hivyo kama ugawaji wa ardhi unafanyika, mwenyeji ahusishwe na kuhusishwa kwa mwenyeji ni kuelimishwa ili apate kuelewa.Asanteni.

**Com. Mutakha Kangu:** Asante. Weka sahihi. Khadija Godana, huyu ni observer, tupate Zainabu Hassan, observer, Musa Ijira, observer, Khadija Kasim is also an observer, Solomon Lunani? Endelea tu.

**Solomon Lunani:** Kwa jina mimi ninaitwa Solomon Lunani, lingine ni Shikamai. Mimi nimeshukuru kwa vile mmetusikia.

Neno langu la kwanza ni: Ninaonelea muda wa Katiba uongezwe, watu wasije wakaleta ukatili, yaani kuna tabia ingine ya kufanyia wengine kinyume, kuangusha Kenya.

Nina sababu ya kusema hivyo kwa maana mwaka wa 1982, walisema baada ya election, tutakamilisha Katiba lakini wakati walifika kwa election, ikapita, hiyo Katiba waliisahau kabisa, ikaenda hivyo. 1997 tena, ilifika hii Katiba iendelee, wakasema wacha tufanye election kwanza, wakabembeleza raia, wakati walibembeza raia, election ikafanyika, ilienda tena tena tena mpaka, tena hiyo inataka kufanyika mwaka huu.

Sisi tunaonelea Katiba ikamilishwe ndiyo election ifanywe.

Point ya pili nitazungumza kwa upande wa uraia wa Mwanakenya: Utakuta ya kwamba kama hapa Bura tuko makabila arobaini na mbili na labda mimi nimekuja na ndugu yangu, ama mtu yeyote ametoka huko Somali ama Mandera ama huko Western, ama Kwale ama Kisii, amekuja amekaa na mimi, ambaye nimekaa hapa kwa miaka ishirini, amekaa na mimi kwa miaka kumi na tano ama miaka sita, ama kumi, amesahau huko, sasa huyo ana haki ya kuwa raia wa hapa kwa maana hata mahali ametoka amesahau hata akienda huko hakuna.

Ana haki ya kukaa hapa, apewe makao hapa na na awe raia wa hapa. Kwa maana utakuta, tuseme tuko na Mborana ambaye ametoka Moyale huko na huyu mtoto labda wazazi wake walikufa huko, na amefuata mwenzake, ama binamu, ama babake mdogo, ama shangazi na amekuja amekaa na yeye, tuseme Kipini ama amekaa na yeye Mombasa, ama amekaa na yeye Garsen kwa miaka sita, saba, huyo mimi ninaona kumkataza uraia itakuwa ni mbaya sana, huyo awe raia.

Tatu: Nitazungumza juu ya polisi; kusema kweli, ufisadi Kenya, mtu ambaye ameleta ni polisi. Polisi wamekuwa ni kama wezi, na yeye si mwizi wa kwenda kubomoa ama kulazimisha, polisi anakuiba kwa kupenda kwa mama utakuta mama ametoka hapa, huyu mama labda ni msichana ama ni mwanamke, labda amararuka nguo na ana shida, akienda kwa polisi ana shida yake atatuliwe, badala ya hiyo utakuta inspector ako very smart, anamuomba eti leta kitu kidogo mama ndiyo nikufanyie hivi, na huyu mama asipompa hiyo kitu kidogo, hatatimiziwa.

Sasa hii mambo ya kutoa hii kitu kidogo, mimi ninaona sheria iwekwe kali sana kwa hao polisi. Polisi yeyote akipatikana na kisa yoyote ya kitu kidogo, huyo afutwe mara moja. Iandikwe iwe sheria.

Ukienda kwa upande wa traffic, polisi tena, hao si ati wameenda kwa barabara kuangalia makosa iliyoko barabarani. Hao wameenda kuokota pesa, kusanyasanya pesa, kwa maana kila motokaa shilingi mia moja, kila motokaa shilingi mia moja, mia moja. Hao traffic wanapoteza tu wakati wao kwenda barabarani, hakuna kitu wanafanya.

Mtu akija na magendo ama amebeba bunduki, land rover imejaa, wanaenda kando, kama mko wanaenda kando wanasema "kuna chai kidogo", hiyo bunduki inaenda, hiyo silaha inaenda.

Hata mtu akiua, akienda polisi na atasema kweli nimeuwa lakini Bwana Ofisa, iko kitu kidogo na atatoka. Sasa kwa polisi inatakikana sheria kali iwekwe, he is the one who has allowed corruption in Kenya.

Nitagusia elimu hata ingawa wenzangu wamegusia: Wajua this is an arid area, sasa hawa shifting, shifting, kuokoa hawa watoto wa Tana River, ni all primary schools should be boarding schools, vile wenzangu wamesema. That should be from nursery to form four, ikiwezekana.

Na nitagusia on the side of parastatal bodies in Kenya: I am going to speak entirely all over Kenya; Parastatal bodies in Kenya should be run by the indigenous; ninamaanisha hii projects kama ya Bura hii, Bura irrigation scheme. Hii Bura iendeshwe na wakulima wenyewe.

Wakulima waunde chama chao, wawe na viongozi, waitishe misaada, wafungue accounts zao, waendeshe schemes zao, tuwachane na hao wezi, wakina ofisa na wengine, hawa ni professional thieves.

(Laughter)

Pesa zikitoka huko nje, hizo zinaenda, huo mradi unaanguka, ndiyo unaona all parastatal bodies in Kenya have failed.

Another point is on the side of factories all over Kenya: Ukienda katika factories, nyingi wananyanyasa sana, ziko na sheria za kikoloni na wakati ule wakoloni wale Wazungu ama wale Wahindi walikuwa wanaunda sheria favouring them, za kunyanyaza mfanyikazi.

Utakuta ya kwamba mfanyikazi amefanya kwa factory kama textile kwa miaka ishirini lakini kosa likitokea kidogo, huyu mfanyikazi anafutwa bila ridhaa.

**Com. Idha Salim:** Ungependelea nini?

**Mr.Lunani:** Ningependelea sheria za factories ziundwe na serikali.

**Com. Idha Salim:** Ili?

**Mr. Lunani:** Ili wafanyikazi wanufaike.

**Com. Mutakha Kangu:** Masaa zinaenda.

**Mr. Lunani:** La saba: Ningeomba sijui nifanye nini ama..ninyi ndio wataalam na tume shukuru sana. Wajua, mimi nikikosea serikali, wanakuja wananishika na wananifunga na serikali ikinikosea? Ninashindwa.

(Laughter)

Inatakikana kifungu ipatikane, ya kushtaki hii serikali kwa maana haswa hapa, mkulima wa Bura aliletwa na ako kwa kifungo, serikali imemkosea, akiamuka ni taabu, akitembea jua linamchoma ni taabu, akilala ni taabu, hata kuna mazao yake alikuwa anatoa, yote serikali inameza. Na kwa maana hakuna sheria ya kushtaki sheria, huyu mkulima anakuwa kwa cell tu na mambo yake. Hata wengine wamekufa hapa kutokana na njaa, watoto wameshikwa na Kwashiokor na ni serikali ndiyo ina-cause hii. Sasa tumeshindwa. Kifungu ipatikane ya kushtaki, ikiwa kosa imepatikana kwa serikali, washtakiwe.

Ingawaje kidogo hii…Sheria ya tohara: Sheria ya tohara, mwenzangu mama alizungumza hapa juu ya kutahiri wanawake. Mimi kidogo nilifundishwa, nilielimika kwa upande wa wanawake, vile mwanamke hawezi akazaa, nini, tukaendako seminar, ninajua. Tafadhali, wasichana ninaonelea wasitahiriwe, na nina sababu. Ukitahiri msichana, wajua kama mbuzi, unaona mpira hii, wakati wanaweka pumzi, hii mpira ina-expand.

(Laughter)

Na hii mpira, kama hakuna pumzi inakuja pamoja. Sasa wakati huyu mama anataka kuzaa, huwa hawa wamekata hii mpira yote, sasa haiwezi ika-expand mtoto akatoka, sasa inalazimisha huyu msichana kitu ya kwanza apate mama mwingine, aende achukue, ikiwa ni kisu, ikiwa ni wembe, aende apasue, ndiyo huyo mtoto atoke. Sasa kwa hawa wamama ni taabu sana.
Ikiwa atazaa watoto kumi, lazima aende na kisu. Ikiwa atazaa watoto kumi na nane, aende na kisu, kila mtoto kisu, ni mbaya sana. Na wale ambao hawatahiriwi, mto hata anaweza akaja wakati mama yuko kwa mtoni, ama akafika ameenda hospitali ametoka huko, ama anaokota kuni, mama anazaa tu kwa maana hiyo mpira iko, wakati mtoto anafika, hiyo mpira inapanuka halafu mtoto anatoka, hawezi akahitaji kisu.

**Com. Mutakha Kangu:** Ya mwisho sasa, masaa yako imekwisha.

**Mr. Lunali:** Salaries ya MPs wamezugumza, na mimi nitarudia: Salaries ya MPs iwe scaled kama wafanyikazi wengine wa serikali.
Na la mwisho, President wa Kenya, mnisikilize vizuri, President wa Kenya akiwa ni mwanamume, mimi ninaonelea mwanamke awe vice President.

(Applause)

**Com. Mutakha Kangu:** Weka sahihi pale na yule anafuata ni Mahmud Barak, huyo ni observer, Abdul Rahaman Mohammed is also an observer, Roberto Carlos, observer, Oliver M.C. observer, Emmy Dan, observer na Yusuf Mohammed?

**Yusuf Mohammed:** Ya kwanza nawasalimia Commissioners na wananchi wenzangu, mimi ni Mwenyekiti wa Pastoralists Education Fund.
Jambo ambalo ningeeleza Commission ya kwanza, ingawa imezungumziwa, lakini ni mzuri pia kupitia.
Katika wilaya ya Tana River tuko na shida moja, ya kwanza ni kitambulisho. Mzozo wa kitambulisho imeendelea kwa muda mrefu, tangu ukoloni mpaka leo na hio imethibitishwa na viongozi duni. Ningependelea ya kwamba iwekwe kwa Katiba, hiyo ipelekwe kwa vijiji, kamati ambayo huwa inakaa kwa vijiji, wapewe uwezo wa kupeana vitambulisho badala ya kupatiana kwa watu ambao huwa hawajui mahali kitu inaanzia na inaishia.

Ya pili ni ile kadi nyekundu ya mwaka wa 1989, hiyo pia mimi ningesema ni haramu kiwa sababu ile kitu iliyoko ilikuwa ni ya mtu binafsi, yule councillor Simba Arthe amesema.

**Com. Salim:** Rudia tena hapo?

**Yusuf Mohammed:** Kuna hii screening, card, hii kadi nyekundu,ya 1989, ilikuwa ni ya mtu binafsi.

**Com. Salim:** Endelea.

**Yusuf Mohammed:** Ile kitu iliyoko, ningependa sana ifutiliwe mbali. Kama sisi ni watu wafugaji ama wa kuhamahama ama wakulima, kwa jumla, ya kwamba screening card isitajwe na itupiliwe mbali, isiwekwe kwa kitambulisho.

Mambo ya ardhi: Kwa mfano tuko na Kora game reserve; inaonekana inathaminiwa maisha ya wanyama kuliko ya watu na tungependa sana ya kwamba wananchi wawekwe mbele, badala ya wanyama kuwekwa mbele kwa sababu sehemu hiyo ni kubwa sana, kama Kora game reserve na watu wa kuhamahama huwa wanauawa, wanapigwa na serikali kila wakati, hawana haki.
Ningependa sana iwekwe kwa sheria, badala ya maisha ya wanyama kuthaminiwa, binadamu wathaminiwe, ingawaje wanyama pia wako na haki yao.

Ya tatu: Kuna hii bwawa inajengwa ambalo inaitwa Tana-Athi. Hiyo imeleta shida nyingi sana, mzozo sana kwa wakaaji kama wa Tana River. Ningependa sana hiyo ujenzi isimamishwe na serikali na itafute mbinu ingine kwa sababu hii mto hakuna kitu inatusaidia sisi vile tunaona, tunakaa karibu tu nayo. Shida yenyewe sasa ni kupata maji na tuko karibu, hata aifiki kilomita tatu. Sasa tunaona ya kwamba pia serikali inatuonea.

Ningependa kusema ya kwamba kama sisi Waislamu, tumekubaliwa kuowa wanawake wanne na sitaki iwekwe kwa sheria ya kwamba mwanamume kama ni Muislamu aoe mwanamke mmoja, no, kama sheria, vile tumeambiwa ya kwamba tunaoa

wanawake nne, tunataka ipitishe nai iwe hivyo.

Ingine ni kusema wanawake na wanaume wako sawa. Hiyo ninawaambia ya kwamba mtu pia amekosea Mungu; hawako sawa. Mwanamke ni mwanamke na mwanamume ni mwanamume na ningependa kwamba, kulingana na sheria ama dini ya kiislamu, ya kwamba kati mwanamke na mwanamume kuna tofauti kubwa na hawako sawa. Hiyo ningependa kujulisha kila mtu ya kwamba iwekwe kwa sheria, ijulikane ya kwamba ijulikane ya kwamba wanaume wako juu ya wanawake na ni vizuri wafuate ama watii sheria lakini si ati haki yao inadhulumu haki ya wanawake.

Kuna kutoa mimba kwa wanawake, sana sana kama tuseme huko sehemu za wafugaji, ambao watu hawajui pengine mambo ya hospitali. Ningependa Tume ihakikishe, ipeleke hilo ombi letu na iwekwe sheria, wale ambao huwa wanatoa mimba, kudhulumu wale wako tumboni, wauwawe. Hawa wanawake wauwawe, wasiishi, wauwawe. Kama wanauwa yule mtoto aliye tumboni, pia wao wauwawe, iwe sheria, ipitishwe, ndiyo waache.

Kuna kutahiri: Kutahiri, nikizungumza kwa ukweli, sheria ya Kiislamu imekubali na hakuna mtu anaweza kupinga kulingana na dini. Ningependa kueleza Tume ya kwamba hiyo kwetu hatuwezi kuacha milele na maisha na iwekwe kwa Katiba ya kwamba sisi Waislamu tutatahirisha wasichana wetu na wavulana kwa jumla.

Mashirika isiyokuwa ya kiserikali ambayo huwa wanazuru wilaya ya Tana River ni mashirika yasiyo eleweka kabisa. Ni mashirika ya siasa, ambao wanatoka huko kwao, hakuna uzaidizi wanatupatia, tungependa hizo mashirika, kuna councillor alizungumza hapa, nitapitia, yachujwe kutoka juu na kama wanataka kutoa usaidizi, watoe uzaidisi huko mashinani, kwa vijiji na waende watoe usaidizi wao na watu waone.
Sasa hivi ninapozungumza, kuna zaidi ya mashirika kumi katika wilaya ya Tana River na hakuna usaidizi wanatoa, hatujui ni kazi gani wanafanya. Mashirika kama haya, tungependa kama sisi wafugaji, yatolewe kabisa. Hakuna usaidizi wanatupatia, ni shida wanatuletea.

Mambo ya afya ama mazingira: Watu wa kuhamahama wamedhulumiwa na serikali, sijui serikali inataka nini. Unaweza kutembea kilomita kumi na upate watu population yao pengine ni watu kama elfu tatu, elfu nne na hakuna hata hospitali, watoto huko wanaumia, wamama, kama ni kujifungua, kama ni malaria, tunakimbilia kiliomita mia moja ama mia moja na hamsini. Je, hatuna serikali? Hatuna haki?

Wilaya ya Tana River imekuwa ni moja ya wilaya ambayo kuna mzozo wa kikabila. Ningependa kufahamisha Tume ya kwamba sisi kama wale ambao huwa wamekalishwa ofisi hiyo na Tume, hawakukuwa wamefanya vile Tume iliwaambia kwa sababu tulikuwa tunataka waende watembelee mashambani, kama mimi ninakaa reserve. Hadija na Fatuma wanakaa huko, wangetoa maoni yao, kueleza vile Katiba ingefanywa. Je, kama ninaambiwa ya kwamba Halima na Fatuma hawajui kuandika, kwa sababu wanakaa huko msituni, wao ni watu wa kuhamahama. Je kwani nini kama Halima yule ambaye yuko town

anapewa haki yake ya kutoa maoni yake juu ya Katiba, kwani sisi wote sio binadamu? Sisi zote tuko sawa, haki yetu ni moja. Ningependa ya kwamb watu hawa ambao huwa Tume imewalete waende kila mahali, hawajafanya kazi yao na ningeeleza Tume ya kwamba hata ile kuchaguliwa kwao ilikuwa ni kisiasa walichaguliwa, si matakwa ya raia.

Ingawaje Tana River ni mahali pa mzozo, mali za watu huwa haidhaminiwi kabisa. Kuna kuchoma manyumba ambayo thamani yao ni nyingi, pia kuna kuua mifugo kama ng'ombe, mbuzi, ngamia, punda na kadhalika. Ningependa kueleza Tume ya kwamba wanyama hao wako na haki. Kama mtu akikata ng'ombe ama punda kwa sababu hajui kuzungumza au kusema, pia hata yeye mwenyewe akatwe katwe, vile amekatakata. Iwekwe kwa katiba iwe sheria.

**Com. Mutakha Kangu:** Jaribu umalize, masaa yako yameisha.

**Yusuf Mohammed:** Elimu ni chanzo moja ambayo hata sisi wote imetujumuisha mahali ambako hata saa hii tumekaa, bila elimu hatungefanya mkutano hapa sasa hivi. Serikali ya sasa imewadhulumu wafugaji wetu wa kuhamahama. Sehemu zingine inawapatia haki yao lakini wilaya ya Tana River imepuuzwa. Watu wa kuhamahama hawapewi elimu na serikali, hawapewi walimu wa kuwasomesha, watu wa kuhamahama hawapewi vitabu, hawapewi madawati. Na pia hakuna kitu ingine wanaweza kusaidiwa juu ya kuelimishwa kwa sababu safari hii unajua kuna ugonjwa hatari wa ukimwi, utaendaje kwenda kuelimisha mtu ambaye huwa hajui kusoma ha kuandika? Itakuwa ni vigumu.

Je, kama Halima na Fatuma wako msituni, pia hata wao wako na haki yao ya kupata elimu, si ati ninapeleka Mohammed na Abdi shule. Ningependa iwekwe kwa Katiba.

Tume ninawaeleza ya kwamba iwe sheria ya kwamba kuna wale wamama ambao huwa haki yao imedhulumiwa, hasa watu wa kuhamahama; mama anachota maji kilomita kumi, siku tatu, siku nne, huko msichana atanajisiwa, huko anabebeshwa mzigo usio wake. Je, huyo mtoto na mama hawana haki?
Ningependa Katiba iwekwe, wafugaji, watu wa kuhamahama, watoto na wamama, wapewe haki yao. Nimesema asante.

**Com. Mutakha Kangu:** Ibrahim Danesh ni observer, Maulid Guyo.

**Maulid Guyo:** Mimi kwa jina ninaitwa Maulidi Guyo. Maoni yangu ni hivi: Ningependa hapa nchini Kenya, kuna Waislamu na Wakristo, na ningependa Waislamu wapatiwe nafasi ya kuhukumiwa kwa sheria zao.
Koti ya Waislamu iwe koti huru ya kuendesha haki ya Waislamu.

Cha pili: Kama maofisa wa utawala, kama DO, DC, ma-chief, wengine ni watu wanakuja transfer, wanahudumia hiyo sehemu. Lazima ashirikiane na wananchi lakini huyu mtu hashirikiani na wananchi na anawanyanyasa vile anataka.
Kwa maoni yangu, ningependa aweke kamati ya wananchi, kama yeye haendi vizuri, huyo mtu aondolewe huko, kama DC na

DO.

**Com. Salim:** Ukisema washirikiane na wananchi, maanake ni wafanye nini na wananchi?

**Mr. Guyo:** Lazima hawa watu washirikiane na wananchi, kama huyo mtu utaratibu wake ni mbaya, wamwondoe. Hana haja ya kukaa kunyanyasa wananchi.

Chiefs: Ma chief ni kama wanakuwa ----? ya wananchi, hakuna sheria ya kumwondoa. Kwa maoni yangu ningependa ma-chief, baada ya miaka tano, wapigiwe kura, wachaguliwe kwa kura.

Ningependa sisi raia wa Kenya, kila mahali inaonekana wamepatiwa haki yao, lakini sisi wafugaji tumekosa haki yetu. Samaki inatafutiwa soko nje na sisi wafugaji tungependa vile samaki inatafutiwa soko, watutafutie soko ya ng'ombe nje.

Ya mwisho kabisa ni mambo ya tender: Tender, kuhusu kuajiriwa kazi, lazima kuweko na kamati ya wananchi kwa district, division, location and sub-location. Lazima ishughulikie vile tender inatolewa, vile hii kazi inaandikwa, si eti mtu analetwa kutoka mahali ingine, yeye tu anasimamia kazi yake, anafanya vile yeye anataka. Lazima wananchi washughulike wao wenyewe. Asante, mimi ninakoma hapo.

**Com. Mutakha Kangu:** Osman Algi ni observer, Ibrahim Roga, observer, Ibrahim Omari, pia yeye observer, Noor Dara, observer, Salim Jilo, observer, tupate Abdalla Deko, hayuko, Koro Auchi.

**Koro Auchi:** Asante. Kwanza kupata nafasi hii…

**Com. Mutakha Kangu:** Taja Jina.

**Koro Auchi:** Mimi ninaitwa Koro Auchi. Mimi nimefurahia sana katiba ya nchi kuletewa sisi wanachi wenyewe, ni furaha yangu. Kutoka tulinyakuwa uhuru, tulikuwa tunatumia Katiba ya ukoloni na sasa ni asante.

Mimi mambo ya kwanza ni juu ya tenant: Tenant ni mtu asiye na nchi. Tunataka hii jina tenant iondolewe kabisa kwa sababu tulipata uhuru.

Ya pili, ardhi ya nchi iwe inatolewa na kipimo kwa sababu ardhi haizaliwi lakini sisi tunazaa na sisi tukinyakua mbele, watoto watapata shida. Ardhi iwe na kipimo ndiyo wale watoto wa nyuma wawe wana haki yao kwa taifa hii.

Kuhusu sisi wazee, kulingana na dawa yetu ya Afrika, sisi tunaweza kuoa na tulee watoto mpaka wakati wanapata kazi. Saa

hiyo mama anakataa kabisa sababu anajua wamefanya kazi na saa hiyo wanatengana na watoto wake, wewe mzee unabaki unakaa hapo pekee yako.
Ninataka serikali iangalie haki sawa ya mama na ya mzee.

Hali ya kilimo yetu kama ya scheme inategemea maji; tunataka iangaliwe, hii Tana, kuliko imwage maji baharini, wafunge maji ielekee pande zote za Tana River ndio wananchi wapate kufaidika.
Na yangu ninafikiri wengi wako nyuma, huwezi kumaliza, ni asante kwa sababu mlitufikia wakati huu.

**Com. Mutakha Kangu:** Tupate Kassim Mtagani.

**Kassim Mtagani:** Mimi kwa jina ni Kassim Mtagani Kunno.
Maoni yangu ya kwanza ni kuhusu wafugaji: Wafugaji hawana haki hapa Kenya kwa sababu kuna nchi zingine wafugaji wana haki kwa sababu ng'ombe zao zinahifadhiwa, wanajengewa viwanda ya nyama, ya kutengeneza ile vipuli, ile pembe ya ngo'mbe kwa sababu ng'ombe ina faida mingi sana za zile faida sisi hatufikii na hapa Tana River wengi wetu ni wafugaji lakini ile ng'ombe zetu, hakuna ile faida tuko nayo. Soko ya maana hatuna, kitu ya kwanza, kwa sababu matajiri kutoka mbali hatuna.

Ya pili, ile ng'ombe, ile faida yake, nyama, hakuna viwanda ya nyama. Katika Kenya, hapa Coast province, kulikuwa na Kenya Meat Commission, ile kiwanda ya KMC imekufa na haijafunguliwa mpaka saa hii na ni zaidi ya miaka ishirini.
Ndiyo unaona wafugaji katika Tana River wamerudi chini sana kwa sababu mwaka wa sabini na sita, Tana River County Council ilikuwa council tajiri katika Kenya na leo, kitambo ile kiwanda imekufa, haina faida yoyote.
Sasa sisi, kama Katiba hii mpya, tunataka wafugaji wahifadhiwe sana, tujengewe viwanda ya ng'ombe, hiyo ni kitu ya kwanza.

Ya pili: Serikali iwahifadhi wananchi kwa kutekeleza haki. Kwa sababu uhuru ilipopatikana, ilisemekana mwananchi ni mpaka apate elimu, apate afya bora na apate malisho, kwa upande ya chakula. Sisi hapa Tana River, hizo tatu zote serikali imetupuuza sana, hakuna kitu tumepata.

Elimu, hakuna elimu sisi tuko nayo kulingana na Kenya kwa sababu kwa vile tuko wafugaji, kama serikali ni serikali ya haki, na imesema mwananchi yeyote wa Kenya apate haki yake ya elimu, ingekuwa imefanya vile hawa wafugaji watapata elimu kwa kuwajengea shule hizi za nomadic boardings. Tupate kujengewa nomadic boardings kwa vile sisi ni watu wa kuhamahama, hizo boardings zikijengwa, mtoto tunaweza tukampeleka shule aende asome, baba naye ahame pahali anataka, lakini mtoto atakuwa amepata haki yake kwa kusoma.

Ingine tunasema matunda ya uhuru: Hiyo uhuru hata sasa bado hatujaiona kwa sababu mtu anavuna matunda akiwa na shamba. Shamba hatuna, matunda tutatoa wapi kwanza?
Kwa vile tungepata shamba, Tana River ni tajiri sana kwa sababu mto kubwa katika Kenya ni huu unapita hapa, haifiki hata

maili kumi, kilomita kidogo sana, kama kilomita nane kutoka hapa.

Scheme ile moja ile tumepata ni hii leo iko hali hii, ingine ni ile ya Hola, ingine ni ile ya Tana Delta. Hizo zote, hakuna ile inafanya na hakuna ile haki, tumeona hapo serikali imepuuza haki za watu wa Tana River.

Lingine wenzangu wamepitia sana ni kuhusu mambo hii ya kitambulisho. Kitambulisho, naona imepangwa, kuna chief, assistant chief imeandikwa katika hiyo form, chief imeandikwa, kuna DC imeandikwa, kuna Registrar, yule mtu wa kutoa kitambulisho. Hapa tumekuja kushangaa, kwa vile hatuna haki, kuna wazee, elders, wale wanatambua yule mtoto, hata wajua siku ile alizaliwa, kuna chief au sub-chief yule ametoka katika sub-location, anajua huyu mtoto ni mtoto wa fulani, kuna chief wa location anakuja anaweka sign, anajua mtoto ni wa fulani, lakini kwa vile hatuna haki unakuta yule DO au DC yule aliye hapo, anasema huyu mtoto mimi simjui.

**Com. Mutakha kangu:** Sasa unataka nani ahusike?

**Kassim Mtagani:** Sasa hii kitambulisho tunataka wazee wahusike.

**Com. Mutakha Kangu:** Irudishwe kwa wazee?

**Kassim Mtagani:** Irudishwe kwa wazee, ile ya zamani, kama vile zamani kuna kimila ile ilikuwa inafanywa.

**Com. Mutakha Kangu:** Na ujaribu kumaliza mapema.

**Kassim Mtagani:** Ingine ni kuhusu hii screening card, hii ya Wasomali. Hiyo kadi imetuletea shida sana, wanaoongea hii lugha ya Kisomali ndio… na hii ilikuwa maoni ya mtu binafsi, alitoa, na alikuwa anataka kujifaidi yeye mwenyewe, sijui. Na huyo mtu, saa hii kule kwao North Eastern, hiyo kadi imetolewa lakini sisi hapa bado, watoto wetu hawapati kitambulisho. Kuna wanawake wengine wamezaa watoto wawili watatu, bado hawana kitambulisho.
Tunaomba katika Katiba mpya, hiyo kadi itolewe kabisa.

Ile ingine tunaomba Tume ichangie ni ya kuwa kutekeleza haki ya wananchi, elimu ienezwe mpaka ndani kwa sababu hapa, ile shida tuko nayo ni kuhusu waalimu.
Waalimu, ikiwa Kenya ni moja, na waalimu wanachukuliwa katika TSC na wanatumwa katika kila district, hii district yetu unakuta ni kabila moja inasomesha.
Hivi juzi tulipata shida ya hii tribal clash ilitokea, shule zetu hazijafunguliwa karibu miezi sita kwa sababu wale walimu walikuwako ni kabila moja tu na wao wakagoma na serikali ilikuwa ikiwaangalia wao macho tu, hakuta utekelezi yoyote serikali imechukua mpaka hivi juzi karibu muhula mbili ilikwisha na watoto…

Kwa hivyo tunaomba serikali, kama ni serikali ya haki, itekeleze elimu kwa kila mmoja, yaani kusomesha Kenya yote.

Nikimalizia, kwa vile ninaona ninasukumwa mbele, hapa kwetu Tana River ninasikia kuna Trust land na kuna hii ya serikali. Trust land, maanake ni ilikuwa zamani serikali ilisema ni kama ile nchi haina watu na sisi watu wa Tana River tunakaa hapa katika hii trust land hii. Nimeshindwa kama serikali wakati hiyo, yaani ilikuwa haifikirii sisi kama ni watu ndio wakasema ni trust land.

Ninataka mwananchi wa Tana River apewe haki yake ya nchi yake ili tupate kama ni ranch, tupate ranches zetu, kama ni kugawa ardhi, tugawe sawa kwa ardhi kwa sababu ukiangia mtoni, kabila zile wanaishi hapa Tana River, kuna Pokomo, Wata, Makarote, Waorma, lakini unakuta katika mto ule, ng'ombe yangu leo ikiwa na kiu ya maji, kuingia ule mto ulikuwa shida ndio juzi ililete hii mambo ya shida.

Sasa tunaomba kama serikali itagawa ile ardhi, wananchi kwanza waelimishwe juu ya faida ya ile ardhi ni nini ndiyo wapate kujua faida yake ni nini. Pahali ya kutengea ng'mbe tutenge, kwa sababu kuna wanyama, pahali pa kutengewa wanyama tujue na pahali pa kulima tujue. Ile ardhi wananchi waelimishwe na tugawiwe watu sawa na haki.

**Com. Mutakha Kangu:** Asante basi. Na tupate Siad Abdulahi. Endelea ndugu.

**Siad Abdulahi:** Salaam Alleikum wananchi? Mimi maneno yangu ni machache kwa sababu kila nilichokuwa nikitaka kuongea, wenzangu wametangulia lakini mimi pia nitaongeza kidogo.

**Com. Mutakha Kangu:** Taja jina.

**Siad Abdulahi:** Jina langu ni Siad Abdulahi.

Sisi hapa Tana River kuna wakulima na wafugaji. Sasa, mkulima na mfugaji ni watu wanakaa mahali moja na tangu mbeleni, tangu ukoloni mpaka leo wanakaa mahali moja. Lakini sasa imeleta shida na hiyo shida nafikiri wale ambao wanaweza wakaitoa shida ambayo wameleta na mpaka dakika hii bado wanatoa nguvu ni ma chief na ma home guard hao.

Sisi tunataka kama vita ilikuwa imetokea, sasa imekuwa salama. Lazima chief na wazee wakae chini waangalie, waongee, sehemu za mashamba na sehemu za malishoni. Si ng'ombe ingie kwa shamba tu na mbuzi au katikati, hapana.

Kipande: Sisi hapa Tana River tuko na shida ya kipande; Utakuta mama amezaa watoto watano na hana kipande na hiyo hatujui maana yake. Kwa hivyo tungependa serikali ituangalilie sana hali ya kipande hapa Bura. Watupatie ili, kuna wazee wa committee hapa ambao wametoka kila location ambao wanajua kila mtu.

**Com. Mutakha Kangu:** Wazee ndiyo wanweza fanya hiyo kazi.

**Mr. Abdalla:** Ndiyo. Apewe, itakuwa kila mmoja ataweza kupata kipande kwa urahisi, kwa hivyo yangu ni hayo. Asante.

**Com. Mutakha Kangu:** Johnson G. Mburu.

**Johnson Mburu:** Kwa jina ninaitwa Johnson G. Mburu na ni Chairman wa Jua Kali, Bura division.
Nikianza, ninatazamia mtazamo mkubwa, hasa kwa watoto wetu ambao ni wadogo. Tunapoanza pale katika serikali ya chini, kwa jamii, tuseme mtoto ni nguzo ambayo inamshirikisha awe mwananchi wa kesho au awe mzazi.
So, unakuta serikali inateuwa vitu vigeni na kiasi cha kufikiwa kiwango cha yule mtoto kufundishwa inakuwa hakuna. So unaona serikali inatoa mtazamo wake kupitisha, tuseme kama sheria fulani upande wa watoto, inawabana njia fulani kiasi yule mtoto wa chini hajapata kuelimishwa. Ninaona ya kwamba ni lazima tu focus, tuangalie mtazamo ama mwelekeo wa kufunza yule mtoto aliye mdogo pale kuanzia miezi tisa mpaka miaka kumi na minane, kuwe na uangalifu.

Nikiangalia kama mtazamo wa kule Ulaya, mtoto anatazamiwa zaidi maana kuna board ya kuangalia mtoto kutoka kwa mama, kutoka nyumbani na kuangalia vile mtoto anavyokua. So, ningeomba serikali itoe mtazamo wa kuteua boards kama hizi za kutoa uangalifu kwa mtoto ili asipatwe na madhara ama asiige tabia ambazo ziko wakati huu, hasa kama vile ulevi, tabia potofu, njia ya kwamba itaweza kuwalinda.

Ninatazamia zaidi kwa mahakama yao pia. Unapoona mtoto anaposhikwa kutoka pale chini nyumbani, akipelekwa tuseme kama ni askari amemshika akampekeka cell, unakuta yule askari pengine anamwadhibu yule mtoto kiasi ya kwamba si kama mtu.
Ningeomba pengine board iteuliwe, board maalum ambayo itashirikisha mwananchi, kutoa mtazamo wake wakati yule mtoto yuko ndani ya cell ama remand, ambayo itakuwa ni board ya kutetea haki ile ya mtoto.

Ninapoingilia zaidi, ninaona mtazamo wa kwamba kuna hatari ya kwamba tunapowaacha watoto wetu kiholelaholela waige tabia potofu, lawama inakuja kwa mzazi. So, ninashirikisha pia court ya Home Affairs litoe mtazamo na sheria kali, ishirikishe serikali ya kwamba mtoto anapoadhirika, baba anachukuliwa jukumu la kuadhibiwa na njia ya kwamba yeye ana huduma ambayo anahisi kupatia mtoto na haki zake kabla serikali kushirikisha tuseme katika haki ya kiskuli, haki ya kihospitali.
Yeye kama mzazi ni mwalimu wa kumfunza huyo mtoto kuliko kumwachilia akawa pengine kama chokoraa kutokana na tabia potofu.

Ninapotoa mtazamo kwa yule mtu anaitwa baba: Unakuta baba ni mtu amekuwa amekuwa akionea mama saa zote katika njia ya kwamba anataka kumkosoa mama ndiyo apate bibi mwingine na mwingine hata wanafika kiasi ya kwamba ni kumi.
So, ninapendekeza ama ninaonelea serikali itoe mtazamo ya kwamba yeye aliye kama baba anastahili kuwa na bibi mmoja ama wawili kuliko kuwa na bibi wengi ambao wanaleta kizazi kikubwa ambacho kitashirikisha jamii ama serikali katika matatizo.

Nikitazamia hivyo ninaona baba ana jukumu na serikali ina jukumu. Kwa hivyo iwe ni sheria itapitishwa na iwe na makubaliano ya kwamba baba anafaa kuwa na idadi ya watoto kuliko kuwa na watoto wengi ambao watakuwa wakiadhirika barabarani ama katika nyanja ambazo si halisi.

Ninatazamia pia kwa kina mama ama kwa kina baba wale wanaoingilia kati katika wapendwa wawili, tuseme kama mtu na mumewe, maana unakuta mimi ni baba nimeoa na ninatoa mtazamo wangu kwa wale watoto wameoa msichana wangu na mimi ni kijana wangu, kutaka kutenganisha. Ninaonelea serikali ingetoa mtazamo mkali na kuikazia sheria zake, kuhukumu yule anayesimama kutenganisha kwa maana atafanya wale watoto wawili wainukie katika nyanja ambazo hazingefaa. Pengine mama aingilie katika nyanja za ulevi, atokomee umalaya na baba aingilie katika nyanja za ulevi na mwishowe baadaye tukose njia yeye anaweza kushirikisha serikali.

Kwa hivyo ninaomba kuwe na sheria madhubuti ambayo italinda baba ambaye anapeana msichana na kijana anayepewa, yaani wale wazazi wawili wanaoshirikisha upande wa watu hawa wawili wakati wa kufunga ndoa ili wawe ni board ya kulinda wale wanaoanza maisha yao mapya.

Ningeomba kuwe na board ya kuwafunza, kushirikisha jamii zao kuanzia chini hadi juu ili baba naye atakuwa na uhuru mzuri na jamii yake, kufunza jamii yake, kufunza jamii yake kimwinukio wa maisha.

Ninaporudi hapo wakati mtoto anapoathirika tunapoona mtazamo wa kwamba watoto wengi wanapowekwa ndani ya seli ama rumande, wanapata madhara kwa vile pengine station ile iko na askari wa kiume pekee yao na saa zingine yule aliyeshikwa mbali, tuseme, kama Bangale akaletwa katika police station hapa ni msichana na station ile haina msichana. So ningeomba serikali ipitishe kama sheria kila police post na station ziwe na wanawake wa kutoa huduma kwa wanawake wenzao, siyo mwanamume anaandamana na mwanamke kumpeleka mahakamani ama mwanamke analala ndani ya cell pasipokuwa na mwanamke mwenzake wa kumchunga.

Unakuta wanawake wetu ama wasichana wetu wanapata madhara katika vijana wanaotoka college na kutoa services zao kwa serikali, so ningeona ya kwamba tuwe na mkazio, na board ya kuchunguza upande ya wanawake kuna madhara gani inayotokezea wanapokuwa ndani ya cell ama marumande.

Pia upande wa vijana vile vile unaweza kuona kijana ameshikwa ni wa miaka kumi na tano hivi, amewekwa ndani ya cell kwa muda na rumande kwa muda, baadaye kukawa na askari ambaye ametoka college kwa siku na amekaa college muda mrefu, unakuta hata pengine yule kijana anaweza pata madhara ya sodomising katika cell.

So, ndiyo hii mimi ninazingatia kuwe na board special ya kuchunguza watu hawa, watoto hawa wawili ndani ya cell na rumande na kuwe na seminars za kuwafunza watu hawa wanapokuwa katika umri mdogo na wawe na uhuru wa kutoa maoni yao, si kuwa ati serikali inachukua jukumu ya kupitisha sheria bila kuwafunza kule nyanjani, ndio sheria ikubalike kupitishwa wanafaa kufunzwa.

Kama sasa koti la watoto limeteuliwa na linashika kasi na watoto wale walio reserve hawajui sheria zao na haki zao. Ningeomba serikali kuchukulia mkakati wa kupitisha miswada fulani, pengine kama watoto, kuwe na seminars to all districts za kuwafunza wale watoto ama kuwe na kamati maalum itakayoteuliwa kuwashirikisha, kuwafunza kama kule Ulaya. Iwe itakuwa inatoa mtazamo wao.

**Com. Mutakha Kangu:** Jaribu umalize sasa.

**Mr. Mburu:** Jambo lingine ninapoitazama ni zile hasara tunazozipata kutoka kwa serikali na njia ya kwamba inapitisha pengine taxation. Pengine unaweza kwenda kama hospitalini ukute kuna cost sharing. Cost sharing hii kwanza inapitishwa kabla layman hajafundishwa maana yake.

Unakuta kitu kama PSV ama VAT inapitishwa kabla mwananchi hajafunzwa na unakuta vitu hivi vinawanufaisha watu binafsi. Pengine katika ile ministry, PS ndiye ananufaika, so ningeona kuwe na mtazamo wa kuwafunza watu hawa kiasi ya kitu fulani kinainukia kimfikie katika daraja inayostahili.

Ninatoa pia mtazamo mwingine wa serikali kuteuwa Commissioners. Unakuta Commissioners ni wengi wa ajabu ama ministry ya Commissioners ni nyingi. Na unakuta Commissioner anapewa daraja kubwa ya ajabu kiasi ya kwamba kumshirikisha mwananchi inakuwa ni taabu.

Kama sasa Commission kama hii yenu, kumshirikisha mwananchi pahali alipo na coordinator, unakuwa kuna utatanishi. Pengine ungeanza kwenda kwa ofisi, uone pengine coordinator yule yuko pale ni mtu wa ubinafsi, pengine ana uhusiano fulani wa kisiasa katika jamii fulani. So ningeomba uteuzi ule wa Commissioners uwe ni uteuzi pengine wewe ni mzaliwa wa Tana River na ungefaa kuwa Commissioner, usiwe Commissioner katika Tana River, uwe Commissioner katika district ingine na yule wa district ingine aje hapa kwetu ili aweze kutoa zile haki zimfikie yule mtu wa kawaida.

Na unawezaona pengine kama coodinator ni mzaliwa wa Tana River lakini huduma zake zitakuwa pengine duni ama zitakuwa za kiubaguzi. Ningeomba wakati mwingine kuwe na njia ambayo itaweza kupatia mwananchi yule wa kawaida inayompasa katika mgeni maana nitakapoingia katika ofisi yake nitatoa heshima.

Kwa hivyo ningependekeza idadi ya Commissioners ipunguzwe maana provinces tuko na pengine sita hivi. Kwa hivyo kama ni uteuzi wa Commissioners tuwe na Commissioners pengine wa electoral tuwe na Commissioners kama sita, pengine hii yenu iwe kama sita, kuliko kuwa na Commissioners wengi wakati nchi inaadhirika kiuchumi, wakati nchi inahitaji misaada na pia tunaomba tusiwe na Commissioners wa kutoka nje kama Ghai vile.

Tuna watoto tulionao wengi wa kutufaa, tunateuwa Commissioner hapa hapa kwetu nchini. Ni hayo ndugu zanguni, ninaona unaniharakisha, lakini ni wakati wangu nitoe mawazo yangu maana sijapata mwalimu wa kunifunza, so wakati ninapotoa mawazo, ninakuomba unipatie muda zaidi.

**Com. Mutakha Kangu:** Unataka muda kiasi gani?

**Mr. Mburu:** Mpaka nitakapokuambia nimekoma lakini ikinikata choo mbele ya mawazo yangu itakuwa ni matatizo so msituharakishe maana ni nguvu yetu leo tutoe mawazo yetu.

**Com. Mutakha Kangu:** Unajua uko na haki na hata hawa wote wako na haki. Ndiyo ninakuuliza, tuongezwe muda kiasi gani tukikupa mpaka umalize na ukipeleka mpaka jioni na wengine? How much more time do you need?

**Mr. Mburu:** Mimi nitatii amri yako sasa maana amri ni kubea kuliko yule anayeitoa, lakini msituharakishe ati kwa ajili ya kwamba mnataka kwenda pahali pengine, ni haki yetu kwa vile tumeona leo, maana pengine ningepewa muda wa ma grassroot hatujafundishwa. So ninaomba wakati mwingine pengine kama kutakuwa na nafasi mtupe nafasi.

**Com. Mutakha Kangu:** Babuka Abdi, huyo amesema ni observer, Salaat Bulale, observer, Abdi Hassan, pia yeye ni observer, Abdi Ghaldesa?

**Abdi Ghaldesa:** **S**alaam Aleikum. Basi mimi ninataka kusema mambo ya usalama.

**Com. Mutakha Kangu:** Sema jina lako.

**Abdi Ghaldesa:** Mimi jina langu ni Abdi Ghaldesa. Mambo ya usalama hapa sasa watu wetu ile siku tulipigana, watu walitoka North Eastern, watu walitoka nchi nyingine.

**Speaker:** Tafadhali karibia kipaza sauti.

**Abdi Ghaldesa:** Usalama wetu hapa Tana River imekosekana, ni mgeni, mgeni hata kama watu wanataka, watu wa Tana river, kila watu wako na nchi yao, district yao, warudishwe huko.

Ya pili ni mambo ya mto Tana: Hiyo mto wetu wa Tana River kutoka barabara mpaka Kipini ni ya Tana River. Lakini mtu akitoke upande hii ya barabara, akipita huko kuna watu wengi, Orma na hata Marakoti, Osanya na -----? Wengine ni wakulima, wengine ni wafugaji lakini mtu akifika mahali inaitwa Roka, kuna wenyewe.

Miaka ya mbele watu waliopigana ni watu wametoka mahali ingine lakini mwaka huu waliopigana ni watu wa Tana River, Orma na Pokomo chanzo cha vita ni mto. Mto ya mbele kutoka ------? Mto yote ni ya Tana River, ni yetu zote lakini mwaka huu imekuwa ni ya Pokomo pekee yao na ikifika hapa, iko na mwenyewe. Mpaka hapa serikali iko na uwezo, mambo ya hiyo jina ya mwenyewe, hiyo mtu anaitwa mwenyewe ipotee. Mambo inaleta vita ni hapo.

Ya pili:  Sisi watoto wetu, kazi ikitokea, sijui ni kwa nini, hawapati hiyo kazi.

Ya tatu:  Sisi tuko na shida moja, hiyo mali yetu ng'ombe na mbuzi, hiyo mnyama akila sisi hatuwezi pata hata kulipa. Ng'ombe na mbuzi hakuna haki ya kulipa.  Hapa sisi wakulima wa scheme, wakulima wako na shida kwani wamefanya kazi kama farasi lakini hawapati hiyo kitu.  Scheme sasa, kama tunavyosikia, imerudi. Je, scheme ikirudi, hapa iko watu wako kwa ofisi hii, serikali iwatoe hawa watu, hawa watu wametunyanyasa kwa ofisi hii.
Kama sasa nyinyi mnataka wakulima wapate haki, hawa watu walio kwa ofisi hii, toeni.

Basi kuna maneno mengi watu wengi wameongea mbele yangu.  Mimi ninafupisha hapa.  Asanteni sana.

**Com. Mutakha Kangu:**  Mzee, weka hapo sahihi.  Mako Manyale ni observer, Abdi Boshi, pia yeye observer, tupate John karanja.

**John Karanja:**  Mimi sina mambo mengi sana ya kuzungumza, mengi yamesemwa na wale walikuwa mbele yangu lakini kwa sababu tuko nyumbani hatukosi moja ambayo imesahaulika kidogo.  Mimi ninaitwa John Karanja ambaye ni mkulima hapa Bura.

Ningetaka kusema yangu ya kwanza ni serikali ambayo tunaenda kuunda kwa uchaguzi ujao, itendee wananchi haki, isiwe dictator kama serikali inayotuongoza sasa.  Kwa sababu kama leo, ikiwa watu wa Bura tumekosa kutoa maoni ya kutusaidia kwa kipindi kama miaka mia moja ingine itakuja, sisi ikiwa mtu anahukumia kwa ile kosa ya amefanya kwa ile kosa amefanya ya kuua, sisi tunaweza kusema hii Tume imetuweka kamba, imetuweka kitazi kwa sababu haikuelimisha wananchi vile inatakikana ndio mnaona wananchi hata ni wachache sana hapa.

Sasa tusipotoa maoni ya kutusidia, nyinyi ndio mmetupoteza.  Ningetaka kusema yangu, haswa nikiingia kwa maoni, ni upande haswa wa DC.  Kwa maoni yangu, ma-DC wangefaa wapunguziwe uwezo wao kwa sababu DCs wanatutumia sisi kama ndiye Rais wa nchi.  Kwa sababu DCs wanatumia njia nyingi, ikiwa DC yule amekuja wilaya yenu hataki maendeleo, anarudisha district yenu nyuma zaidi kwa kazi yake pekee yake na anasema yeye ndiye macho ya rais katika district.

Unakuta serikali ndiyo niseme hivyo, inatumia ma DC kwa njia ingine mbaya kwa sababu unakuta hata wakati wa campaign, ile chama inatawala nchi, unakuta yule Rais ako anamtumia DC kufanya campaign na mwananchi hana haki ya ku claim kwa sababu utakuta hiyo ofisi ya DC, na ndiyo deparment kubwa katika district, kiongozi ambaye ni DC ndiyo inafanya hiyo kazi.
Hiyo ningeona vizuri kabisa, ikiwa haki inatafutwa kwa mwananchi, ipunguzwe na iwekwe sheria ambayo DC akisikika akifanya kazi kama ile, yule Rais amechaguliwa, hiyo ichaguzi ifutiliwe mbali.

Ya pili: Ningetaka kusema tena, Kenya ni nchi tunataka kuendelea na uchumi wetu umerudi nyuma sana, mawaziri wakichaguliwa, wawe wanachaguliwa kulingana na ile kazi mtu amesomea kwa sababu kukiletwa waziri ambaye hajajua mambo ya mifugo wakati huu, hatajua dawa ya mifugo ni gani inatakikana kutafutiwa wafugaji wake.
Akichaguliwa waziri asiyejua mambo ya kilimo, hatajua kitakuwa namna gani, hata ni mbolea gani inatakikana ama ni mmea gani unataka ipandwe mahali kwa sababu wale wamechaguliwa wamerudisha nchi yetu nyuma hata ukienda kumwelezea kitu kimeharibika, anashindwa ni kitu gani hiyo unaenda kumwelezea.

Sitaki kuendelea sana mambo mengi, ningetaka kusema hata Rais asikae mda mrefu sana, asikae kupita miaka mitano. Achaguliwe mtu aliye na huruma wa kuokoa nchi yetu.

Lingine ni juu ya mashamba: Kama sasa mashamba Kenya, kila mtu anadai ni kweli ni mwananchi amepata uhuru, hii nchi ni yetu, ilipiganiwa ikatoka kwa ukombozi kutoka kwa mkoloni, na mwananchi ako na haki ya kurithi na kupata ardhi katika nchi yake kwa sababu akikosa kupata nchi yake atapata nchi gani na yeye si mkimbizi?

Ningetaka kusema wale watu ambao hawakubahatika kupata ardhi sehemu zingine, serikali itawachukua ikawapeleka mahali ingine, ma scheme ambayo iko within Kenya, tuseme yote ni nchi yetu.
Ningeomba mimi katika Katiba inayobadilishwa sasa, hayo schemes yawe yakilindwa na serikali kwa njia ya uangalifu. Kwa sababu ingine ni kilimo ambayo kinaweza kuwa na gharama ya juu, kama tukisema kwa mfano, kama hii ya Bura na sehemu zingine, inakuza mimea na kunyunyizia maji mashamba. Ikiwezekana kuwe na ministry yake ambaye waziri atakuwa amesimamia. Hiyo mashamba ambayo ni scheme ya serikali na inagherimu pesa mingi ya serikali, iwe na waziri wake ambaye inahusika na mashamba ya kununyizia maji mashamba ndiyo iweze scheme kama hizo zikianguka. Kama hapa Tana River tuko na tatu zimeanguka, ziwe zikijulikana mambo yake haraka kuliko kitu kikiharibika kinamalizika miaka kama ishirini, kama hii yetu ya Bura inaelekea kumaliza miaka kumi na moja sasa ikiwa imelala na serikali iko.

Sina mambo mengi ya kusema kwa sababu mengi wengine wamesema na wamerudia, sitaki kurudia.

Ya elimu mimi ningetaka kusema kwa sababu serikali yetu inaendelea na ikiwa wabunge wanaweza kupata karibu milioni moja, mawaziri, mishahara, ningesema hata mimi serikali haiwezi kukosa pesa ya kusomesha watoto kutoka nursery mpaka form four; inaweza pata pesa kwa sababu sisi ndio tunatoa kodi, iwe ikiwalipia school fees kwa sababu wananchi wamerudi nyuma sana kumaendeleo na hata pesa hawana.
Hiyo ningetaka nirudie, ilikuwa imesemwa na hata mimi nimeongezea hapo tu, hiyo ningeomba serikali iweze kusomesha watoto kutoka nursery mpaka form four.

Nimemalizia sitaki kusema maneno mengi, nilikuwa nimeandika kwa kifupi tu. Asante.

**Com. Mutakha Kangu:** Asante basi. Hellen Njeri?

**Speaker:** Andikisha pale.

**Hellen Njeri:** Kwa jina naitwa Hellen Njeri Karibo.

**Com. Mutakha Kangu:** Endelea

**Hellen Njeri:** Mimi nimekuja kwa ajili ya kuongea kuhusu wanawake; sisi wanawake wa hapa Tana River tumeonelea tuwe tukipata mambo haya ya social services. Hatupati mikopo vile inahitajika kwa ajili tangu tuanze hivi vikundi vidogo vya kujisaidia wakina mama, hatupati mikopo, mikopo tunasikia ina kuja na inarudishwa Hola au Nairobi bila sisi wanawake kujifaidisha na hiyo mikopo.

**Com. Mutakha Kangu:** Mikopo inatoka wapi mama?

**Hellen Njeri:** Kutoka kwa serikali. Tungeomba serikali nayo iangalie wakina mama sana kwa ajili sasa tukikosa kujisaidia, hatuna mtu wa kutusaidia hapa. Serikali ndiyo tunaangalia sana. Hatuna kilimo, hatuna chochote na tukipata kazi kidogo kidogo ya kusaidia watoto wetu, inaweza kutusaidia.

Kuhusu watoto wetu: Watoto wetu hasa wale walemavu wamekosa elimu sana. Hakuna shule hata ya walemavu tumepata katika district nzima. Watoto wengi wale walemavu wanakaa manyumbani bila kupata elimu. Wengine ni viwete na hawana pesa ya kununua ile miguu ya kwanda nazo, wengine wanaenda na mkono, wengine wanaenda na miguu bila kupata huduma.

Tuone kama hawa wenda wazimu: Watu wengi hapa kwetu Tana River, wengine ni wenda wazimu, hawawezi kupata madawa ya kuwatibu juu ya hiyo wazimu yao, wengine hawajui Nairobi, wengine hawajui mtoto wake atafanywa nini ndiyo apate huduma ya hospitali.

**Com. Idha Salim:** Sasa mama, ungetueleza ni mambo unataka ifanywe. Tupe mapendekezo yako.

**Hellen Njeri:** Mapendekezo ya?

**Com. Idha Salim:** Elimu ya watoto, walemavu….

**Hellen Njeri:** Kuhusu watoto walemavu, tafadhali wawe wanajengewa shule ya walemavu. Hapa Tana River hakuna. Wengine viwete, wengine wazimu, hawawezi kujisaidia.

Kuhusu ugonjwa ndiyo nilikuwa ninasema hakuna mahali wanaweza kupelekwa, hawajui kupeleka mbali kama Mathari. Tunasikia watu wengine wanapelekwa Mathari kwenda kutibiwa huko. Watu wa hapa ni maskini, hawana pesa ya kwenda mbali namna hiyo.

Kuhusu biashara: Biashara zamani tulikuwa tukifanya kukiwa na mambo ya kuwa kama iko kiwango chake cha pesa lakini siku hizi mtu anafanya biashara yake vile anataka. Sasa biashara ikiwa itakuwa namna hiyo, mambo mengi ndio inaleta uchumi kuwa chini. Afadhali tungekuwa na kiwango ya kama vitu vinauzwa, ni serikali ipeane kiasi ya kuonyesha vile watu watakuwa wakiuza. Wengine wanauza chini, hata mwingine hajui vile anauza, anauza vibaya chini, anaenda hasara. Hakuna elimu ya kutosha kuhusu kuelimishwa juu ya biashara.

**Com. Idha Salim:** Kwa kina mama si wazee?

**Hellen Njeri:** Kwa kina mama hata wazee wanahusika huko.

Mengine ni hii tunasema kuhusu watoto kupata kutahiriwa: Mimi singeunga mkono watoto wa kike watahiriwe kwa ajili sasa wakitahiriwa wameharibu miili yao na tena ile damu inatoka hakuna mtu analipa, tena mtoto anatahiriwa anakosa damu, damu inaisha kwa mwili na mama anaona ati ni raha na hiyo hakuna raha.

**Com. Idha Salim:** Wewe hupendelei?

**Hellen Njeri:** Sipendelei watoto wa kike kutahiriwa.

Mambo ingine ni hii mambo ya hospitali: Tunaweza kwenda hospitali na tukose huduma vizuri kwa ajili ya hiyo mambo ya kutahiriwa.

Kuhusu koti: Imeonekana ukishikwa upeleke kotini hapa polisi, unapewa siku ya huko unakaa siku mbili, upelekwe rumande ukae siku tatu halafu ukipelekwa hukumuni, ile siku ulikaa hukumuni na seli hakuna kitu imehesabiwa hapo, unahukumiwa kutoka hapo.

Ningeomba koti au serikali iangalie hapo kwa ajili watu wengine wanateseka rumande wakingojea hukumu. Hukumu ikitajwa hakuna kwenda kuhesabiwa ile siku yako ulikaa kwa rumande. Hiyo nayo inakuwa ni shida sana kwa wananchi.

Yangu ni hayo.

**Com. Mutakha Kangu:** Asante sana. Anastasia Mukundi, ni observer, Makai Shalambo, observer, Ilai Kesane, observer,

tupate Peter K. Kwambai.

**Peter K. Kwambai:** Yangu ni kusema asante kwa Tume kwa sababu wametuwezesha kufika hapa ili tupate nafasi ya kutoa maoni yetu kuhusu Katiba ya siku zijazo.

**Com. Mutakha Kangu:** Taja jina.

**Peter Kwambai:** Kwangu ni Peter Kwambai na ni mkulima kutoka Bura.
Basi, yangu ya kwanza ni kuhusu habari ya utawala kwa Rais:
Namba moja ni kuhusu kuchaguliwa kwa urais: Mimi ningeomba Tume ya kwamba kuchaguliwa kwa urais achaguliwe moja kwa moja badala ya kupitia kwanza awe mbunge kwa sababu mtu akiwa atachaguliwa kwa ubunge, tutampoteza yule mtu ambaye Mungu amechagua, ambaye angekuwa Rais, lakini pia ni kwa sababu huyu Rais ana kazi nyingi ya taifa nzima, ni vyema kuchugua Rais moja kwa moja bila kupitia ubunge ili kazi yake ipate kuwa rahisi.

Namba ya pili ni kuhusu mambo ya utawala wa urais: Ningeomba ya kwamba katika mambo ya kuongoza kwa Rais, kila wakati tangu tuliponyakua uhuru, ilikuwa ni kuchaguliwa miaka tano tano. Kama wananchi wanakukubali, utarudi katika hiyo miaka tano ingine na kama wananchi wanaona kwamba kazi yako si sawa, basi itakuwa wewe urudi nyumbani kuchunga kama wananchi wengine.
Ombi langu ni kwamba katika wakati wa vyama vingi, waliweka sheria fupi sana na hiyo sheria siyo ya Waafrika, pengine walitafuta kutoka katika sehemu za Amerika kwa sababu walikuja kuweka ya kwamba miaka kumi, Rais atawale.
Mimi ningeomba ya kwamba hiyo namba ya miaka ya miaka kumi iondolewe kwa sababu kama ni kijana ya miaka thelathini na tano, anaongoza serikali vizuri, miaka tano anafanya campaign, anarudi kwa kila miaka tano. Kama yeye si vyema katika utawala wake, atakuwa anarudi nje na kama kazi yake ni nzuri katika ile miaka tano ingine, ni vizuri awe na nafasi ya kugombea kwa sababu katika utawala, si watu wote wanaweza kutawala. Ni kipawa kutoka kwa Mungu.

Kwa hivyo ningeomba ya kwamba katika ile sheria waliweka juzi juzi tu,miaka kumi iliyopita, iondolewe hiyo namba ya miaka kumi. Yaani iondolewe iwe free,yaani iwe tu ni ya kila miaka tano, agombee kiti.

**Com. Mutakha Kangu:** Ukiwa mzuri unaendelea.

**Mr. Kwambai:** Ukiwa mzuri unabaki kuendelea bila kuwekewa mpaka.

**Com. Mutakha Kangu:** Haya! Enda mbele.

**Mr. Kwambai:** Ya tatu ni kuhusu Bunge, Bunge mbili: Bunge mbili kwa sababu ni vyema tuwe na Bunge ya wazee na Bunge

ya kawaida. Ninasema hivyo kwa sababu Afrika nzima imepata taabu nyingi sana kwa sababu yule Rais mmoja akipinduliwa na jeshi, wananchi wanabaki taabani sana. Kitambo kwenda kurudisha Rais mwingine imekuwa na taabu nyingi ndiyo unaona Afrika imekuwa na shida kwa ajili ya Rais mmoja, ndiyo wale majeshi wanapata nafasi ya kupindua.

Kwa hivyo mimi ningeomba ya kwamba Rais wawe wawili, yaani Bunge la wazee, ile inaitwa Bunge la Senate, upper house na lower house ili huyu Rais wa chini kama atakuwa anatumia amri kwa njia isiyofaa, basi itakuwa wale wazee watakuwa wakimfunza. Pia ninafikiri serikali haiwezi kupinduliwa kwa sababu kuna Bunge la wazee na kuna Bunge la kawaida. Kwa hivyo ningeomba ya kwamba ziwe Bunge mbili katika hii sheria ili tupate amani.

Namba la nne….. niko kwa ngapi?

**Com. Mutakha Kangu:** Sema tu ukiendelea hata kama hakuna kupeana namba.

**Mr. Kwambai:** Sawa sawa. Nataka nisije nikapita kwa sababu ni maneno muhimu. Basi namba nne ni kuhusu mambo ya chiefs.

Ningesema kuhusu mambo ya chiefs ya kwamba kila wakati katika chiefs wako assistants wao na kuna wazee wale wa mtaa wa kusimamia area. Ningeomba ya kwamba katika wale chiefs, wapigwe transfer katika round ya district. Kwa sababu wako chiefs wengine wanaweza kufanya kazi maendeleo mazuri, ni vizuri hayo mambo ya maendeleo izunguke katika district; na kama itakuwa ngumu, huyo chief apigwe transfer, chiefs wazunguke katika division ili mambo ya maendeleo ipate kusonga mbele kwa sababu kila wakati wananchi wanapata shida kwa sababu yule chief anajua ya kwamba hakuna siku ambayo mimi nitapigwa transfer kwa hivyo anakuwa na unyonge wa kufanya kazi, amezoeana na watu zaidi na utakuta ya kwamba watu hawaendelei vyema.

Kwa hivyo chiefs wapigwe transfer katika district.

**Com. Idha Salim:** Wasipigwe transfer kwingine?

**Mr. Kwambai:** Kwingine hapana, wazunguke katika district.

Jambo la sita ni kwamba katika Kenya wakati tupate Waziri Mkuu kwa sababu katika Kenya wakati huu tumepata wasomi wa kutosha, tumepata mali ya kutosha, kwa hivyo kama tuko na utawala wa Rais, utawala wa wazee, utawala wa Waziri Mkuu, tunaona ya kwamba imegawanya kipande katika ile utawala. Na utaona ya kwamba serikali itakuwa tight kwa sababu ni watu wengi wanaongoza ile serikali. Na ninafikiri katika Afrika mzima, ni Kenya tu na Tanzania ambayo imebaki katika amani.

Kwa hivyo nigeomba ya kwamba tupate Waziri Mkuu ili Kenya ipate kunufaika katika amani kama tulivyoendelea kwa miaka thelathini na tisa wakati huu.

Sisi tuna wasiwasi kwa sababu huyu mzee wetu alikuwa ni mzee wa kutulia na ana maarifa mengi. Hatujui vile yule atakuja

kutawala, kama atatumia power zaidi ama atatumia ukabila lakini kama kuna sehemu sehemu katika ile utawala, basi ninafikiri watafanya kazi vyema na mambo ya amani itazidi kuendelea.

**Com. Mutakha Kangu:** Jaribu kumaliza.

**Mr. Kwambai:** Langu la mwisho kabisa ni kuhusu mambo ya kuunda Bunge au kuunda serikali. Ningeomba ya kwamba katika wanavyama vyote, wale wamejiandikisha katika Kenya, wakati wa kuunda serikali, wengine wamepata wabunge watano, wengine wamepata mbili, wengine wamepata kumi.

Ningeomba ya kwamba hao wabunge, kutoka vile vyama vyote, wawe na nafasi ya kuunda serikali pamoja. Wewe ulete waziri wako wawili, huyu alete mmoja, huyu alete watatu na waunde serikali iwe pamoja kwa sababu tumepata shida tangu juzi ilipowekwa vyama vyama vingi kwa sababu katika serikali ambayo inaongoza, kuna wafanyikazi wengi kama DC, kama Katibu, kama wengine, sasa wanafanya contract, wanafanya kibarua kwa ile chama ambayo inaongoza.

Wewe huwezi kujua ya kwamba anavuta kamba, anavuta kamba, hawezi kufanya kazi kwa sababu anataka ile serikali iko mbele halafu ndugu yake apate kuchukua lakini kama wote wataignia serikalini pamoja, watafanya kazi wakiwa wafanyi kazi wote, wakijua ya kwamba serikali ni yetu na ninafikiri ya kwamba kazi hiyo itaenda vyema. Na hata wakipitisha kitu katika Bunge, watakuwa wakipitisha kwa sababu wana nia moja ya kwamba serikali ni yetu.

Basi asante kwa Tume.

**Com. Mutakha Kangu:** Mohamood Garso, observer, Halima Shaffarti, observer, Aretho Bakari, pia huyo ni observer, Mohammed Wario?

**Mohammed Wario:** Asante sana Commissioners. Tunawashukuru kwa kututembelea.

**Com. Mutakha Kangu:** Kama hatujaendelea Bwana Wario, tunataka kutambua Bwana Mheshimiwa amekuja kuungana na sisi, tutampa nafasi ya kuzungumza baadaye lakini wacha tuendelee na wewe. Asante.

**Mohammed Wario:** Asante. Mimi ni Mohammed Wario na pia team leader ya kamati ya uwakilishi bungeni ya Bura Constituency.

Mengi yameongelewa na wenzangu, mimi nitakuwa na machache tu ya kuongeza.

Ya kwanza nikiongea kuhusu serikali: Serikali na mwananchi wa kawaida ni watu wawili ambao wameandikiana mkataba na kila mtu yuko na wajibu wake wa kufanya. Kwa mfano, wajibu wa mwananchi ni kutoa ushuru vile inavyotakikana kulingana na Katiba ya nchi, na kutiii sheria ya nchi na kadhalika. Baada ya hapo sasa, serikali wajibu wake ni kupatia wananchi mahitaji yale ya muhimu kwa mfano elimu, afya, usalama, na pia uchumi wa taifa au ya mwananchi wa kawaida.

Mwananchi hakuna siku ambayo ameshindwa kutoa ushuru kwani ni lazima atoe au zingine anatoa kwa njia ambayo yeye mwenyewe hajui lakini sasa serikali inashindwa kutimiza wajibu wake. Kwa hivyo kungekuwa na kifungu cha sheria ambacho kinaweza kusimamia serikali iwe ni lazima ipatie mwananchi elimu ya bure, afya ya bure, usalama wa kutosha na kuinua hali ya kiuchumi ya mwananchi na kuwe na kifungu, kama serikali haikufanya hivyo, serikali hiyo aidha iondolewe mamlakani au ishtakiwe.

Ya pili: Wenzangu hapa waliongea kuhusu miradi ambazo zimekufa kama Bura irrigation scheme, Hola irrigation, TARDA na kadhalika. Nikiongezea juu kuhusu miradi ya Bura, watu walitolewa wengi kutoka sehemu mbali mbali za Kenya, wengine walikuwa na mashamba kidogo kidogo wakaziuz wakitarajia ya kwamba watakuja kupata faida lakini kuja ikawa mashamba hayo yamekufa, wananchi wanapata taabu, madhara wanaletewa na serikali, mahali walikuweko wametolewa.
Kwa hivyo serikali hiyo ilazimishwe na Katiba kuwalipa fidia hao watu ambao wameharibiwa maisha yao na serikali.

Na miradi mengine ambazo zimeuawa kimakusudi katika taifa hili, nikitoa mfano kama factories za sugar kama ya Ramisi na zingine. Tumeona ya kwamba miradi zingine zimeuwawa kimakusudi ili kunufaisha watu fulani. Taifa la Kenya siyo nchi ambayo ingekuwa inahitaji kuleta sukari kutoka nje. Tunaweza kutoa sukari ya kutosha, tunaweza kutoa pamba ya kutosha. Kwa hivyo kuwe na kifungu cha sheria kuwa serikali isilete vitu ambavyo sisi wenyewe tunaweza kukuza na iwe ni hatia kwao ku-import vitu ambavyo zinaweza kukuzwa katika taifa hili letu.

Ya tatu, nikienda haraka kwa sababu ya masaa, ni kuhusu uajiri wa vikosi vya usalama: Ni hatari kwa nji kuajiri wanajeshi kutoka kwa kabila fulani kwa wingi kwani tumeona madhara kama hiyo kama sehemu za Rwanda, Burundi na nchi zingine.
Kwa hivyo wakati serikali inaajiri vikosi kama hivyo, itangazwe kwe taifa nzima, ijulikane ya kwamba mwaka huu taifa la Kenya inaajiri wanajeshi wangapi na kila wilaya iwe na quota system na kila kabila iwe na nafasi ili kuwe na usawa katika uajiri kwa sababu vijana pia wanahitaji kuajiriwa kwa wingi.

Nikiongeza ya nne ni mambo ya mipaka: Nimesikia wengine wanasema mipaka inasongeshwa hapa na pale. Ninafikiri ingewekwa Katiba ya kwamba mipaka ile ambayo imeekwa ya wakoloni, kutoka mwanzo administrative boundaries ziheshimiwe na zibaki vile vile na kama kuna mabadiliko, ikaliwe, kama iundwe tume, kama ikionekana kwamba kuna haja, ndiyo ibadilishwe lakini siyo kubadilisha mipaka ovyo ovyo.
Kuhusu DDC na Tender boards vile wenzangu walitanguliza, ninafikiri hao ambao wanaitwa departmental heads kuwa kama wanakamati wa hizo Tender Boards au DDC na si wakaaji wa hapo, hata kama watakuwa members, wawe wanakaa hapo kama technical assistants lakina wasiwe na uwezo wowote wa kutoa tender, hata akiwa ni DC, asiwe mwenyekiti. Mwenyekiti na kamati wengine ambao watakuwa na uwezo, wale wawe wakaaji wa pale pale, ambao watajua tatizo la hapo.

Nikisonga mbele nambari ya sita, ni kuhusu mamlaka wa Rais: Katiba iliyoko sasa inampatia uwezo sana Rais wa taifa, kama ku-appoiint mawaziri, ma-Commissioners wa Tume ya uchaguzi, ma Jaji Wakuu na kadhalika.

Kwa hivyo ningependelea hii mamlaka ya Rais, ninafikiri tuko na mikono tatu ya serikali kubwa kubwa; the Executive, the Judiciary na Parliament. Hizi mamlaka, vile ziligawanywa katika hizo sehemu tatu, ili hawa watu watatu, wawe kila mtu akitaka kufanya kitu, awe anaogopa huyu, yule anaogopa yule ili mwananchi asiumie hapo katikati lakini tukiweka uwezo kwa mtu mmoja, itakuwa mwananchi anaumia.

**Com. Idha Salim:** Uwezo wa nani?

**Mohammed wario:** Uwezo wa Rais ipunguzwe, igawanywe.

**Com. Idha Salim:** Kati ya nani?

**Mr. Wario:** Kati ya hizi mikono tatu; Executive, ingine iende Bunge, ingine kwa Judiciary.

Matumizi ya pesa: Kama budget inasomwa, ingekuwa vizuri kwa serikali itangaze kwamba ni pesa kiasi hicho imetolewa na ipatie kila wilaya quota yake na siyo kwamba ati wilaya fulani inapata nyingi kuliko zingine. Ile keki igawanywe sawa kwa sawa kwa kila wilaya, hata kama ina population ndogo.

Nikirudi nambari ya nane ni mambo ya ardhi, nafikiri wengine wameongea. Itolewe katika mikono ya serikali na pia rasilmali pia isimamiwe na wananchi wenyewe.
Kwa mfano tuko na Game Reserves ambazo zinasimamiwa na serikali, haina faida yoyote kwa mwananchi wa kawaida, haujui pesa zinazopatikana zinaenda wapi. Kwa hivyo hivyo vyote viwekwe mikononi mwa wananchi wenyewe ili wapate faida kwa rasilmali zao.

Nikiongea kuhusu ushuru: tunasikia au tunasoma kwa magazeti kwamba mtu fulani amekwepa ushuru wa serikali, pengine milioni mia tano, na hatuoni hatua yoyote anachukuliwa. Kwa hivyo kuwe na kifungu fulani ambayo mtu yeyote atakaye kwepa kutoa ushuru wa serikali, huyo hakukosea serikali bali amekosea mamilioni ya Wakenya kwa sababu huzo mamilioni ambazo amehepa nayo ingesaidia watu wengi.
Kwa hivyo kuwe na kifungu ambayo watachukuliwa hatua kali hata kama ni ya kifo.

Nambari ya kumi ni kuhusu service charges: Tunasikia kuna service charges sijui inaenda kwa local authority lakini hatuoni ni kazi gani hizo charges zinafanya. Kwa hivyo kama hiyo service charge itakuweko, hizo service charges afadhali zipelekwe kwa ministries zile muhimu ambazo saa hii tunaambiwa ya kwamba kwa sababu ya hali ya kiuchumi haiwezi kusimamia vitu vingine kama ya elimu, ili kusaidia watoto kuwanunulia vitabu, ili wananchi wa kawaida wasisumbuliwe na zingine ziende kwa mahospitali ili wananchi wasiulizwe pesa wakati ambapo wanakuja hospitali kwa sababu sehemu kama hii unaweza kuleta mtoto mgonjwa hospitali na kwa sababu hauna shilingi, unaambiwa rudi na huyo mtoto na anaweza akafia njiani, na hiyo

imetokea mara nyingi.

Ya kumi na moja ni kuhusu Katiba yenyewe: Katiba hii tunaendelea kuunda lakini kuna wengine pengine hawataiona. Kwa hivyo ningependelea hata baada ya kuundwa, hii elimu ya raia iendelee ili kila mwananchi ajue ile katiba yake ambayo ameiunda ili ajue njia ile ambayo atafuata.

Ya mwisho ni kuhusu vyama vya kisiasa: Tunasema Kenya ni nchi ya vyama vingi sasa kila siku tunaona chama kinaongezeka mpaka itafika sijui arobaini na ngapi. Sasa kama vyama itakuwa milioni moja, inakuwa vigumu kuondoa serikali ambayo iko pale mamlakani na inaendelea kukosea mwananchi.
Kwa hivyo kuwe na idadi maalum, hata tukisema ni mbili, ili hii ikikosea tunatoa hii tunaweka hii, lakini tukisema vyama vingi tu ambavyo havina mwisho, ninafikiri si vizuri.

**Com. Idha Salim:** Unapendekeza ngapi?

**Mr. Wario:** Viwili. Asante.

**Com. Mutakha Kangu:** Asante basi. Abona noor, huyo ni observer, Halima Hassan, ni observer. Maybe basi tumsikize Mheshimiwa kama bado tunangoja karatasi ingine. Mheshimiwa.

**Hon. Mohammed Abdi Galgallo:** Mabwana Commissioners wa Constitution of Kenya Review Commission, kwanza nawashukuru kwa kuwa mmefika hapa.

**Com. Mutakha Kangu:** Mheshimiwa, for recording purposes, you mention the name so that it can be recorded with us.

**Hon. Galgallo:** Okay. Mimi jina langu ni Mohammed Abdi Galgalo, mimi ndiye mbunge wa Bura ambapo ninapenda kuwakaribisha nyinyi kwa kuja kuchukua maono ya watu wanyonge.

Jambo la kwanza Bwana Commissioner, sehemu tulioko sasa, ambapo ni wilaya ya Tana River, ni sehemu ambayo haikutambuliwa kama sehemu ya kenya. Haikutambuliwa na wakoloni kwa sababu hali ya anga haikuwapendeza; jua ni kali, pana mbu wengi, haina altitude njema ya wao kukuza zile walikuwa wanazitaka, communication kutoka hapa kwenda Nairobi, Mombasa ilikuwa ngumu. Kwa hivyo ni sehemu imekuwa katika Kenya tu basi, lakini ni serikali ya mkoloni haikushughulikia kabisa.

Tumeachwa nyuma kwa mambo ya elimu, tumeachwa nyuma kwa mambo ya kukuza chakula, tumeachwa nyuma hakuna stima, tumeachwa nyuma hakuna barabara ya saga.

Kwa hivyo yote hayo tukichanganya ilikuwa ni sehemu ambayo haikuhesabiwa kama Kenya na baada ya sisi kupata uhuru, kumetokea matatizo jirani ng'ambo ile na watu wetu hapa pia wameumia sana kwa sababu ya spillover. Kwa hivyo kwa kuwa tuko karibu sana na wale, ikawa sisi imewekwa kama buffer,
Tana river was regarded as a buffer between the hostile north and the stable Kenya.

Wakati mambo yamekuwa sawa na watu wa North Eastern wamewacha ile siasa ya kutaka kujitenga, ikawa manake wao wamepata priority na huduma za serikali zimeenda huko nyingi. Sisi tumekaa kama buffer, tumerukwa. Mambo yanafanyika upande ule mwingine na yanafanyika upande huo mwingine.

Ninataka kusema bwana Commissioner, tumekuwa marginalized kiasi cha kuwa sisi tukiwa katika Coast province, hasa wilaya hii na constituency, hii inahesabiwa haiko katika North Eastern, wala haiko Coast province, sababu haupati share sawa na sehemu zingine, divisions zingine za mkoa wa pwani, na pia haiko katika eastern.
Kwa hivyo ninasema sisi kwanza kikatiba, nataka kuwakumbusha historia kwamba constituency hii kabla ya Lancaster House, ilikuwa inatawaliwa kutoka Garissa district na haikua katika ---? na Tana River, constituency hii ya Bura. Lakini baada ya kujadilia Lancaster House na kufanya serikali ya majimbo, sehemu hii ikarudishwa katika Coast province, maanake sisi hatakuwa na jambo kwa sababu hata Coast province pia ni sehemu ya Kenya.

Lakini sasa hatupati share ya mkoa wa Pwani, hatupati share ya mkoa wa Mashariki na hatupati share ya Mashariki Kaskazini, tumeajwa hapo katikati. Ndiyo ninasema tungetaka hata ma officers wanaokuja kufanya kazi hapa, wanafanya kazi kusukuma siku tu. The commitment hamna na hapo ndiyo mahali kumekuwa na clashes nyingi. Tuna- clash na watu wa North Eastern province, saa ingine tuna-clash na watu wa Ukambani, na hii imetuumiza sana, imesemekana sisi mahali tuko hali ya amani ni mbaya na hata madaktari hawataki kuja kufanya kazi kwa sababu ya situations ambazo zimetengenezwa na serikali.

Kwa hivyo ninasema kikatiba tunataka tuwe sehemu moja katika Kenya, katika mkoa wa Pwani kamili na tunapata allocations zetu na tunaletewa officers ambao wako dedicated kutumikia serikali, si kuleta officers hapa kwa punishment sababu walikosea kufanya kazi vizuri kwingine.

Jambo la pili: Mzungu ameanzisha Hola irrigation scheme hapa kuwaweka MauMau detainees; imefanya vizuri mpaka tukapata uhuru, imefanya vizuri. Serikali ikasema, kwa recommendations za Food and Agriculture Organization, ya kwamba kwa sababu sehemu kubwa hapa iko na black cotton soil, inaweza kukuza pamba, na wakaanza survey, wakaanza kutoka Bura, walisema itaenda mpaka Wenje. Na FAO ika-convince European Union itoe pesa ya kuweza kukamilisha mradi huu.

Pesa zilimiminwa, mradi ukaanza,watu wameletwa kutoka kila mahali Kenya hii kuja kuwekwa hapa. Mradi huu ulikuwa umepangiwa kuwe na vijiji ishirini na tatu. Pesa zilizotolewa ziliwa 5.7 billion Shillings kutoka kwa European Union and the Kenya government was supposed to contribute the same amount. Walifanya vijiji kumi badala ya ishirini na tatu. Wamefanya,

wameweka pump station ambayo inakunywa mafuta kuliko kuweka gravity. Tenants wamejengewa nyumba ya matope ovyo, when they were supposed to get permanent houses. Hiyo yote ilikuwa ni uporaji na ambayo inaonekana hata serikali imekubalia kwa hivyo wakati mtu anakaa hapa na anasema sisi tungeomba compensation kwa sababu watu waliwekwa na serikali ikaruhusu hizo scheme zififie.

Tunataka Katiba ambayo italazimisha serikali kutochukua sehemu yoyote ya ardhi ya watu, kuweka mradi bila kuhakikisha ya kwamba itakamilisha huo mradi. Katiba ambayo italinda ardhi ya watu pamoja na wananchi ya kwamba ikiwa serikali itaamua kuchukua hiyo ardhi, kwenda kufanya mradi fulani, serikali hiyo inalazimika kukamilisha huo mradi kama imetoa ardhi kutoka kwa wananchi hawa. Na kama haikukamilisha, Katiba italazimisha hiyo serikali ikamilishe huo mpango la sivyo itawalipa wale wananchi ambayo iliwanyang'anya hiyo ardhi na wale wananchi ambayo imewaleta na ikawaacha ovyo bila ownership ya ardhi.

Tunataka Katiba ambayo itazuia serikali kuchukua ardhi ya watu na kwenda kukodishia mwingine bula kuleta manufaa kwa wenye ardhi hiyo. Ninaweza kupa mfano; 1966, serikali ime apportion 1.5 million acres of land na ikamkodishia Mzungu anayeishi Amerika, hiyo ardhi inaitwa Ghalana Game and Ranching na alikuwa amepewa lease ya forty-five years. Masharti ambayo yalikuwa katika mpango huo ni kwamba kila mwaka kwa majirani waliokuwa hapa karibu, wenye hiyo ardhi, ambao walizuiliwa wasiingie, watachimbiwa dam na borehole every year na kwamba part of that agreement was 12% of the share ya hilo shamba, itapewa wananchi wenye hiyo ardhi ambao walikuwa jirani. Yote haya hayakutendeka na twenty years later, serikali ime-reposses hiyo ardhi na ikapeana agency yake kwa jina la ABC.

Tuliambiwa wakati huyo na ndiyo ilikuwa agreement ya kwamba hao baada ya muda wa miaka kumi na miwili, watakuwa wameweka ng'ombe elfu arobaini na tano ambazo pia sisi tutatumia kama breeding herds kwamba sisi tunaweza kwenda kuchukua bulls kutoka kule, zitakuwa zikifanya part of it breeding na part of it ranching ambapo tukianza kuweka ranches sisi wenyewe, bulls tutapata, breeding herds tutapata kutoka kule.

Leo, mpaka saa hii, the government holds that land. Wananchi wa hapa hawaruhusiwi, tumekatazwa access ya mto Sabaki kwa sababu serikali imeamua kunyakua hiyo ardhi na kwamba wakati huu kwa sababu ya concentration, serikali haikuhusika kujengea watu mabwawa ya maji, kuwatengezea hawa accessibility ya maji ya aina ingine yoyote, baada ya kuwafungia Sabaki concentration ikawa na river Tana, ndiyo inaleta pressure kwa mto hapa, ndio sababu tumekuwa na vita vya aina ya makabila kati ya wafugaji na wakulima kando kando ya mto. Ni mpango wa serikali kuchukua ardhi ya watu kwa nguvu, kwenda kukodeshea wengine na baadaye kunyakuwa kama mali yake na kuzuia wananchi wasifikia Mto Sabaki.

Tungetaka Katiba inayokuja, rais wala nani, hatakuwa na uwezo wowote wa kunyakuwa ardhi kwa mahitaji ya agency fulani ama kwa mahitaji ya binafsi, unless it is serving, it is in the good cause of the general Republic of Kenya.

La tatu, nataka kusema land reform. Nchi yetu imekaa, ardhi yote ni ya serikali, be it state land or trust land. Lakini serikali pia

imeshikilia kwa masilahi ya wananchi wa sehemu hiyo. Na kama alivyosema, kama ni adjudication inakuja, adjudication ifanywe ile inaweza kusaidia wakaaji wa sehemu hiyo. Hii ni serikali imesukuma mambo ya adjudication, tunataka Katiba mpya isimpe President uwezo wa kuchukua ardhi na kumpa mtu kwa sababu yeye ni raisi ama for political favours.

Tumeona sehemu za Pwani, sheria inasema ikiwa utachukua sehumu ya beach, lazima uonyeshe ya kwamba una resources ya ku-develop hiyo sehemu kama beach resort ama tourist resort. Tumeonelea kwa muda, kwa sababu nilitaja hao kwa kisiasa, mtu fulani anapewa, chukua acre ishirini, chukua acre kumi, chukua acre tano, halafu mtu anachukua hiyo ardhi anaenda kumuuzia mtu mwingine. Tunataka kusema, hali ya mazingara, hali ya maisha ya watu serikali haikujali. Tunataka Katiba ambaye itahakikisha ya kwamba when we move to market capitalism, we reduce the casualties both in human and ecological. Tunataka hiyo Katiba i-guarantee hiyo kwa hiyo mtu hawezi kupewa tu kwa sababu President anapenda, la.

Ya kwamba hata sisi pia tungetaka ownership ya ardhi, lakini iwe regulated, iwe inaenda sambamba na matakwa ya wanaanchi hawa. Tumeona sehemu za holding ground sisi ni wafugaji, na wafugaji tunategemea, wengi wa sehemu ya hapa ni wafugaji na northern kenya yote na walikuwa wakitegemea Kenya Meat Commission ama processing plants ambazo zimewekwa na serikali kutoka mkoloni. Inahakikisha ya kwamba wafugaji watakuwa na mahali ya ku-dispose of their livestock. Serikali imeenda ikapeana holding ground ambapo ulikuwa unaweka mifugo hapa ha unahakikisha hali ya diseases ya kwamba iko free na ugonjwa kabla haijaingia kwa soko kuuzwa. Kwa sababu ukichinja mnyama mgonjwa, unadhuru maisha ya wale wanaokula hiyo nyama. Tunataka Katiba hii ihakikishe ya kwamba serikali haitakuwa na uwezo wa kunyakuwa public utilities kama holding ground ambazo ni lifeline ya wafugaji wa nchi hii.

For instance mahali kama Farawa holding ground kumebaki sehemu kidogo. Kwa hivyo hizo ardhi ambazo zimenyakuliwa, holding ground ni maisha yetu, kuondoa acre moja inadhuru maisha ya mfugaji. Katiba ilazimishe serikali irudishe holding grounds kwa wenyeji wafugaji ili waweze ku market mifugo yao.

Lastly nataka kusema hivi, mambo ya electoral process, mimi napendekeza ya kwamba uchaguzi, time table ya Parliament itawekwa na Bunge yenyewe na kwamba haitaongeza siku moja wala haitapunguza siku moja kulingana na kanuni iliyowekwa ya kwamba uchaguzi utafanyika baada ya miaka mitano. No favour whatsoever na hata wakati huu tukizungumza, mimi nasema kazi ya Constitution Review Commission na mambo ya uchaguzi zichanganywe. Watu watatengeneza katiba waendelee hata itachukuwa hawa miaka mitatu au minne, bora watuletee Katiba kamili vizuri. Lakini ninasema uchaguzi uendelee kama ilivyo pangwa, neno kwenda kuongezewa mwezi, miezi miwili zaidi kuliko ile mumeahidiana na wananchi wangu, sitaki. Kwa hivyo nasema, Constitution Review Commission iendelee na kazi yake mpaka wakati ambapo, na ndiyo hiyo Katiba mpya ilisema, kwamba kama kuna review ya aina yeyote, isichanganywe na siasa ya kundi la watu au mtu binafsi.

Na kwa hivyo napendekeza in future, tuwe na President na Vice-President ambao hawatataka kura ya wananchi. Kwamba President, nataka nifaamike, kama mtu anataka kuwa raisi wa nchi hii, hakuna haja kwenda kutafuta kiti cha Bura, he should

just come out na anataka kiti cha President. Hii mambo ya President kusema lazima awe elected member of parliament, nataka iondoke katika katiba mpya. President na Vice- President, wajitokeze kule, wawache kiti cha Bunge, wapiganie urais na makamu. Wakishinda, wawe hapo. Wakikosa waende nyumbani. Lakini mtu amekosa President sasa anakuja hangaisha sisi katika Bunge, hapana. Hii ndio mapendekezo yangu.

La pili: Tuna concentration of powers mingi sana kwa President, kwamba yeye ndiye hata anateuwa ma-DO na DC na PC. Mimi naona Katiba mpya ipendekeze competence ya mtu ndio itampa promotion kupitia Public Service Commission, na miaka aliyotumikia serikali. Mbona ma-DO wametumika less than seven years wanakuja hapa kama ma DC na kung’ang’ana na wananchi wa kawaida. Competence and years of service should be the qualification kwa mtu kupata promotion kuwa DC, kuwa PC, kuwa Permanent Secretary.

Na kwamba Katiba mpya iseme, yule ambaye atateuliwa kuwa permanent secretary ama balozi, ama minister lazima apitie vetting ya parliamentary committee. Ndiyo tuseme tunakuwa na watu sawa, watu competent, watu watatumikia nchi hii kwa nguvu yao yote. Sio kwamba wewe unapenda mtu, mtu alikuwa kwa polytechnic jana, leoe ameingia Bunge kwa kusaidiwa halafu anakuwa minister. Sasa ile anafanya huko hakuna mtu anajua, hata PS hana uwezo. Mimi ninasema ministers must all be equal, must be answerable to the country.

Na mwisho ninataka Katiba mpya iseme, ikiwa mtu atashtakiwa kwa mambo ya hongo na corruption, ataenda mahakama na atajitetea, na ikiwa atapatikana na hatia, hatakaa kwa kazi ya serikali tena ataadhibiwa kulingana na sheria iliyowekwa, na hatashika ofisi ya serikali tena na hataingia siasa tena, hatakuwa diwani.

Shida tuliokuwa nayo nchi hii ni kwamba mtu atapelekwa ofisi fulani, atapora hii anaangusha, anatolewa pale anaenda kuwekwa ingine. Anaenda kupora hiyo, anamaliza, anaenda kupelekwa ingine.
Ninataka Katiba iwe ni ya haki kwa watu wa Kenya. Ikiwa mtu amekuwa implicated through public account or public investment, or any other agency, aonekane huyu kweli amehusika na mambo ya rushwa na hongo, wizi, asishike ofisi yoyote ya serikali tena na apelekwe mahakamani na mahakama imwadhibu kulingana na sheria iliyowekwa.
Hayo ndiyo maoni yangu na ninawashukuru sana, nitawapa watu wengine nafasi. Asanteni.

**Com. Mutakha Kangu:** Asante Mheshimiwa.

(Applause)

**Com. Mutakha Kangu:** Basi kuna Musilima Yusuf, huyo ni observer, Musilima Hassan, pia yeye observer, Habiba Mohamood, observer, Edward Munga, observer, Hawah Aden, observer, tupate D. Man.

**Diman:** Mimi kwa jina ninaitwa Diman.

**Com, Mutakha Kangu:** Diman ee, endelea.

**Diman:** Nikitoa maoni yangu ninaanza na muundo ya Katiba ambayo tungeitaka: Ninatoa maoni ya kwamba Katiba yetu ianze na jina la Mwenyezi Mungu na hivyo hivyo, Katiba yetu iwe ni katiba isiyo na aina yoyote ya domination.

Nikizungumzia kuhusu human rights, ninasema serikali iwapatie wananchi wake vile vitu ambavyo tunaita basic rights au basic needs kwa mfano maji, chakula na malazi. Hiyo iwe ni jukumu la serikali. Pia katika sehemu hizi zetu ambazo watu wanaishi chini ya poverty line, elimu ya msingi na elimu ya secondary ifanywe lazima na serikali isimamie hiyo elimu.

Katika kushughulikia usawa wa wanawake na wanaume, kuwe na hatua madhubuti ambao ichukuliwe. Kusiwe tu na maneno ambayo yanasemwa bila kuitenda.

Katika hali hiyo hiyo, nasema kwamba kuna aina zingine za mila ambazo zinagandamiza. Kwa mfano, pale ambapo wasichana wanatahiri na pia hali ya wanawake kumilikiwa, kuwa inherited kama kwamba ni vyombo. Mila kama hizo ziachwe.

Katika system of government ninapendekeza ya kwamba Kenya ikubali muundo wa serikali sawa na ile ya Ufaransa.

Na pia ninasema ya kwamba powers za President isiweko katika dissolution au prolonging of Parliament.

Ni vyema iangaliwe retirement benefits za ma-President, wale ma-Presidents ambao wamepita, yule President ambaye yuko na wale Presidents ambao watakaokuja, retirement benefits zao ionyeshwe na ijadiliwe katika Katiba hii mpya.

Ninatoa pendekezo ya kwamba Kenya iwe na chamber mbili ya Parliament. Moja iwe inachagua watu moja kwa moja kulingana na uwingi wa watu. Chamber ya pili iwe inasimamia jamii au makabila ndogo ndogo kama vile Wasanye ambao hawangeweza kupeleka mtu wao Bunge kwani jamii kama hiyo kutoka Kenya ijipatie uhuru, hakuna mtu wao aliyewahi kwenda Bunge. Kwa hivyo kuwe na chamber kama hiyo ambayo inashughulikia jamii au makabila ndogo ndogo na pia special interest group kama vile the disabled or other disadvantaged persons like the pastoralists.

Ninazungumzia the electoral system: Ninatoa maoni yangu nikisema kwamba ni vyema tungeangalia uwezekano ya kuwa na muundo ambao utapunguza hii hali ya makabila kupigania nafasi ya kupeleka mmoja wao Bunge au nafasi ya kila kabila kupigania ile nafasi ya kuwa Rais wa nchi.

Nikiwa ninazungumzia hiyo hiyo point, ninasema mimi ninaunga mkono kifungu ya sheria kinachosema asilimia ishirini na tano ya

kura lazima ipatikanwe na mgombezi wa Rais iwapo anataka kuwa Rais wa nchi hii. Kwa hivyo ninasema kwa maoni yangu, hiyo kifungu ya sheria iwe retained.

Ninazungumzia constitutional role of political parties: Ili kulinda utengamano miongoni mwa kabila ambazo wako hapa nchini, ingekuwa ni vyema iwapo tutakuwa na vyama viwili pekee yake.

Iwapo ninazungumzia devolution of powers, ninasema kwamba ni vyema iwapo serikali ita-maitain its present unitary system for the sake of national unity.

Nikizungumzia kuhusu national unity and ethnic diversity, ninatoa maoni yangu ya kwamba kungekuwa bora kama kungekuwa na muundo wa kupiga kura ambapo haitafanya hii hali ya ukabila iwe nzito kwa mfano, pengine kama katika zile constituency ambapo kuna makabila mengi ambao wanaishi, ili mtu achaguliwe kuingia Bunge, inafaa huyo mtu apate kura nyingi kutoka kila kabila, siyo kwamba apate kura ya kabila yake pekee ili aweze kwenda Bunge.

Nikizungumzia point hiyo hiyo, ninasema ni jukumu la serikali kuinua lugha za minorities. Kuna watu ambao lugha yao haiwezi ikafundishwa katika shule za msingi na inafaa maanake kuna hatari ya kwamba kugha kama hizo zitakuja kupotea. Kwa hivyo ninatoa maoni kwamba katika hii Katiba mpya, serikali ijihusishe na kuchapisha makala za hizo lugha na kusimamia gharama ya hizo lugha kufundishwa katika shule za msingi mpaka class ya nne.

Nikiendelea ninasema kwamba ile hali ya watu kuchaguliwa katika maofisi makubwa makubwa ni lazima izingatie jambo moja; the case of the historically disadvantaged minorities especially among the pastoralists.
Hawa watu hawana nafasi ya kuchaguliwa katika vyeo mbali mbali kwa sababu wao hawana watu katika serikali hii yetu. Kwa hivyo watu kama hao wakati inaposemekanwa kwamba mtu awe na qualification fulani ili achaguliwe awe katika cheo fulani, watu kama hao wasipewe masharti kama makabila yale mengine. Kwa mfano hapa, wa-Orma hawajasoma kwa hivyi siyo lazima m-Orma awe na degree ili achaguliwe katika cheo fulani.
Sababu (Jukumu) ya wa-Orma kukosa elimu ni ya serikali kwa hivyo serikali isitumie vile vitu ambavyo ilitumia kugandamiza hii jamii ili kuwagandamiza zaidi kwa kutowapatia nafasi kuwateuwa katika vyeo vikubwa vikubwa.

Nikizungumzia zaidi nasema hivi: Kuna mapendekezo ya kwamba watu wawe na kiwango fulani ya elimu. Mimi ninatoa maoni yangu ya kwamba kwa vile jamii yetu hawakusoma, masharti kama hayo yasikuweko, viongozi wetu wawe councillor, wawe ni wabunge, bora mtu ajue kusoma na kuandika au mtu aweze kuzungumza kwa lugha ya Kiswahili, inafaa awe kiongozi wetu. Hiyo mambo ya kwamba councillor awe na standard eight, vitu kama hiyo isitumike katika jamii kama hii yetu.

Nikizungumzia hali ya anti-corruption: Hii mambo ya ufisadi imezidi sana. Mimi ninatoa maoni yangu ya kwamba kamati ya anti- corruption ambayo imekuwa pingamizi kubuniwa hapa nchini, iundwe kutokana na watu wa ma dini. Tuseme katika jamii

ya Kiislamu kutolewe ma sheikh fulani na kutoka Wakristo pia kuchaguliwe watu fulani ambao wako na msimamo katika jamii ya wanaheshimiwa.

**Com. Mutakha Kangu:** Jaribu kumaliza.

**Diman:** Katika hali ya kumalizia kuna jambo moja: River Tana, mto Tana, imetumiwa kama pingamizi na watu fulani kama kwamba hiyo mito wanaimiliki. Kwa hivyo mimi ningesema itolewe, ninatoa kama maoni yangu katika Katiba hii mpya, iwe maji ya mto Tana ni haki ya kila mtu na siyo mali ya mtu mmoja au mali ya watu fulani.

Nikiendelea zaidi ninasema kwamba, iwapo tuchukulie jamii yetu hawakupata nafasi ya kusoma, basi sasa tupewe nafasi ya kujiunga na national schools. Ninasema kila kabila wapewe percentage fulani ya ku-join hiyo national kutegemea idadi yao. Iwapo sisi tuta-form one percent ya Kenya population, basi na sisi tupewe asilimia at least mmoja wetu aweze kuingia na kusomea kwa national school.

Hali ingine pia ninazungumzia habari ya boarding schools. Ninasema ya kwamba ni vyema iwapo serikali itachuka jukumu kujenga boarding schools kama ilivyoahidiwa hapo mbeleni katika wilaya hii yetu maanake hiyo ndiyo suluhisho la pekee ambayo itaweza kufanya watu wetu kusoma vizuri.

Na hali ingine ya elimu nikiongezea, katika jamii yetu ambapo hakuna waalimu, tungepengependelea ya kwamba Katiba isingatie sana kwamba hii hali ya uajiri wa walimu kutoendelea, hiyo kitu isitumike kwa jamii ambao wamekuwa historically disadvantaged kama hii jamii yetu.
Asanteni.

**Com. Mutakha Kangu:** Na Elizabeth Njenga ni observer, Dhahir Bile, pia yeye ni observer, Johana Saitoti, pia yeye ni observer. Kuna list ingine hapo? Hebu leta. Wes Dhahir, observer, Ali Dhahir pia ni observer, tupate Ismael Osman, unataka kuzungumza au hapana? Asante basi. Hussein Gure, observer, Mohamud Balagha, yuko wapi? Haya! endelea Bwana Mohamud.

**Mahmud Balagha:** Asante sana. Nitaanza mara moja vile ningependelea.

**Com. Mutakha Kangu:** Taja jina Mzee.

**Mzee Balagha:** Mimi ninaitwa Mahmud Balagha.
Ningetaka Katiba yetu ya wakati huu, hii tunayotengeneza, kwanza iwe na jina linaloonyesha kuwa ni yetu yenyewe tunamiliki, yaani iwe na umilikaji kwa mfano sisi Wakenya tumeamua hivi na hivi, iwe ni hilo inaanzia kwa Katiba yetu.

Halafu nikisonga mara moja kwa yale maoni ambayo niko nayo: Maoni yangu ningesema kuwa katiba hii iwe kama ile, siku ile tumepata uhuru, Katiba kama hiyo tuifanyie marekebisho hivi; kwa mfano, upande wa urais tunaona kuwa kweli tunachagua rais, mkuu wa nchi, kakini tungeweka viwango kuwa rais akichaguliwa kwa mfano, aanzie miaka arobaini mpaka miaka sitini. Zaidi ya hapo,huyo ni mzee,asipewe hiyo jukumu ya kuongoza taifa.

Ningependelea katika Katiba, Rais wa nchi asiwe kiongozi wa serikali, yaani tuwe na Rais na Waziri Mkuu ili tusifanye Rais awe na kila kazi, yaani upande moja ni Rais, upande mwingine ni kiongozi wa chi ama wa serikali, hapo inaleta shida maanake anakuwa na kazi nyingi zaidi ambazo sasa ikipata mtu ambaye hana ujuzi, anaweza kuharibu nchi.
Kwa hivyo ingekuwa ni maoni kuwe na ofisi ya Waziri Mkuu na pia kuwe na Rais wa nchi ambaye kazi yake itakuwa, tumwite kama ceremonial na huyu Waziri Mkuu awe ndiye yule ataenda kuomba kura kwa wananchi. Wakati chama chake kimepata asilimia hamsini na moja, basi waziri mkuu kama huyo apewe ile uwezo wa kutengeneza serikali.

Upande huu wa Waziri Mkuu, tukiangalai sehemu kama hii yetu nikifafanua kidogo, kama tutaenda na mwenendo ule tukonao wa serikali kubakia Nairobi pekee yake, tutapata shida sehemu hizi maanake wakati tutakapokuwa na waziri mkuu, tungependekeza pia tuwe na jimbo.

Tukiangalia wilaya yetu ya Tana River, haya mizozo yote mnayoyaona inaletwa kwa sababu zile rasilmali zinazotumwa, wananchi hawazipati kwa kitu kimoja; managers huwa si wakaaji wa area hii. Kukitokea tender, hiyo tender, kwa vile managers si wa hapa, wanapatia watu wao. Kwa hivyo ukiangalia ile rasilmali ambayo sasa ingekuwa ni ya eneo hili, inarudi tena. Kwa hivyo kama tungekuwa na jimbo, serikali yetu iwe ya majimbo, bila shaka ule mfuko unaotumwa kwa sehemu kama hii yetu, wakaaji wa jimbo hilo wangefaidi.
Ndiyo maoni yangu. Tuwe na serikali ya majimbo.

**Com. Mutakha Kangu:** Ongeza ingine kama iko, hiyo tumesikia.

**Mr. Balagha:** Nyingine, pia wakati tunafanya uchaguzi, tukichagua, kwa mfano tumechagua Rais, tumechagua mbunge, kuwe na namna hawa watu wanaweza kuadhibiwa kama hawatekelezi jukumu lao. Kwa mfano mjumbe, kama miezi sita ama mwaka mmoja, mjumbe wa kwako haujamsikia jina likitajwa, iwe wakaaji wa eneo hilo wawe na nguvu fulani katika Katiba hii tutakayoanzisha na njia ya mbunge kama huyo kuchukuliwa hatua.

Lingine ni upande wa mahakama: Tukiangalia mahakama yetu hayako huru. Pale mwazo mahakama yalikuwa huru. Wakati huyu jaji mkuu, kulikuwa na tume ambayo ilikuwa na nguvu ya kumchagua huyu na watu wa mahakana. Kwa hivyo ni pendekezo langu pia ile ile tume iwe na nguvu ya kumchagua, isiwe anachaguliwa na waziri ama yeyote yule ambaye amechaguliwa na kura. Pia wakati anatajwa, Rais nguvu yake iwe ni kupendekeza jina la huyo…

**Com. Mutakha Kangu:** Wewe unapendekeza hawa watu wawe wanachaguliwa na nani badala ya Rais?

**Mr. Balagha:** Mimi ninapendekeza hawa watu wachaguliwe na Bunge baada ya Rais kuwapendekeza, Bunge liwafanyie vetting hawa watu mpaka hata kwa DC.

Jambo lingine ni kuweka sheria hasa hii mambo ya mto. Tukiangalia, mito mingi iko na sheria lakini mto wetu wa Tana River, ama huu mto unaoitwa Tana River, tunaona sheria ya sasa haipatii, ama hakuna sheria inayomlinda yule ambaye yuko chini ya huo mto. Mto unaanzia juu ikiwa tributary lakini ukifika upande huu hakuna sheria. Kwa hivyo kuwe na sheria ya kusema level ya huo mto usipungue kwa kiwango fulani ili wale wanaotumia huyo mto upande huu kwa kunyunyizia maji, wapate fursa ya kutumia huo mto bila kusumbuliwa maanake tunaangalia mto, ukiangalia wakati kumejaa, sijui ma dams zao zikijaa, mto unafunguliwa bila hata notice, hata hakuna simu ya kusema sasa maji upande huu imejaa, wacha tufungulie.
Inafunguliwa vile wanavyotaka, haya mambo tumeona kuwa yanaathiri maisha ama hali ya maisha ya wakaaji wa area hii maanake kunakuwa na mafuriko kwa hivyo mapato yetu yanakuwa kidogo kwa sababu ya hiyo. Kwa hivyo kuwe na sheria ile itakayowekwa kusema mto huu, level ya maji yasipugue kiasi fulani.

Labda ni hayo tu Bwana Commissioner.

**Com. Mutakha Kangu:** Asante sana. Nenda uweke sahihi hapa Mzee, pale pale. Wa mwisho ninaona John Ngugi alisema ni observer. Yakob Gunyo? Na Mzee uharakishe. Endelea.

**Yakob Gunyo**: Maoni yangu ya wazee katika Bura division ni machache, nitaweza kuharakisha lakini.
Maoni ya kwanza: Kwa jumla ya maoni ya Tana River mzima, sisi wakaaji wa Tana River, tuna vitambulisho vya Kenya lakini haifanani na ya Kenya, ni kama sisi si raia wa Kenya maanake hakuna sheria.
Viongozi popote anatoka mahali ya sheria, wote kama wanafika hapa Tana River, wanakaa kama wale watu wanachunga mbuzi, wanatuongezea zaidi ya shida yetu.

Kitu ninaomba katika Katiba ya mwaka huu mpya, sio serikali itufanyie kama tuko Kenya ingine. Shida yoyote ya Tana River sisi tunashindwa kutoka maanake hakuna mtu yeyote anakuja kutoa sisi au anaeleza sisi vile Kenya ingine inaendelea. Sasa kama ilikuwa sisi hatujapata hiyo Katiba ya mbele, sisi watoto wetu na wabunge wetu watuonyeshe kama sisi ni wa Kenya ingine.

**Com. Mutakha Kangu:** Haya! Enda kwa lingine.

**Mr. Ghuno:** Sasa maombi yangu katika hiyo Katiba, tafadhali sheria ya Kenya hakuna ndani sisi iko kitambulisho ya Kenya

pekee yake. Tafadhali tujulishe tuonyeshwe njia ya sehemu zingine ya Kenya.

Sasa iko shida watu wengine wasio wa Tana River wanaleta shida nyingi hapa, hata kama sisi tunazungumza, ama tunakuja kumwambia huyo kiongozo yetu, hakuna hatua yoyote. Sisi tumeshindwa mahali tunapeleka hiyo shida yetu.

Hao watu wanaotoka mahali ingine kuja hapa, kama sisi tunawaambia wao ni wageni, wanasema sisi si wageni wenu, hii ni nchi ya Kenya. Ni nchi ya Kenya lakini hiyi ardhi yako ni hiyo nchi yako ni kama shati yako lakini watu watoka nchi ingine kama waingia hapa, sisi tunalalamika, wanasema sisi tumekuja Kenya, hatujakuja kwenu, hapa si nyumbani kwenu.

Tafadhali mtueleze kama sisi tuko kando ya Kenya, ni kitambulisho tu pekee yake unakaa nayo kama ng'ombe, Katiba itueleze.

Tufufuliwe hiyo shamba yetu ya Bura. Vile sisi tunakosa, sasa serikali inatuambia tufufukishe hiyo shamba, hata sisi tufufukishiwe kama Kenya ingine. Sina maoni mengine, asanteni sana.

**Com. Mutakha Kangu:** Asante basi Mzee. Weka sahihi hapo. Wa mwisho, basi tusikize, wacha kelele. Mtu wa mwisho kwa list hapa ni Kuso Adan.

**Kuso Adan:** Mimi nitaongea lugha ya Kisomali ama ya Kiorma.

**Com. Mutakha Kangu:** Unataka kuzungumza Kiorma?

**Kuso Adan:** Kiorma ni Kisomali, yote ni sawa.

**Com. Mutakha Kangu:** Nani atatutafsiria, nani anaelewa Kisomali? Nani atatusaidia? Kuja ndugu, kuja utusaidie. Na wengine wanyamaze. Haya! Basi.

**Kuso Adan:** (Speaks in Somali dialect) Aniga sual ban qawa.

***Translator:*** Yeye ana swali.

**Com. Mutakha Kangu:** Ataje jina kwanza.

**Kuso Adan:** Kuso Adan. Waxan rawa in an ogatho sharciga Kenya xaqa binaathmaka in u mit yaxay ama lawa.

***Translator:*** Katika sheria ya Kenya, haki ya binadamu ni moja au si moja?

**Kuso Adan:** Qofka tajirka eh iyo qofka maskin eh iney isku xaq yixin yan rawa in an ogatho.

***Translator:*** Tajiri na maskini wako na haki moja?

**Kuso Adan:** Mit ka aqristey iyo kan aqris laanta eh iney isku xaq yixin yan rawa inana kalaogatho.

***Translator:*** Mwenye amesoma na mwenye hajasoma wako na haki sawa?

**Kuso Adan:** Sababta lawa qof xathey thambi qaawan ey dhowlada Kenya ey qawato.

***Translator:*** Wawili wakiwa na dhambi, yaani wamefanya kosa na serikali iwashike,

**Kuso Adan:** Ninki lacag lagaxelo dhowlada wey sithaysa kikalana wey maxkamaeysa.

katika serikali ya Kenya mwenye anapatikana ako na pesa anawachiliwa na asiye na pesa anapelekwa kotini.

**Kuso Adan:** Polista kenyana nninku qabto maxkamath umamothiyan ila sethax wik lacag bey kusugayan.

***Translator:*** Police wa Kenya wakiwashika watu, hawawapeleki mahakamani haraka, wanakaa nao karibu wiki tatu wakingojea pesa.

**Kuso Adan:** Mathax thena xath uimato xata waraq dalasha oo ilma kumabuxinayan ila ey ama wax kaxelan ama qof aqristey xathatha taxay maogiye.

***Translator:*** Kila ofisi ukienda, hata ile barua ya kuzaliwa, ukitaka kujaziwa ile form ya kuzaliwa, ni mpaka utoe kitu, hautatimiziwa haki yako. Mpaka uwape kitu kidogo.

***Kuso Adan:*** Xasa anaga dhadki xola daqatatha oo thurka an naxay.Wax musacitha na dhowlada kaxelney majirto.

**Translator:** Hasa sisi tukiwa wafugaji , hakuna haki tunapata katika serikali ya Kenya.

***Kuso Adan:*** Waqti kasta waxa xolaxa dacaa tug.

***Translator:*** Wakati wowote kuna wezi wale wanapora mali za wenyewe, kuiba ng'ombe kwa mfano,

***Kuso Adan:*** Aniga xatha meshan kaimathey konton killomita bey jirta.

mahali ametoka ni Welesonreak, karibu kilomita hamsini, hajui kilomita yenyewe lakini huwa anasikia ni fifty kilometers.

***Kuso Adan:*** Makasai sas uban maqla moogiye. Xathi xolaxa lagaqatho oo meshan ath casir imato mpaka kesho bey kudaxayin dhowlada.

Anasema ng'ombe wako wakiibiwa, ukiotoka pale kuja kupeana ripoti, polisi wanasema mpaka kesho tena.

**Kuso Adan:** Beri salathi xath reportka kanthith mutha sathax saqathoth reportka bey kaqarayin.

***Translator:*** Tena ukileta hiyo ripoti asubuhi tena, muda wa masaa matatu wanaandika ile statement yako,

***Kuso Adan:*** Wexey kuweythinayin cathowgi xolaxatha qathey ama aw dhadki daqacay imisuaxa

wanakuuliza wale watu waliiba ng'ombe wako na kuua watu wako walikuwa wangapi?

***Kuso Adan:*** Silaxatha ey waten nocmey exeth.

Walikuwa na silaha aina gani?.

**Com. Mutakha Kangu:** Sasa yeye anapendekeza namna gani?

***Translator:*** Marka athi maxath lethaxay.

**Kuso Adan:** Waxan weythinaya xaqa in umit yaxay ama lawa.

***Translator:*** Anauliza, yeye anasema haki kama ni moja au si moja.

**Com. Mutakha Kangu:** Unajua vile unasema, umetueleza, inaonekana kama hakuna haki sawa na wakati tunataka tutengeneze Katiba inaweza kupeana haki sawa, sasa wewe utupatie ni mambo gani inawezawekwa kwa Katiba yenye inahakikisha nyinyi mnapata haki sawa.

***Translator:*** Marka wuxu kudaxat wan ognaxay xaqa in uxalko exen marka athi maoniga ath baxsanni xaiso sitheth rabta in uaxatho ama lobathalo.

**Kuso Adan:** Waxan rabna sikasta oo anaga nalugusacitheyni karo dhowlada iney ogato xaqa iyo waxan kunolnaxay.

***Translator:*** Njia yoyote serikali ina weza kutoa huduma za wafugaji ili serikali itoe.

**Kuso Adan:** Xata waxa jirta ….(gap cos of end of tape)

***Translator:*** Wao wakipita, vile wako kwa hiyo barabara, yule mtu anakuta ndiyo wanampea tu chanjo, hawaingii ndani ndani hakuna mtu anajua habari zao.

**Kuso Adan:** Dhadki thurasha kujirey nin wax kaog malaxa, dhadki xanshimaxa aqriyena waxa kuqoron bey nadexen wain guri kasta latago.

***Translator:*** Na ukisoma katika zile karatasi vile wanaandika ile maandishi yao, wanasema ni lazima wafike nyumba kwa nyumba.

**Kuso Adan:** Marka anaga waxan dhoneyna xaqa xathu mit yaxay.

***Translator:*** Saa hiyo wanasema *kama* ni kweli haki ni moja,

***Kuso Adan:*** Jitki nalugusacitheyni laxa ban rabna inan ogano.

njia yoyote ile serikali itatusaidia, tunataka tuipate.

**Kuso Adan:** Mita kaley waxajirta anaga xolaxena xath io jerbo baxal bacuna.

***Translator:*** Sisi tukiwa wafugaji, ng'ombe wetu huwa wanaliwa na wanyama

***Kuso Adan:*** Xolaxana walairaxtha dhowlada aya iskaley.

na hawa wanyama wanasemekana ni wa serikali.

***Kuso Adan:*** Nin an repot ukeneyno ama arkeino malaxa anaga.

***Translator:*** Hakuna mtu tunaona akija kudai wale ng'ombe wetu.

**Com. Mutakha Kangu:** Wale wanapiga kelele jaribu kukimya, kama utaki kukimya, uende nje pole pole. Haya! Endelea Mzee.

***Kuso Adan:*** Marka maaragno wax xolaxana nagaqabsanayo ama nasacitheynayo xolanana baxal bacuna.

***Translator:*** Na wale wanyama, simba akila wale ng'ombe wako, ukiuwa yule simba, serikali wanadai umeuwa simba na hakuna fidia yoyote tunapata kutoka kwa serikali, hata pahali pa kupeleka ile ng'ombe yetu sisi hatuoni.

***Kuso Anan:*** Jitkasta o nalagusacitheyni karo anaga wan ogalnaxay.

***Translator:*** Njia yoyote serikali inaweza kutusaidia nayo kuhusu hawa wanyama, ili watenge ile wanyama wao na na sisi tupate fidia ya ng'ombe wetu.

***Kuso Adan:*** Mathathenana xola jiran oo safar bey wadhanka mariyan.

**Translator:** Ng'ombe wanatolewa pahali pengine bila ya afya yao kuangaliwa na wanapita katika Tana River hii yetu hii

***Kuso Adan:*** Anagana waxan kaognaxay majirto.

na sisi tukiwa ni wananchi wa hapa, wakaaji wa hapa Tana river, hakuna kitu tunajua.

**Kuso Adan: Shida umbey anaga markasta nokenan xolaxanaga markasta kudinta.**

**Translator:** Na hao ng'ombe wagonjwa wakati wamepita, ile shida wanawacha tu hapa Tana River, na ng'ombe wanakufa.

***Kuso Adan:*** Ninki looatha watey lamaxathli kartith lakini mathaxtha yu waraq kawata.

***Translator:*** Na yule mwenye ng'ombe saa hiyo hiyo hauwezi kuongea na yeye kwa sababu amepata barua kutoka kwa maofisi.

**Kuso Adan:** Marka maonnigega waxa wayey dulka,

***Translator:*** Maoni juu ya ardhi iwe iko katika mikono ya wananchi,

***Kuso Adan:*** Iney dhowlada ey iskabitisheynanin waxan dhowlada ey wananchiga kunol imet weythiyo xathi dul lasinayo xathi xola labixinayo ila ayaga ey ralii kunoqythan

si eti serikali inapitisha tu, wale wenyeji wanakaa waulizwe hata kama ni ng'ombe Wanapita, kama ni haki ingine ya kulinda ng'ombe, iwe ni wananchi ndio wanaulizwa.

**Kuso Adan:** Xathan firino waxalairiy ninkasta Kenya uhuru bu qawa.

Tukiangalia tunaambiwa ya kuwa Kenya kila mmoja ako na uhuru.

**Kuso Adan:** Lakin xathan sas ufireini xolaxanaga io anaga iskuxisab umban naxay.

***Translator:*** Anasema tukiangalia sisi watu wa Tana River, anasema sisi na wale wanyama hayawani, wale tuko nao, kama ng' ombe wetu, tuko laini moja tu.

**Kuso Adan:**

***Translator:*** Kwa sababu tumeona hata serikali ya Kenya, jeshi ya Kenya, wakiwa wameuwa, hata polisi, ng'ombe wetu, kila mtu anajua, wamepiga risasi na hakuna kitu…

**Kuso Adan:** Xata wan aragney cithama Kenya ooxayawan thilen oo xabath kuduften.

***Translator:*** Hawa polisi wameuwa punda, wamepiga risasi na hakuna hatua yoyote imechukuliwa na ripoti wenye kuletewa ripoti na hao hakuna njia ile unaweza pitisha ile ripoti yako.

**Kuso Adan:** Xata axata thamey bey thilen wax waxnogaqawano malaxa. Waxan umaleyni anaga berkena usan sharci jirin.

***Translator:*** Sisi tumefikiria ya kuwa sisi hatuko katika sheri ya Kenya.

**Com. Mutakha Kangu:** Asirudie ile yenye amesema. Ile imebaki (Inaudible)

**Translator:** Wax kaley sheg.

**Kuso Adan:** Sikasto o nalugusacitheyni karo wan rabna anaga.

***Translator:*** Njia yoyote tunaweza ile tunaweza saidiwa nayo tunataka.

**Com. Mutakha Kangu:** Tumemaliza yale majina tulikuwa nayo na ningetaka kufikia kiwango hicho tuelekee kumaliza mkutano na nitauliza district coordinator Bwana Omar Dhato atumalizie mkutanao na utaratibu aliyonao.

**Omar Dhato:** Asante sana Chairman wa mkutano wa leo, Commissioner Mutakha Kangu, Professor Idha Salim, Mheshimiwa Mbunge wa sehemu wa uwakilishi bungeni ya Bura Bwana Muhammad Galgallo, viongozi wanaowakilisha utawala wa mkoa, viongozi wa kisiasa, ma councillors, viongozi wa tabaka mbali mbali na wananchi kwa jumla. Tunashukuru kwamba tumefika ukingoni mwa mkutano wa leo.

Tungependa kuendelea lakini na watu ambao kwamba wameandikishwa pia nao wameisha, kwa hivyo kwa kweli ma-Commissioners leo wamekuwa wavumilivu na wamesikiza maoni ya watu wa Bura kwa makini, hawakuwa na mahali popote pa kwenda mpaka mtu wa mwisho asikizwe na hivyo ndivyo mambo yalivyokuwa.

Kwa hivyo hatutawalaumu kwa kusema pengine walikuwa na haraka ya kwenda mahali popote kwa sababu tuko na wao na kama watu bado wangekuwa wapo, pia tungezidi kuendelea kuwasikiza. Kwa hivyo tunawashukuru sana Commissioners kwa

kazi mmefanya ya kutembea tena kwetu, karibuni safari nyingine na pia hasa Commissioner Mutakha Kangu kwa kujaribu kuja kulala Bura kwa sababu tulifikiria watu wengi hawapendi sehemu hii lakini yeye anaonekana ako na mahaba na watu wa Tana River, kwa hivyo tunashukuru sana.

Commissioner Idha Salim ni mara ya pili kuja na tunawakaribisha kila mara watutembelee hata Tume itakapomaliza kazi. Ningependa basi kutoa shukurani na tangazo moja ambalo litakuwa ni muhimu kwa Commission na pia Mheshimiwa Mbunge yuko hapa, kwa hivyo ni nafasi nzuri sana kurekebisha yale mambo ya kamati yetu ya sehemu ya uwakilishi bungeni.

Tulikuwa na kamati niliyoitangaza wakati nilipochukua hatamu za kuzungumza, wakati wa kuaza mkutano, kamati yetu ya sehemu ya uwakilishi bungeni alikuwa ni Mheshimiwa Muhammad Galgalo, Salat Gharaja, Chairman county council, Omar Dhatho, coordinator, Mahamud Wario, Hawa Luli Aden, Elizabeth Wanjiku, Jilo Zakaria, Maramba Hussein, Jamila Salat Wato na Madam Johora Omar, lakini wawili wame-resign kama nilivyosema, mmoja alifariki na mwingine ameshindwa kufanya kazi sehemu ya Bura.

Kwa hivyo kwa sababu hiyo imebidi tufanye mabadiliko na hayo mabadiliko tuliondoka na Mheshimiwa tukaenda kuangalia na lile ambalo hakulikubali pia tumelirekebisha ili tuwe pamoja ndio tu-submit hii list kama official list kama official list ya kamati yetu ya sehemu ya uwakilishi bungeni ya Bura. Kwa hivyo kamati yetu mpya ambayo imekubaliwa sasa na Mheshimiwa na mimi na tutaipatia Tume, itakuwa Mheshimiwa Mbunge wa Bura Bwana Muhammed Galgalo, Salat Gharaja, Chairman wa County council ya Tana River, Omar Dhatho, coordinator, Mohammed Wario, ambaye atakuwa anawakilisha vijana, Hawa Luli Aden, ambaye ni mwanachama, Elizabeth Wanjiku, anayewakilisha wakulima na Noor Mohammed anayewakilisha jamii ya Wata, Wata Community. Tuna Aden Ibrahim Arale, atakuwa akiwakilisha watu wa sehemu ya Bangale,tuna Osman Abatano, atawakilisha sehemu ya Madogo na Hassan Bagana atakuwa akiwakilisha jamii ya Malakote kwa hivyo kamati hii tumejaribu kufikia kila sehemu ya constituency hii na kila jamii pia ihusishwe katika mambo ya Katiba.

Kwa hivyo hii ndiyo kamati yetu sasa mpya ambayo tutawaandikia barua wale wapya ambao wameingia ili na wao wajiunge na kukiwa na shughuli zingine baada ya leo, pia na wao watakuwa ni wanachama. Kwa hivyo hii ni official list sasa ambayo nitapatiana kwa Tume.

Basi, mtaniwia radhi kwa kuzungumza mambo mengi, mkutano sasa umefika mwisho na kama nilivyosema, hatukuweza kupatiana pesa za haina yoyote kwa mfano kama allowance ama bus fare kwa wale watu ambao wamekuja kushiriki kwenye mkutano lakini mipango ya kamati yenu ya sehemu ya uwakilishi bungeni ya Bura, tulikaa kikao tukasema watu wetu ni watu wanashida nyingi, wanatoka sehemu mbali mbali na itabidi baada ya mkutano warudi huko, kwa hivyo tuwatayarishie kitu ambacho watashikilia tumbo wakati watakapokuwa wanaenda. Kwa hivyo iko mchele mwingi, wali umepikwa, pilau, kwa hivyo kile ambaye amehudhuria ahakikishe amepata chakula, ndipo muweze kurudi nyumbani.

Tungeweza kufanya zaidi lakini kwa sababu ya ukosefu wa pesa, hatukuweza kumpa kila mtu shilingi mbili, ishirini ama mia moja, hatukuweza lakini chakula kamati imesema tuandae kwa ajili ya wale ambao wamehudhuria mkutano. Kwa hivyo tutakula pamoja na Commissioners na Mheshimiwa, hawaendi mahali pengine kula watakula hapa hapa ndio wapate nafasi ya kuondoka.

Kwa hivyo ningeomba sasa mzee mmoja, sikuwako mwanzo wa mkutano, sijui nani aliomba, kama ni Mkristo ama ni Mwislamu.

**Com. Commissioner:** Alikuwa Mwislamu.

**Dhatho Omar:** Basi tutapata ndugu wetu Mkristo mmoja ambaye ataweza kuja kutufungia mkutano mkutano wa leo kwa maombi. Kwa hivyo yeyote yule ambaye yuko tayari aje mbele na ukija useme jina ili uweze kurekodiwa, tujue mkutano wa Bura wewe ndiwe umetufungia kazi.

Kwa hivyo nawashukuru kila mmoja ambaye ameshiriki kwenye mkutano na ninawaombea heri mrudi salama na Mwenyezi Mungu awabariki. Asanteni.

Asante. Mimi nitaiwa Johana Ekuru lakini kwa upande wa Wakristo.

**Prayer:** Baba ni asante Mungu wetu mtakatifu na mtakatifu. Bwana ni asante kwa wale viongozi walikuja hapa Bwana, Bwana ni asante hata kwa Katiba ya nchi Mungu. Mungu tunakabithi baraka zako kwa hiyo Katiba Bwana, Bwana iwe Katiba yenye kulinda wananchi wa nchi hii Bwana.

Bwana iwe ni Katiba yenye baraka ya kulinda watoto wa nchi hii Bwana, Bwana iwe Katiba yenye umuhimu wa kulinda Bunge yetu ya taifa hii Bwana. Bwan iwe katiba yenye baraka ya kulinda Rais wa taifa hii Bwana. Bwana tunaomba Mungu na upate kubariki kila mmoja aliyeweza kuja kwa huu mkutano wa Katiba hii Bwana.

Bwana ni asante kwa sababu wewe ndiwe uliyeumba binadamu kupitia kwa mkono wako Bwana. Bwana na upate kubariki safari yao Bwana, Bwana upate kuandamana nao Mungu, Bwana pahali hawa watasimama Bwana uwe unasimama wao Bwana kwa sababu Bwana wametoka sehemu mbali mbali Bwana.

Bwana tunakukabithi kwa kuwa wewe ndiwe Mungu wetu Bwana, Bwana baraka na ipate kuanguka sehemu sehemu yetu ya Bura Bwana, Bwana mavuno mzuri na ipate kuanguka hapa Bwana.

Bwana tunaombea Mungu hata Bunge letu Bwana. Bwana na upate kulinda Bwana, Bwana tunahitaji uongozi bora kwa taifa hii Bwana. Bwana tunahitaji watoto wenye elimu taifa hii Bwana. Bwana ninakuomba, ninakuomba na kuamini katika jina la Yesu Kristo nakuomba na kuamini.

The meeting ended at 3.57 p.m.

*********************************************************************